# UCHANGANUZI LINGANISHI WA MASWALA YA VIJANA NA JINSI YANAVYOSHUGHULIKIWA NA WAANDISHI KATIKA DIWANI YA *TUNU YA USHAIRI*

**NA**

**ROSE NYAMEMBA**

**C/50/84035/2012**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**IDARA YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya Shahada ya aina yoyote katika chuo kikuu chochote kingine.

Sahihi……………………………………………….….Tarehe……………….…………

**Nyamemba Rose**

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi Walioteuliwa na Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Sahihi……………………………………………….….Tarehe……………….…………

**Prof. Rayya Timammy**

Sahihi……………………………………………….….Tarehe……………….…………

**Ms. Mary Ndung’u**

## TABARUKU

Kwa wazazi wangu James na Jane Nyamemba kwa kunipigania nipate elimu. Pia kwa mume wangu Robert ambaye alinitia moyo hadi mwisho pamoja na wanangu Hope na Hermonie.

# SHUKRANI

Utafiti huu si mchango wa mtu mmoja. Wengi walinishika mkono ili nifaulu. Hivyo sina budi kuwashukuru. Kwanza namshukuru Mola kwa kunipa uwezo wa kushughulikia kazi hii. Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Rayya Timammy na Ms. Mary Ndungu kwa ushauri na kuwa mhimili katika safari ya uandishi wa tasnifu hii. Mola awabariki.

Ningependa kuwashukuru wahadhiri wa Idara ya kiswahili ambao walinipa maarifa. Hawa ni Prof. Habwe, Prof. Mwenda Mbatia, Prof. Kineene wa Mutiso, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Bw. Mungania B.G, Dkt. Mbuthia na Dkt. Iribe Mwangi. Ninaomba Mola awazidishie maarifa na busara.

Ningependa pia kuwashukuru wanafunzi wenzangu ambao tumesoma nao tangu mwanzo hadi mwisho. Nao ni Judith Kemunto, Queen Ndoni, Nyandiwa Hudson, Gladys Kinyua, Peter kilonzo, Lydiah Shaviya, Julita Wanjala, Miricho Mutahi, Evaline Kanyange, Timothy Mukaria, Dinah Osango, Paul Sito, Otuoma Damaris, Zani Edward, Florah Omosa. Asanteni kwa kunifaa katika mijadala na kwa ushauri.

Sina budi kuwashukuru wazazi wangu James Nyamemba na Jane Nyansiaboka kwa kuhakikisha nimepata elimu nzuri na kunitia moyo wakati wote. Pia ningependa kumshukuru mume wangu Robert Arasa kwa kunitia moyo na kuwa mvumilivu wakati wote. Mola awabariki nyote pamoja na wanangu Hope na Hermonie. Labda sikuweza kutaja kila mmoja aliyenifaa kwa njia moja au nyingine. Kwenu nyote nasema asante sana.

# IKISIRI

Katika tasnifu hii tumeonyesha maswala ya vijana na jinsi yanavyoshughulikiwa na waandishi katika diwani ya *Tunu ya Ushairi* ambayo ina mkusanyiko wa mashairi ya waandishi wanne tofauti.Waandishi hawa ni pamoja na Andanenga, Nyanje, Kiponda na Arege (2013). Utafiti huu umeonyesha kwamba vijana wana changamoto nyingi katika jamii ambazo ni lazima hatua ya dharura ichukuliwe ili kuokoa kizazi kijacho. Tumeshughulikia mashairi kumi na saba ambayo tulichagua kwa kutumia sampuli lengwa. Katika utafiti huu, nadharia ya uhalisia imetumika kuonyesha ukweli wa mambo katika jamii. Ukweli huu ni ule ambao unaweza kuonekana na kuthibitishwa pasi na tashwishi yoyote ile. Nadharia hii ya uhalisia iliwezesha kuhakiki maswala ya vijana katika jamii na jinsi waandishi wa diwani ya *Tunu ya ushairi* wanavyoshughulikia maswala hayo. Maswala haya ni pamoja na elimu, ukosefu wa maadili, umaskini, magonjwa, ukosefu wa malezi bora na ukosefu wa ajira. Baada ya kufanya utafiti wetu kwa kina tuligundua kwamba ni kweli vijana katika jamii tofauti huwa na changamoto sawa. Pia makisio yetu kuwa waandishi wote katika diwani ya Tunu ya ushairi wana mwelekeo sawa kuhusu vijana ni kweli kwa sababu maswala wanayoyashughulikia ni maswala ibuka katika jamii na yanawahusu vijana.

## YALIYOMO

UNGAMO ..... ii

TABARUKU ..... iii

SHUKRANI ..... iv

IKISIRI ..... v

YALIYOMO ..... vi

KIFUPISHO ..... ix

**SURA YA KWANZA ..... 1**

1.0 Utangulizi ..... 1

1.1 Tatizo la Utafiti ..... 3

1.2 Madhumuni ya Utafiti ..... 4

1.3 Nadharia Tete ..... 5

1.4 Sababu za kuchagua Mada Hii ..... 5

1.5 Upeo na Mipaka ..... 7

1.6 Yalioandikwa kuhusu Mada ya Utafiti ..... 8

1.6.1 Maswala ya Vijana katika Ushairi wa Kiswahili ..... 9

1.6.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Maswala ya Vijana Katika Kazi Zingine ..... 12

1.7 Msingi wa Nadharia ..... 16

1.7.1 Nadharia ya Uhalisia ..... 16

1.8 Mbinu za Utafiti ..... 19

1.8.1 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli ..... 20

1.8.2 Ukusanyaji wa Data na mbinu za Ukusanyaji Data ..... 20

1.8.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ..... 21

1.9 Hitimisho........................................................................................................21

**SURA YA PILI:DHIMA YA USHAIRI, DHANA YA VIJANA NA MASWALA YANAYOHUSU VIJANA KATIKA JAMII...............................................................22**

2.0 Utangulizi........................................................................................................22

2.1 Dhima ya Ushairi Katika Jamii.......................................................................22

2.2 Dhana ya Kijana..............................................................................................24

2.3 Maswala Yanayowahusu Vijana katika Jamii ...............................................28

2.3.1 Matumizi ya Mihadarati na Ulevi..............................................................29

2.3.2 Ukosefu wa Elimu Bora............................................................................33

2.3.3 Ukosefu wa Maadili...................................................................................36

2.3.4 Umaskini...................................................................................................38

2.3.5 Maradhi ya Ukimwi na Magonjwa mengine ya Zinaa...............................40

2.3.6 Ukosefu wa Malezi Bora ...........................................................................43

2.3.7 Ukosefu wa Ajira .......................................................................................46

2.4 Hitimisho........................................................................................................49

**SURA YA TATU:JINSI WAANDISHI WANAVYOWIANA KATIKA DIWANI YA *TUNU YA USHAIRI*.........................................................................................50**

3.0 Utangulizi........................................................................................................50

3.1 Wasia/Onyo......................................................................................................50

3.2 Elimu...............................................................................................................60

3.3 Malezi .............................................................................................................63

3.4 Ukosefu wa Maadili.........................................................................................76

3.5 Ndoa na Mapenzi .............................................................................................83

3.6 Changamoto za Maisha kwa Vijana ....................................................................91
3.7 Hitimisho....................................................................................................................95
**SURA YA NNE:JINSI WAANDISHI WA DIWANI YA *TUNU YA USHAIRI* WANAVYOTOFAUTIANA ....................................................................................96**
4.0 Utangulizi....................................................................................................................96
4.1 Ukosefu wa Ajira ........................................................................................................96
4.2 Utumizi wa Madawa ya Kulevya na Ulevi ..................................................................99
4.3 Magonjwa ....................................................................................................................101
4.4 Umaskini ......................................................................................................................103
4.5 Utamaduni....................................................................................................................105
4.6 Hitimisho......................................................................................................................107
**SURA YA TANO:HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..........................................108**
5.0 Utangulizi....................................................................................................................108
5.1.0 Hitimisho..................................................................................................................108
5.1.1 Madhumuni ya Utafiti..............................................................................................109
5.1.2 Matokeo kuhusu Nadharia Tete ...............................................................................109
5.2 Mapendekezo ..............................................................................................................110
**MAREJELEO ...........................................................................................................111**

## KIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **K.H.J** | Kama hapo Juu |
| **N.K** | Na kadhalika |
| **UK.** | Ukurasa |
| **K.L.B** | Kenya Literature Bureau |

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Utafiti huu unahusu uchanganuzi linganishi wa waandishi wanne katika diwani ya *Tunu ya ushairi*, ili kuchunguza kufanana na kutofautiana kwao katika kuzungumzia maswala ya vijana katika jamii. Uchunguzi huu umejifunga katika kuchunguza jinsi waandishi hawa wanavyoshughulikia maswala ya vijana katika diwani ya *Tunu ya ushairi*. Katika utafiti huu tumezingatia kijana kama binadamu wa kiume au kike aliye kati ya umri wa miaka 15 na 35 kulingana na Katiba ya Kenya (2010).

Kipindi hiki cha maisha hudhihirika kuwa cha mpito, ambapo kijana anabadilika kutoka maisha ya utoto hadi utu uzima. Data ya kufafanua uamuzi huu imetolewa katika sehemu inayoifasili dhana ya vijana. Nchini Kenya, kuna kauli kwamba, '*vijana ni viongozi wa kesho;* hii ni kauli ambayo hutolewa mara kwa mara na viongozi katika majukwaa mbalimbali ya siasa ili kuwapa vijana motisha.Utafiti huu unadhamiria kuonyesha jinsi waandishi wote wanne wa diwani hii ya *Tunu ya ushairi* wameshughulikia maswala ya vijana katika jamii.

Tunatumia Nadharia ya Uhalisia katika utafiti wetu, hii ni kwa sababu nadharia ya uhalisia hujikita katika ukweli wa hali halisi ya maisha katika jamii mahsusi na mashairi hushughulikia maswala mazito na muhimu yanayomhusu binadamu katika jamii.

Kulingana na Kimani na Chimerah (1999), ushairi ni sanaa ya lugha inayoeleza jambo au wazo kwa njia ya mkato, na kwa namna inayoteka hisia za msomaji au msikilizaji. Maneno katika shairi huteuliwa kimaksudi (ili yalete taswira maalumu akilini mwa

msomaji au msikilisaji). Maneno hayo pia hupangwa ili yatoe mdundo fulani shairi linapoimbwa, linaposemwa, au linaposomwa. Waandishi hawa wanaendelea kusema kwamba, ushairi hulenga moyo wa binadamu kwa sababu hueleza jambo na kutuingiza katika hisia fulani. Ushairi unaweza kumfanya mtu ahisi uchungu au furaha, hasira au ridhaa; waweza kumburudisha mtu hadi moyo wake utulie ama kumhamasisha mtu achukue hatua fulani ya kubadilisha hali, kama yafanyavyo mashairi mengi ya ukombozi. Upekee wa ushairi hutokana na jinsi ambavyo lugha inatumika ili kudhihirisha upekee wa umbo na nafasi katika muktadha wa sajili na arudhi za kishairi.

Licha ya upekee wa umbo na mtindo katika matumizi ya lugha, ushairi huzingatia maudhui na mazingira ya kijamii kama ilivyo tanzu zingine za fasihi. Ushairi wa Kiswahili ni wa aina mbili: mashairi ya jadi au mapokeo ambayo yanatungwa kwa kuzingatia arudhi au kaida za utunzi kama vina, mizani, idadi maalum ya mishororo katika ubeti, vipande n.k. Pili, kuna mashairi huru ambayo yanakiuka kaida hizo na badala yake kutegemea mbinu nyingine za kishairi kama uruwazaji wa kimuundo kuuwasilisha ujumbe wake.

Hivyo basi, watunzi wana uhuru wa kutunga aina za ushairi waupendao almuradi wafikishe ujumbe kwa hadhira. Hii ndio sababu tukaamua kuchagua diwani hii ya *Tunu ya ushairi* ambayo imechapishwa (mwaka wa 2013) na mashairi mengi yaliyotungwa pale ni mashairi huru.

Diwani hii ina mashairi yenye kushughulikia masuala mapana katika maisha ya mwanadamu. Kuna mashairi kuhusu mazingira, unafiki, ufisadi, ubinafsi, mapenzi, ndoa, utaifa, msako wa nafsi, ulemavu, mauti, falsafa kuhusu maisha, nasaha na kadhalika. Mashairi haya yanatujia kwa sauti tofauti tofauti; zipo sauti za kubeza na kukebehi, sauti za huzuni na masikitiko, sauti za  unyonge na majonzi, sauti za kukemea na kukashifu, sauti za kuonya na kunasihi, na sauti za furaha na vicheko. Kwa jumla ni sauti za maisha. Diwani ya *Tunu ya ushairi* ni ya kisasa na ina mkusanyiko wa mashairi mia moja na ishirini na tatu na mashairi hayo yameandikwa na waandishi wanne tofauti. Hawa ni pamoja na:-

*(i)* *Amiri A.S. Andanenga* ambaye ni mshairi mkongwe wa ushairi wa Kiswahili.

(ii) *Mwalaa M. Nyanje* ni mtunzi anayeinukia. Mbali na utunzi wa mashairi, Mwalaa ni mtunzi wa kamusi.

(iii) *Joseph Kiponda* ni mwanafunzi wa shahada ya Uzamili katika Kiswahili Chuo Kikuu cha Pwani ambaye utunzi wake unaonyesha kuwa ni mwandishi aliyekomaa.

(iv) *Dkt. Timothy M. Arege* ni mhadhiri mkuu wa fasihi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Arege ni mtunzi wa tamthilia, hadithi fupi na mashairi. Pia ni mwandishi wa vitabu vya kiada na ziada kwa ajili ya shule za upili.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Nchini Kenya vijana wanawakilisha asilimia 75% ya wananchi wa Kenya. Jambo la kusikitisha ni kwamba vijana hao wanakumbwa na changamoto chungu nzima ambazo chanzo chake kinafaa kichunguzwe.Wao ndio msingi na tegemeo la taifa husika. Kwa

hivyo basi tatizo la utafiti wetu ni kuchunguza na kubainisha aina za changamoto pamoja na wajibu na maswala yote yanayowakumba vijana kama yanavyoangaziwa na waandishi mbalimbali katika *Tunu ya ushairi.* Mbali na utambuzi huo wa changamoto hizo utafiti huu vilevile umelenga kutathmini msingi wa maswala hayo.Tumebainisha kinachochangia maswala haya. Utafiti wenyewe umeangazia maswala yanayowakumba vijana kwa jumla, wawe wa jinsia ya kike au kiume na vilevile yanavyojitokeza katika diwani ya *Tunu ya ushairi.* Aidha, utafiti huu umelinganisha na kulinganua jinsi waandishi mbalimbali katika *Tunu ya Ushairi* wanavyoshughulikia maswala ya vijana kwa jumla.

Tofauti na utafiti huu, kuna tafiti nyingine zilizoshughulikia maswala ya vijana katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi, kwa mfano riwaya za Kezilahabi *Rosa Mistika na Kichwa maji,* tamthilia za Kithaka wa Mberia *Kifo Kisimani* na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* na hadithifupi kama vile *Namchukia Babangu* na *Achekaye Mwisho* za Iribemwangi katika *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine.* Utafiti huu umejikita katika ushairi wa Kiswahili na diwani iliyotumika ni *Tunu ya ushairi*. Katika kufanya hivi, utafiti huu umeongozwa na *Nadharia ya Uhalisia* ambayo inasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu kama yanavyoonekana hasa na mtu wa kawaida.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Lengo letu la kimsingi ni kuchunguza jinsi ambavyo watunzi tofauti tofauti katika diwani ya *Tunu ya ushairi* wanavyoshughulikia swala la vijana kwa jumla. Katika kufanya haya

basi tunalenga kutathmini namna waandishi hawa wanavyofanana na kutofautiana. Malengo ya utafiti wetu hasa ni:-

**i)** Kuchunguza maswala ya vijana yanayoshughulikiwa na waandishi wanne tofauti katika diwani ya *Tunu ya ushairi*.

**ii)** Kutathmini mwelekeo sawa wa waandishi katika diwani ya *Tunu ya ushairi* kuhusu vijana.

**iii)** Kuchunguza jinsi waandishi hawa wanne wa mashairi katika diwani ya *Tunu ya ushairi* wanavyotofautiana katika kushughulikia maswala ya vijana.

## 1.3 Nadharia Tete

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

*a)* Vijana katika jamii tofauti tofauti huwa na changamoto zinazofanana.

*b)* Waandishi wote katika diwani ya *Tunu ya ushairi* wana mwelekeo sawa kuhusu vijana.

*c)* Waandishi hawa katika diwani ya *Tunu ya ushairi* wanatofautiana, kuhusu ambavyo wanashughulikia maswala ya vijana.

## 1.4 Sababu za kuchagua Mada Hii

Tumechagua mada hii kwa sababu kadha. Kwanza, kulingana na ufahamu wetu ni machache yameshughulikiwa kuhusu dhana ya vijana na maswala yanayowahusu katika utanzu wa ushairi. Watafiti wengi wameshughulikia swala hili katika tanzu zingine kama vile riwaya za Kezilahabi *Rosa Mistika* na *Kichwa maji*, tamthilia za Kithaka wa Mberia, *Kifo Kisimani* na *Maua Kwenye Jua la asubuhi* na hadithi fupi kama vile *Namchukia*

*Babangu* na *Achekaye Mwisho* za Iribemwangi katika *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine.* Lakini kulingana na uelewa wetu ni mashairi machache tu yameshughulikia suala la vijana katika ushairi wa Kiswahili. Pili mada hii inahusiana na kundi muhimu sana katika jamii ambalo ni vijana. Umuhimu huu unatokana na sababu kwamba, vijana wanawakilisha asilimia kubwa sana ya idadi ya watu wote nchini Kenya. Kulingana na Becker (2011), asilimia sabini na tano inawakilisha vijana chini ya umri wa miaka thelathini, na wenye umri wa kati ya 15 hadi 24 wanawakilisha asilimia ishirini na mbili. Mbali na idadi yao kubwa, wanawakilisha uhai wa taifa; tuna maana kwamba vijana wanategemewa sana katika jamii kwa kiasi kikubwa. Nchi ambayo haina kitengo cha vijana bila shaka haina matumaini kabisa.Haya yanatokana na ukweli kwamba vijana ndio viongozi wa kesho na vile vile msingi wa kizazi cha sasa katika taifa. Nchi yoyote ambayo haina vijana haina matumaini yoyote ya kukiendeleza kizazi chake. Kwa hivyo kitengo cha vijana ni lazima kishughulikiwe ipasavyo.

Sababu nyingine iliyotufanya kuichagua mada hii ni kwamba inahusiana na kutokuwepo kwa maadili miongoni mwa wanajamii na haswa kwa upande wa vijana. Kuna mambo mengi yanayoshuhudiwa miongoni mwa vijana katika jamii ambayo yanakiuka maadili ya kijamii. Mambo yenyewe ni anuwai kama vile ulevi, matumizi ya mihadarati, ukosefu wa elimu, umaskini, ndoa za mapema, mapenzi yasiyo halali, ukosefu wa malezi mema, magonjwa, ukosefu wa ajira, ukosefu wa maadili, vijana kutumiwa na wanasiasa na mengine mengi. Kwa hivyo ni jukumu la kila mwananchi kuona kwamba vijana wamebadilisha mienendo yao na kuwa watu wa kutegemewa katika jamii.

Utafiti huu pia unachangia katika kukuza na kuiendeleza fasihi andishi ya Kiswahili. Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kuwa diwani hii ya *Tunu ya ushairi* imeandikwa na waandishi wanne tofauti na ina mashairi ambayo yanashughulikia masuala mapana katika maisha ya mwanadamu akiwemo kijana. Diwani hii pia ni kati ya diwani ambazo zimechapishwa hivi majuzi mwaka wa 2013 kwa hivyo maswala mengi yanayoshughulikiwa hapa ni maswala ibuka.

**1.5 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu umehusu uchanganuzi linganishi wa jinsi waandishi katika diwani ya *Tunu ya ushairi* wanavyoshughulikia maswala ya vijana. Utafiti wenyewe unatilia maanani matatizo yanayowakumba vijana kwa jumla pamoja na yale yanayoibuka katika ushairi.Utafiti huu umejikita tu katika kulinganisha na kutofautisha waandishi katika diwani ya *Tunu ya ushairi* kuhusu maswala ya vijana ili kubainisha wanavyofanana na kutofautiana.Tumeongozwa na nadharia ya uhalisia ambayo inasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu kama yanavyoonekana hasa na mtu wa kawaida.Tumechagua nadharia hii ya uhalisia kwa sababu wahusika hapa ni vijana na jamii inawategemea, na diwani hii ya *Tunu ya ushairi* bila shaka inaoana na nadharia hii kwa sababu changamoto zile zinazowakumba vijana ni kiwakilishi kamili cha hali halisi ya jamii tunamoishi.

Kutokana na maelezo haya, tunaona kuwa nadharia ya uhalisia hujikita katika ukweli wa hali halisi ya maisha katika jamii mahsusi. Mtafiti anayejikita katika nadharia hii ya Uhalisia, hutafiti jinsi mwandishi alivyofanikiwa kudhihirisha ukweli wa mambo kupitia maswala yaliyopewa kipao mbele. Kwa sababu hii basi, mtafiti huangalia jinsi ukweli

ulivyobainishwa katika lengo la mwandishi ili kufanikisha mawasiliano katika mazingira fulani mahsusi. Nadharia hii itakuwa mhimili muhimu katika utafiti wetu kwa sababu itatupa taswira halisi ya vijana na maswala ambayo wanakumbana nayo.

Tumeshughulikia dhana hii ya kijana katika mashairi kumi na saba yaliyoteuliwa kati ya mashairi mia moja ishirini na tatu yaliyoko kwenye diwani hii ya *Tunu ya ushairi* ambayo yanadhihirisha maswala ya vijana katika jamii. Hata hivyo mwandishi mmoja ambaye ni Nyanje amezungumzia kwa ziada maswala ya vijana ndio maana tumeongeza shairi lake moja zaidi ya yale manne tuliyoyateua. Tumeyateua mashairi hayo baada ya kuyahakiki mashairi yote kwenye diwani hiyo na kupata kuwa hayo tu ndiyo yameshughulikia maswala ya vijana kwa jumla na tumeteua mashairi manne tofauti ya kila mwandishi. Mashairi haya ni pamoja na *Fanya ulizio,Kidau,Hili na lile,Pendo la pesa* mashairi ya Amiri A.S.Andanenga.Mashairi mengine ni ya Arege Timothy haya ni pamoja na*Maisha, Kizazi,Vidato vya maisha na Ule Mwamba Mkubwa. Mwanangu sikubali, Jana si leo, Dagaa na Maisha vidato* mashairi ya Joseph Kiponda. Mashairi ya Mwalaa Mranga Nyanje ni *Wasia, Wanaume ni wanyama, Malezi mema, Lauzi mwanangu, na Wanangu Nawasia*.

**1.6 Yalioandikwa kuhusu Mada ya Utafiti**

Uchunguzi wetu kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada hii umejikita katika ushairi wa Kiswahili. Mashairi hushughulikia masuala mazito na muhimu yanayomhusu binadamu katika jamii.Ingawa hatukuweza kuona kazi ambayo hususan inashughulikia diwani ya *Tunu ya Ushairi* moja kwa moja, tumepitia kazi kadhaa ambazo zinashughulikia maswala

ya vijana na ambazo zimetufaidi sana. Aidha, yaliyoandikwa katika nyanja zingine yametufaidi mno kwa sababu yametupa mwongozo unaofaa.

### 1.6.1 Maswala ya Vijana katika Ushairi wa Kiswahili

Wataalamu mbalimbali wameshugulikia mambo muhimu kuhusu somo hili. Hii ni pamoja na *utenzi wa Mwanakupona*, *utenzi wa Hati na Adili* na *utenzi wa Siraji*.

*Utenzi wa Mwanakupona* ulitungwa na Mwana Kupona Binti Msham, akimuusia mwanawe na kuhofu kuwa angeaga dunia kabla ya kutimiza dhima yake ya mama kama mlezi. Mama anachukua jukumu la kumpa wasia binti yake ambaye ni mchanga kiumri ili awe na uhusiano mwema na mwenyezi Mungu pamoja na mumewe. Anampa wasia kuhusu dini na hili ndilo jambo la kwanza na muhimu analomwambia. Anamwambia binti yake kwamba ashike waadhi na dini kabisa kwa sababu Mungu atamhifadhi na kumuepusha kutokana na maovu, awe na adabu aseme mambo ya kweli na ajihusishe na watu wazungumzao ukweli.

Jambo lingine ni kwamba ni bora kabisa aepukane na watu wanaozungumza mambo machafu na wajinga wasojua kujichunga. Badala yake awe marafiki na waumini na asiwapende tu wenye jamali na mali na pia asiwadharau maskini bali awasaidie. Jambo la pili ni kuhusu mumewe. Mwanakupona anamwambia binti yake amsifu mumewe siku zote watakazoishi pamoja, anaendelea kumwambia kwamba ampende mumewe kwa dhati na akitoka kwenda safari aagane naye vizuri, wakati wa kurudi amkaribishe na amtengenezee mahali pazuri pa kulala. Anaendelea kumwambia kwamba ni jukumu lake kumpikia mumewe, asimkasirikie bila sababu na kumwambia mambo mabaya. Jambo

lingine analomwambia binti yake ni kuhusu usafi. Anamwambia kwamba ni jukumu lake kufanya usafi wa kila aina kule nyumbani. Mbali na usafi wa jumla, ni vyema pia naye aoge na kuchana nywele zake vizuri kila wakati. Utenzi huu ni muhimu sana kwa sababu unashughulikia vijana ambao ni wahusika wakuu katika utafiti wetu hata kama umejikita katika maswala ya mhusika wa kike peke yake. Kazi hii imetufaidi katika utafiti wetu maana inahusu vijana lakini ni tofauti na yetu maana yetu inawahusu vijana wote na hii inahusu vijana wa kike tu.

*Siraji ni utenzi* ulioandikwa na baba kumpa wasia mwanawe. Kulingana na mtunzi wa utenzi huu wa *Siraji*, Siraji ni taa inayomulika na taa hiyo ndiyo itakayomwongoza kijana mhusika maishani mwake. Baba anamweleza mwanawe kwamba jambo la muhimu na la kwanza kabisa ni kumcha Mungu wakati wote. Anamwonya dhidi ya kuiba wala kugusa kitu chochote kisichokuwa chake bila idhini ya mwenyewe. Anamsihi asidanganye wala kuchochea vita kati ya marafiki na awe na marafiki wazuri. Alimwonya pia dhidi ya ufisadi na watu wenye fitina na asaidie wale ambao wanahitaji usaidizi kutoka kwake wala asiwe mvivu kamwe. Anazungumzia swala la mapenzi na ndoa bila kusahau kumwonya dhidi ya kuchelewa kufika nyumbani kama mzee wa boma hilo. Baba mzazi anaendelea kumwambia kwamba ni jukumu lake kufurahisha mke wake siku zote na kwamba ni vyema apate mke wa ukoo wao na ambaye yuko katika daraja lake. Kuhusu mapenzi anasema kwamba hili ni jambo la kweli na kuna kupanda na kushuka katika suala hilo kwa hivyo itakuwa bora wavumiliane na kuelewana.

*Utenzi wa hati* ni utenzi ulioandikwa na Shabaan Robert (1952). Ushairi wenyewe unahusu wasia wa baba kwa binti yake. Baba anamwambia binti yake kwamba dunia ni mvurugo tena ni ngumu sana kwa hivyo anamwandikia hati hiyo na kumwambia jinsi ambavyo ataiweka na kuitunza vyema. Anaendelea kumwambia kwamba atunze hati hiyo maana ni nuru kwa maisha yake yote kwa hivyo aiweke kama herini masikioni na moyoni siku zote. Anazungumzia pia kuhusu ibada, anamwambia kwamba ibada ni muhimu kwa maisha yake aishike na kuifuata kabisa. Anaendelea kumwambia kwamba ni bora apate elimu kwa sababu elimu ni kitu kizuri na muhimu kwa binadamu yeyote yule hasa kijana. Pia utenzi wa hati, una mafunzo kuhusu ndoa. Baba anamwambia binti yake kwamba ni jukumu lake kumpikia mumewe chakula kizuri ili asilalamike, asishindane naye kwa njia yoyote ile kwa sababu mume ndiye kichwa cha nyumba yoyote ile. Anazungumzia usafi pia kwa kusema kuwa, yeye kama binti yake awe mstari wa mbele katika kudhihirisha usafi huo katika sehemu zote kwa jumla. Wala asitie doa katika maisha yake na asishiriki katika uongo na watu waongo. La mwisho ni kwamba awaheshimu watu wote wazima na awe na adabu.

*Utenzi wa Adili* ni utenzi uliotungwa na Shabaan Robert kwa minajili ya baba mzazi kutoa wasia kwa kijana wake Adili. Utenzi huu umefanyiwa utafiti na Watuha A.L (2011) ambaye ameshughulikia maudhui ya waadhi. Anasema kwamba ulimwengu wa leo unatoa peupe wasia mwafaka kwa vijana.Mwandishi anamwambia Adili kwamba ni vizuri na muhimu sana kuishi maisha ya kumcha Mungu mtengeza ulimwengu na mjua kila kitu bila kusoma kitabu chochote kinyume na watu wote tujuao. Pia, elimu ni bora kwa kila kijana kwa hivyo Adili anaambiwa apate elimu maana elimu ni ufunguo wa

maisha. Jambo lingine muhimu ni bora ampende bibi na watoto wake pamoja na watu wote kwa jumla. Utenzi huu utatufaidi sana katika kuangazia maswala ambayo yanahusu vijana hasa kuwapa mwelekeo mzuri kwa kuwapa wasia unaowafaidi. Ni tofauti na kazi yetu ya utafiti kwa sababu inaangazia tu wasia kwa vijana ilhali sisi tunaangazia maswali yote yanayowahusu vijana.

### 1.6.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Maswala ya Vijana Katika Kazi Zingine

Katika makala ya Chacha Nyaigoti Chacha, (1986) mwandishi anamlenga Rosa katika *Rosa Mistika* (1971) kwa kusema kuwa, mhusika Rosa hafai kuhukumiwa ila kuhurumiwa kwa sababu ni mdhulumiwa wa jamii kongwe isiyoelewa mfumo wa maisha ya kisasa. Riwaya hii ni riwaya ambayo kimsingi inaangazia athari za malezi mabaya ya kifamilia katika maisha ya baadaye ya Rosa. Anasema kwamba kuwaelimisha watoto ni haki yao ambayo hawafai kunyimwa na ni jukumu la mzazi kufanya hivyo katika malezi kwa jumla. Kazi hii ni muhimu sana katika utafiti wetu ingawa imezingatia tu kijana wa kike, imetupa mwelekeo mzuri wa jinsi ambavyo vijana wa kike wanavyodhulumiwa lakini sisi tunajikita kwenye mashairi.

Lugano R.(1989) amechunguza namna kezilahabi amewachora wahusika wake na amegundua kwamba Kezilahabi ameangazia zaidi wahusika vijana kama vile Kazimoto katika *Kichwa maji* (1974) na Rosa katika *Rosa Mistika* (1971). Lugano ameonyesha mitazamo ya vijana katika kujikomboa wao wenyewe. Uhakiki huu wa Lugano ni muhimu katika utafiti wetu kwani umetusaidia kuona jinsi ambavyo wahusika vijana wamechorwa katika jamii tofauti tofauti. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu

Lugano ameshughulikia riwaya mbili tofauti za Kezilahabi nasi tunajikita kwenye diwani ya waandishi wanne tofauti.

Obore E.M. (2012), alitafiti kuhusu dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) na *Tumaini* ya (2006). Alisema kwamba swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike linabainika wazi katika riwaya hizo na swala hilo limejitokeza kwa hali mbalimbali na kudhihirisha kuwa kijana wa kike wamekandamizwa na kunyimwa haki. Hali hii imebainika kutokana na sababu ya kuonekana kwa kijana wa kike kama kiumbe duni na jinsia ya kiume yenye misingi na kaida zenye mashiko katika mila na tamaduni zinazompendelea kijana wa kiume. Kazi hii ya Obore imetufaidi mno katika utafiti wetu kwa sababu imeshughulikia maswala ya vijana wa kike hasa jinsi kijana huyu wa kike amedhulumiwa na kukandamizwa bila kupewa haki anayostahili kama mtoto wa kike. Tofauti na kazi yetu ni kwamba yeye amejihusisha na riwaya lakini sisi tunatumia diwani ya *Tunu ya ushairi*. Pili, ameangazia dhuluma dhidi ya vijana wa kike tu nasi tunaangalia maswala yote yanayowakumba vijana wote kwa jumla yaani wa kike na wa kiume.

Nkonge (2006) amechambua riwaya mbili za waandishi tofauti hii ni pamoja na *Nguvu ya Sala* na Kichwa Maji kwa kuyamulika maswala mbalimbali kuhusu vijana. Haya ni pamoja na mapenzi na ndoa, maisha na kifo, malezi, uozo wa jamii na dini. Uchambuzi huu ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu baadhi ya maswala ambayo Nkonge amechunguza yanaoana na yale ambayo tumeyashughulikia katika utafiti wetu. Tofauti iliyopo kati ya kazi hii na yetu ni kwamba Nkonge amechambua riwaya mbili tofauti nasi tunachambua diwani moja ya waandishi tofauti.

Naliaka, R. (2012) amechunguza hali ya vijana katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara*. Uchambuzi wenyewe unatilia maanani matatizo yanayowakumba vijana kwa jumla.Naliaka anagundua kwamba vijana wana malezi duni na wameshindwa kukabili matatizo yanayowakumba katika jamii.Ilibainika kwamba matatizo ya kiuchumi yanachangia pakubwa jambo hili. Wazazi  wengi hukosa nafasi ya kukaa na wana wao na kuwaelekeza kwa sababu muda wao mwingi hutumiwa kwa mambo mengine. Utafiti huu wa Naliaka ni muhimu sana kwa kazi yetu kwa sababu umeangazia matatizo yanayowakumba vijana kwa jumla. Tofauti na kazi yetu ni kwamba ametumia riwaya katika kazi yake kinyume na sisi tunaotumia diwani ya *Tunu ya Ushairi*.

Wafula, R. (1999), anazihakiki tamthilia tatu zenye wahusika ambao ni vijana. Tamthilia hizo ni pamoja; *Wakati Ukuta* (1972), *Hatia* (1972) na *Uasi* (1980). Tamthilia mbili kati yazo *Wakati Ukuta* na *Hatia* ni za Tanzania na *Uasi* (1980) ni ya Kenya. Kauli yake jumuishi kuhusu vijana ni muhimu sana. Anasema kuwa vijana huweza kubadilika kwa urahisi kwa vile imani zao za kimsingi zinaendelea kujengeka. Hata hivyo, uhakiki huo haukubaini kiwango cha mabadiliko au ufaulu wa vijana katika kuinasua jamii kutokana na matatizo yenyewe. Kazi hii ya Wafula ni muhimu sana katika utafiti wetu maana inashughulikia wahusika vijana ambao pia sisi tunashughulikia. Hata hivyo hii kazi ni tofauti ya yetu kwa sababu imejikita kwenye tamthilia na sisi tumejikita kwenye diwani ya *Tunu ya Ushairi*.

Mutua (2007) ameangazia mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili. Kwenye utafiti wake anabainisha kuwa

vijana na wazee kwa jumla wanaunga mkono na vilevile kupinga ukombozi wa wanawake. Tamthilia hizo ni Kitumbua Kimeingia Mchanga (2000), Migogoro (2006) na Natala (1997). Mutua amefaulu kuonyesha mitazamo ya vijana kuhusu uhuru wa mwanamke, ambao ni mchango muhimu sana kuhusiana na ukombozi. Utafiti huu umetupa mwongozo mzuri katika kazi yetu kwa sababu Mutua ameonyesha jinsi ambavyo vijana wamehusika katika ukombozi wa mwanamke kwa hivyo vijana wamewajibika. Ni tofauti na kazi yetu maana tunaangazia maswala ya vijana yanavyowasilishwa na waandishi katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*.

Kiongera (2010) ameshughulikia mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya katika tamthilia nne za Kiswahili ambazo zimeandikwa na waandishi wawili tofauti, nazo ni: *Maua Kwenye Jua la asubuhi* (2006) na *Kifo kisimani* (2001), vitabu vya Kithaka wa Mberia pamoja na Pango (2003)na Seserumbe (2009), vitabu vya Wamitila. Utafiti wake unahusu jinsi vijana wanavyochangia mabadiliko katika tamthilia hizi nne za Kiswahili. Amethibitisha kwamba vijana wanayatambua maovu ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na wanakabiliana nayo. Vijana hao wamefanikiwa kuwaondoa viongozi waovu kutoka madarakani ingawaje wanakabiliwa na changamoto katika harakati za kuleta mabadiliko hayo. Utafiti huu wa Kiongera umetupa mwongozo unaofaa kuelewa baadhi ya changamoto vijana hukumbana nazo katika jamii. Tofauti na kazi yetu ni kwamba ameangazia mabadiliko ambayo vijana wameleta katika jamii nasi tunashughulika na maswala yanayowakumba vijana. Pili yeye ameangalia tamthilia nne za waandishi wawili tofauti ilhali sisi tumejikita kwenye utanzu wa ushairi.

## 1.7 Msingi wa Nadharia

### 1.7.1 Nadharia ya Uhalisia

Utafiti huu umeongozwa na misingi ya Nadharia ya Uhalisia. Uhalisia ni nadharia ambayo inapendekeza kazi ya fasihi iwasilishe maisha ya jamii kwa njia ya kweli na katika mazingira ya kawaida.Katika nadharia hii, mhalisia hujikita katika masuala yanayoonyesha ukweli wa mambo katika jamii. Ukweli huu ni ule ambao unaweza kuonekana na kuthibitishwa pasi na tashwishi yoyote ile.

Kimsingi uhalisia uliwekewa msingi na mwanafalsafa anayejulikana kama Hegel katika kitabu chake kinachojulikana kama *Aesthetik* (ujumi) mwaka wa 1835. Mtaalamu huyu alipendekeza ulimwengu wa maisha ya jamii Wamitila (2002).Wamitila anaendelea kusema kwamba Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa.Baadhi ya kauli za kimsingi na ambazo ni muhimu kuhusu nadharia ya uh7lisia ni kwamba inajikita katika ushabihi kweli. Maana yake ni kwamba kazi yoyote inayoandikwa katika msingi huu ni sharti ikaribiane na kuelezea ukweli katika jamii husika, kwa hivyo maandishi yoyote yanayoegemea katika uhalisia huchukuliwa kwamba yote yaliyomo yanazama na kuwiana na ukweli katika jamii wanayoiangazia.

Wamitila (2003) anasema kwamba dhana ya uhalisia ilizuka kama vuguvugu la kupinga mtazamo wa ulimbwende. Anakubaliana naye Mbatiah (2001) kwamba uhalisia, kama mkondo wa uandishi, unasisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi, kama yalivyo kila siku. Anadai kwamba George Lukacs, mfuasi wa Karl Marx kutoka Hungary ni mmoja wa wataalamu wanaohusishwa na nadharia hii na ambao mchango wao umekuwa na athari kubwa sana katika tapo hili. Lukacs aliamini kwamba uhalisia ulifaa

kusawiriwa katika ukamilifu wake na vilevile picha ya uhalisia inayoshughulikiwa ni lazima ichunguzwe kwa undani ili kuzielewa sheria za mabadiliko ambazo husababisha hali ya uhalisia wakati fulani. Kwa msingi huu, Lukacs aliamini kwamba mwanasanaa au mwandishi ni lazima aelewe kwamba ulimwengu huu anamoishi ni changamano na hubadilikabadilika. Kwa hivyo, mwandishi au mwanasanaa huyo hana budi vilevile kuvielewa vipengele vya kijamii ambavyo vinasababisha mabadiliko kama hayo na kuathiri hali ya uhalisia kila wakati.Wanoegemea katika tapo hili wanaamini kwamba yale yanayoshughulikiwa katika maandishi fulani ni lazima yaweze kuthibitika katika ulimwengu halisi.

Nao Wafula na Njogu (2007) wanasema,dhana hii ya uhalisia ilianza kujitokeza zamani sana katika kipindi  cha enzi ya kati ya mwaka wa 1100-1500 Baada ya Kristo katika karne ya kumi na tisa, kwa azma ya kupinga mkondo wa ulimbwende.Uhalisia kama tapo la kuwaelekeza watunzi ulianza kudhihirika kuanzia mwaka wa 1800 nyakati za mwandishi wa kifaransa Gustav Flaubert ambaye ni mmoja wa waanzilishi wa uhalisia.Baadhi ya waandishi wa awali wa kipindi hiki ambao maandishi yao yalisisitiza hali ya ukweli walitoka nchini Ufaransa wakiwemo Balzec, Stendhal na Gustav Flaubert. Waandishi hawa wa Kifaransa walichangia sana katika kuyawekea msingi maandishi yenye mwegemeo wa kihalisia.Uhalisia ulipitia mabadiliko mengi ya kimatumizi na msingi mkuu wa mawazo haya umetokana na mawazo ya wanafalsafa  kama vile Emmanuel Kant (1790) na hata Schiller (1798) ambao wanachukulia kuwako kwa mfanano kati ya jinsi mtu anavyoweza kuyakabili na kuyang'amua mambo, yaani urazini au ung'amuzi wa kibinafsi.

Waandishi na wahakiki wengi waliotumia nadharia ya uhalisia waliamini ya kwamba dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo. Mhakiki naye alimtathmini kwa namna ambavyo huyo mwandishi alijibidiisha kuonyesha ukweli. Haja kubwa ya kuigiza ilikuwa kuonyesha picha ya mazingira ambamo jamii inapatikana; mathalan, kioo kinavyotumika kutoa picha za mwanadamu. Kulingana na wataalamu hao, mwandishi anapaswa kuitoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku. Dhana ya fasihi kuwa "ni kioo cha jamii" ilitokana na uhalisia. Ukweli ni kwamba ijapokuwa fasihi huzungumzia ukweli, mwandishi huchagua mambo anayotaka kuzungumzia. Mwandishi huchagua, akachanganua na kutenganisha anayozungumzia. Mwandishi wa kihalisia pia huweza kusuta maovu ya kijamii kulingana na Wafula na Njogu (2007).

Msokile (1993) analieleza tapo la uhalisia kama mtindo wa sanaa wa kuonyesha maisha kama yalivyo na kwamba mambo yaliyotokea katika ulimbwende ndiyo yaliyosababisha kuzuka kwa uhalisia.

Mbatiah (2001) anafafanua uhalisia kama istilahi inayorejelea kimsingi mtindo wa uandishi unaojishughulisha na utoaji wa taswira halisi ya maisha ya kawaida katika jamii mahususi. Wasanii walioshughulikia tapo hili waliamini kwamba ukweli uliweza kupatikana katika maisha pamoja na shughuli za kawaida za kila siku za binadamu akiwa katika mazingira yake halisi ya kijamii. Mazingira kama hayo ni lazima yasawiriwe jinsi yalivyo na bila kutiliwa chumvi.

Kutokana na maelezo haya, tunaona kuwa nadharia ya uhalisia hujikita katika ukweli wa hali halisi ya maisha katika jamii mahsusi. Mtafiti anayejikita katika nadharia hii ya uhalisia, hutafiti jinsi mwandishi alivyofanikiwa kudhihirisha ukweli wa mambo kupitia

maswala yaliyopewa kipaumbele. Kwa sababu hii basi, mtafiti huangalia jinsi ukweli ulivyobainishwa katika lengo la mwandishi ili kufanikisha mawasiliano katika mazingira fulani mahsusi. Nadharia hii imekuwa mhimili muhimu katika utafiti wetu kwa sababu imetupa taswira halisi ya vijana na maswala ambayo wanakumbana nayo.

Kwa hivyo tumeichukua nadharia hii ya uhalisia kama msingi wa uhakiki wetu kwa sababu ya maswala ambayo yanaangaziwa katika diwani ya *Tunu ya ushairi*. Diwani hii ya *Tunu ya ushairi* bila shaka inaoana na nadharia hii kwa sababu shida zile zinazowakumba vijana na maswala yote ni kiwakilishi kamili cha hali halisi ya jamii tunamoishi. Baadhi ya maswala yanayozungumziwa katika diwani hii ni kama vile mapenzi, ukosefu wa ajira, madawa ya kulevya, magonjwa, malezi mabaya, utamaduni, elimu, wasia, uhalifu na kadhalika.Maswala haya si ya kidhahania bali yanaonyesha hali halisi na ukweli wa maswala yanayowakumba vijana katika jamii. Huu ndio uhalisia ambao tunachukua kama msingi wa kinadharia wa kazi yetu.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Kulingana na Mugenda O. na Mugenda G. (1999), mbinu za utafiti huhusisha njia zote zinazotumiwa kufanikisha utafiti. Hii inahusisha njia zote zinazotumikakutambulisha data pamoja na njia zozote zile zinazotumika kutathimini matokeo ya utafiti. Sehemu hii tutaigawa katika vijisehemu vitatu kama ifuatavyo:

### 1.8.1 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Tumeteua sampuli lengwa katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu sampuli lengwa kulingana na Mugenda O. na Mugenda G. (1999), ni sampuli ambayo humwezesha mtafiti kutumia kadhia ambazo zina ujumbe kulingana na madhumuni ya utafiti. Sampuli lengwa ni sampuli ambayo huchaguliwa kwa sababu fulani maalum.Tumeteua diwani hii ya *Tunu ya ushairi* katika utafiti wetu kwa sababu: kwanza, mashairi yaliyoko kwenye diwani hii yameandikwa na waandishi wanne tofauti.Waandishi hawa wanne wana mawazo na maoni tofauti tofauti kuhusu maswala ya vijana hata ingawa mawazo mengine yanawiana na hili linatusaidia katika utafiti wetu wa kulinganisha na kulinganua waliyoyaandika; na inatufaa sana katika utafiti wetu. Pili, diwani hii ina mashairi ambayo yanashughulikia maswala mapana ya jamii kuhusu maisha ya mwanadamu hasa vijana.Tumehakiki mashairi yote katika diwani hii ya *Tunu ya ushairi* kwa kuyasoma na kuteua yale yanayoshughulikia maswala ya vijana.

### 1.8.2 Ukusanyaji wa Data na mbinu za Ukusanyaji Data

Utafiti huu umelenga kukusanya data kutoka mashairi ambayo tumeteua kwenye diwani ya *Tunu ya ushairi*. Mashairi ambayo tumeteua ni yale tu yanayomlenga kijana kwa jumla.

Pia tumedurusu matini kadha zenye manufaa kwa utafiti wetu. Azimio hili ni kwa sababu machapisho ya wataalamu mbalimbali wa ushairi yanatarajiwa kupatikana kwenye maktaba za vyuo. Kazi mbalimbali kama vile mashairi na tenzi mbalimbali, tasnifu zinazojadili maswala mbalimbali yanayowahusu vijana katika jamii, vitabu, majarida, na makala yaliyochapishwa yametusaidia katika utafiti wetu na kupitia tovuti kuhusu kazi

zinazozungumzia vijana kwa jumla. Kisha baadaye tulianza uchambuzi wa mashairi na kuona jinsi waandishi tofauti tofauti walivyoshughulikia maswala ya vijana. Pia tumesoma kuhusu nadharia ya uhalisia na kubainisha sifa zake kutoka maktabani na pia tulitumia yaliyomo katika mtandao kuhusu nadharia hiyo, dhana ya vijana na maswala yanayowakumba kwa jumla.

### 1.8.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data iliyokusanywa kwenye utafiti huu imechanganuliwa kwa njia ya maelezo na ufafanuzi kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Uchanganuzi wa data kuhusu maswala ya vijana na waandishi wanne tofauti umefanywa kwa njia ya mjadala huku tukitoa ushahidi kutoka kwenye matini husika. Baada ya data kuchanganuliwa matokeo ya uchunguzi kuhusu maswala ya vijana katika diwani ya *Tunu ya Ushairi* yamewasilishwa kwa njia ya maelezo na ufafanuzi.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura ya kwanza tumejadili usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na msingi wa nadharia ambao ni uhalisia na mwishowe mbinu tulizozitumia katika utafiti wetu.

# SURA YA PILI

# DHIMA YA USHAIRI, DHANA YA VIJANA NA MASWALA YANAYOHUSU VIJANA KATIKA JAMII.

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumejadili dhima ya ushairi katika jamii, dhana ya vijana na maswala yanayowahusu vijana katika jamii. Sehemu kubwa ya sura hii inahusu maswala yote kwa jumla vijana hukumbana nayo katika jamii na visababishi vya mambo hayo yote.

## 2.1 Dhima ya Ushairi Katika Jamii

Kulingana na Kaaru, M.G. (2008) utanzu wa ushairi ni maarufu sana katika fasihi za jamii nyingi ulimwenguni na umeendelea kuwapo kwa kuwa jamii inanufaishwa mno nao. Kwa mfano, katika jamii ya Waswahili ushairi ni maarufu sana na wenyewe una historia ndefu mno. Awali mashairi yalitongolewa majukwaani, kazini na faraghani kama fani ya fasihi simulizi.

Ushairi hutekeleza majukumu yafuatayo katika jamii kulingana na Kaaru (k.h.j.)

i) Kuibua hisia za kuburudisha au kuhuzunisha. Kulingana na Wamitila (2008), burudani inayopatikana katika kazi za kifasihi ni burudani inayoelimisha, kupevusha, na hata kufikirisha. Sifa kuu ya shairi ni kwamba sharti liguse hisia za msikilizaji kwa namna maneno na mapigo ya kimziki yalivyopangwa

ii) Kuhamasisha na kuzindua. Mashairi huwa na uwezo mkubwa wa kuchochea watu kiakili na kuwaamsha wapate nguvu mpya za kutenda

yawapasayo. Hii ndiyo sababu sehemu kubwa ya fasihi ya mapambano dhidi ya udhalimu wa ukoloni ilikuwa, na imezidi kuwa, mashairi.

iii) Kukosoa, kukashifu na kuadilisha. Hutumiwa kuwakashifu walio na tabia zisizofaa katika jamii na kuonyesha namna wanavyowaudhi raia.

iv) Kuelimisha. Mashairi hushauri na kutoa mwongozo bora kwa maswala mbalimbali ya maisha, kwa mfano Kasida ya Burudai.

v) Kuhifadhi matukio muhimu ya historia ya jamii. Mashairi ni kumbukumbu za mambo yaliyowahi kumpata mwanadamu katika awamu mbalimbali za maisha. Kwa mfano biashara, utumwa, ukoloni, dini mpya, vita, uhuru na matendo ya mashujaa na watu wengine mashuhuri. Kwa mfano, utenzi wa Al-Inkishafi unaeleza historia ya mji wa Pate tangu mwanzo, kustawi kwake, hadi kuporomoka.

vi) Ushairi ni pambo la lugha. Ushairi hutamalaki kwa matumizi ya msamiati teule na miundo adimu ya kisarufi. Hivyo basi, mashairi hukuza na kuieneza lugha.

vii) Kufikirisha na kunoa fikra. Shairi hutoa changamoto kwa hadhira. Humwongoza msikilizaji kuchukua mkondo wa fikira wa mtunzi na kumpa kutafakari kuhusu swala alilolizua. Aidha, baadhi ya watunzi hufumba mambo fulani kishairi kumwacha msikilizaji kuyafumbua. Kwa mfano katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* shairi kwa anwani jipu lina maana ya uchungu unaokera moyoni ambao ulianza siku nyingi zilizopita na unaendelea kumkera kama jipu linavyoanza kutunga mwilini na kuendelea kuwa kubwa na kuzidisha uchungu.

## 2.2 Dhana ya Kijana

Ufafanuzi wa maana ya dhana ya kijana unatofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Kulingana na Becker (2011) ujana ni kipindi cha mpito toka hali ya utoto hadi utu uzima. Anasema kuwa hiki huwa ni kipindi ambapo mabadiliko mbalimbali hutokea ndipo mtoto awe mtu mzima. Ni wakati mahususi ambao mabadiliko haya hutokea ingawa si bayana kwa mtu binafsi kwani jamii tofautitofauti huwa na mitazamo mbalimbali ya kitamaduni kuhusu mabadiliko hayo kwa namna zinavyotambua na kuwapa vijana mamlaka na uwezo wa kimaamuzi. Fasili zenye misingi ya kitamaduni, mila na desturi huzua utata na mkanganyo mkubwa sana katika kuielewa dhana nzima ya vijana kulingana na Becker k.h.j.

Erikson (1961:24) anasema kuwa,

> Vijana ni finomena ya kiulimwengu, ambayo huwa
> ni hali ya kibayolojia lakini inayofasiliwa kitamaduni.
> Tofauti zaki-umri hutumika kama vigezo vya kimaamuzi
> Katika maisha ya mtu na kwa vile tamaduni ulimwenguni
> huwakabidhi watu majukumu kwa misingi ya umri usio
> sawa ulimwenguni ni vigumu kusema kuwa kuna umri wa
> vijana kulingana na tamaduni zote ulimwenguni.(tafsiri yetu)

Kitamaduni, fasili ya vijana yaweza kutolewa kutokana na migao ya kazi walizotengewa na misingi ya kuwapa watu mamlaka na majukumu. Erikson anatambulisha majukumu ambayo vijana huhusishwa nayo. Kwa mfano, majukumu ya kijeshi hutengewa vijana kutokana na nguvu zao za kimwili.

Brown na Larson (2002), wanasema kuwa dhana ya ujana ni telezi na kwepevu kwa sababu ya utokubaliano kuhusu maumbile, tamaduni na vipindi vya wakati. Wanaainisha ujana kama kipindi cha maisha kilicho kati ya mwongo wa pili na wa tatu katika maisha ya mtu. Kwa mantiki hiyo ya Brown na mwenzake, umri wa vijana ni kipindi kilichopo baina ya miaka 11 na 29.

Mamuya (1974), anasema kuwa:

> Ujana ni ngazi ya maisha kuanzia kubaleghe
> au kuvunja ungo hadi kuwa mtu mzima
> kamili kuanzia miaka 11 hadi 25.

Kutokana na maelezo na ufafanuzi kutoka kwa wataalamu hawa na kulingana na uelewa wetu tumemchukulia kijana kama kiumbe mwanadamu aliye katika kipindi cha mpito cha kutoka utotoni na kuelekea utu uzima ambacho kinaweza kufasiriwa katika misingi ya kiumri. Kwa vile msingi wa ufasiri wa vijana kitamaduni unaweza kuzua utata mwingi, katika utafiti huu tumetumia ule wa ki-umri ambao kama tutakavyoona pia, una utata wake.

Umoja wa Mataifa unamtambulisha kijana kama mvulana au msichana mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 24; (Ripoti ya Kimataifa kuhusu vijana ya 2011). Nayo Jumuiya ya Madola, ambayo Kenya ni mwanachama wake humchukulia kijana kama mtu mwenye umri wa kati ya miaka 16 hadi 29. Kulingana na mkataba wa makubaliano ya vijana wa Muungano wa Afrika yaani AU, kijana ni mtu mwenye umri wa baina ya miaka 15 hadi 35. Kulingana na sera ya kitaifa kuhusu kijana nchini Kenya, kijana ni mtu yeyote

ambaye umri wake ni baina ya miaka15 hadi 30. Haya ni kutokana na Tarakimu za Wizara ya Vijana na Michezo iliyobuniwa mwaka wa 2008. Kwa misingi hii na kuzingatia sensa ya mwaka wa 2009, zaidi ya asilimia sabini ya watu wote nchini Kenya ni vijana. Katiba ya Kenya (2010) inamtambua kijana kama mwananchi mwenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 35. Kutokana na fasiri hizi tofauti, ni wazi kuwa kuna utata na mkanganyo mkubwa kuhusu ni lini kipindi cha ujana kinaanza na kuishia.

Tunapotumia kigezo cha ki-umri kufasiri kijana ni nani kwa mujibu wa tasnifu hii, tumetumia kigezo cha ki-umri licha ya utata ulioko. Hii ni kwa sababu kile cha kitamaduni huzua utata mwingi zaidi. Tumetumia mseto wa viwango vya umri vilivyowekwa na mkataba wa Makubaliano ya Vijana wa Umoja wa Mataifa ya Kiafrika yaani A.U, miaka 15-35 na Katiba mpya ya Kenya ya mwaka wa 2010 ambayo inaweka vijana kama watu walio kati ya umri wa miaka 18-35. Hii inaturuhusu kuchukuwa kiwango cha chini baina ya hizi mbili ambayo ni miaka 15, na kile cha juu ambacho ni sawa kubaki hivyo, yaani miaka 35. Kwa kufanya hivyo, tumefasiri vijana kama viumbe wa kiume au kike walio kati ya umri wa miaka 15 hadi 35.

Majukumu ya vijana katika jamii yamekuwa yakibadilika jinsi hali ya jamii inavyoendelea kubadilika vilevile. Kwa mfano, katika mfumo wa maisha ya kiasili ya Mwafrika kabla ya maajilio ya wageni na elimu ya Kimagharibi, malezi ya vijana pamoja na kuwaelekeza katika jamii yalikuwa ni wajibu wa jamii nzima. Hii ni kwa sababu watoto walikuwa ni mali ya jamii. Tabia potofu miongoni mwa vijana zilishutumiwa na watu wote kwa vile maisha yalikuwa ni ubia au ushirika. Watoto walikuwa chini ya jicho

pekuzi la jamii nzima kila wakati. Majukumu ya vijana vivyo hivyo yalikuwa bayana huku vijana wa kiume wakiandamana na wazazi wao wa kiume waliowafunza shughuli za kiume kama vile uwindaji na jinsi ya kuihami jamii hata kuikidhia familia yake mahitaji akishaoa. Wasichana nao walifundishwa mambo ya unyago yaliyozingatia utekelezaji kamilifu wa majukumu yao wakishaolewa. Katika hali hii ya maisha ya kitamaduni, vijana hawakuwa na changamoto nyingi kwa sababu kulikuwa na utaratibu wa kuwaelekeza kulingana na kila jamii, Erikson (1961).

Mfumo huu wa kiasili ambao ulijikita katika taratibu za tamaduni maalum ulivurugwa na majilio ya wakoloni pamoja na wageni wengine kutoka nchi za Kimagharibi. Mtagusano na wageni hawa ulivuruga utaratibu wa mifumo ya ulezi ambayo ilikuwako. Elimu ya Kimagharibi ilileta mambo mapya na hata kuvuruga thamani pamoja na maadili katika jamii. Kwa mfano,vijana walilazimika kwenda shuleni na vilevile wazazi wao kutafuta kazi katika sehemu za miji ili kukidhi mahitaji mapya yaliyotokana na njia hizi mpya za maisha. Jinsi jamii zetu zilivyoegemea zaidi kuelekea utaratibu wa maisha ya Kimagharibi ndivyo asasi zilizohusika moja kwa moja na malezi ya vijana katika jamii zilivyoendelea kuporomoka na hivyo kuwaacha vijana bila mwelekeo maalum wa kuwafunza maadili.

Jamii ya kesho inategemea vijana ambao ndio msingi wake. Iwapo basi msingi huo ni dhalili na unakosa uthabiti, basi taifa nalo linakosa matumaini. Baada ya uhuru kupatikana viongozi walioshika hatamu hawakuweka chini sera kabambe kuweza kushughulikia hususan maisha ya vijana. Hata waandishi wa kifasihi katika maandishi

yao ya hapo nyuma hawakuwachukulia vijana kwa dhati sana katika uandishi huo ambapo majukumu yao ya uhusika hayakuwa muhimu sana. Nchini Kenya, waandishi wasomi wengi wao wakiwa wahadhiri katika vyuo vyetu ndio wamechukua jukumu la kuangazia maswala ya vijana. Haya yamedhihirika katika riwaya kama vile *Nguvu ya Sala* (Wamitila 1999) na *Tumaini* (Momanyi 2006), tamthilia kama vile *Maua Kwenye jua la asubihi* (Kithaka wa Mberia 2004) na *Pango* (Wamitila 2003).

Hata hivyo diwani ya *Tunu ya Ushairi* inajitokeza kama kazi ambayo imeangazia kabisa matatizo yanayowakumba vijana katika jamii na jinsi ambavyo waandishi hawa wanne wameshughulikia maswala ya vijana.

## 2.3 Maswala Yanayowahusu Vijana katika Jamii

Maswala haya ni jumla ya maudhui yanayowahusu vijana katika jamii. Msanii katika utunzi wa ushairi hutumia maudhui kadha kuwasilisha dhamira yake. Tujuavyo, maudhui ni jumla ya fikra, mawazo, mitazamo na ujumbe muhimu anaowasilisha mwandishi katika kazi yoyote ya fasihi Wamitila (2002). Ni mambo ambayo kwayo mwandishi hudhamiria kumuasa, kumuonya, kumuelimisha, kumzindua na kumfichulia msomaji uhalisia wa ulimwengu unaomzunguka. Hii ina maana kwamba maudhui ni mafunzo au ujumbe uliomo kwa minajili ya jamii kwa jumla. Ni kupitia kwa maudhui ambapo kazi ya fasihi hupata dhima kuu katika jamii. Kulingana na Njogu, K. na Chimerah, R. (1999), maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi kama vile ushairi, riwaya, tamthilia na kadhalika. Wanaendelea kusema kuwa maudhui ni sehemu ya maana na huingiliana na mada. Ni

katika maingiliano baina ya mada na maudhui ambapo ukweli uliokusudiwa na mwandishi hujulikana. Kwa hivyo, maswala yanayowahusu vijana katika jamii ni mengi na yamejitokeza kwa njia mbalimbali. Baadhi ya maswala hayo ni kama vile matumizi ya mihadarati na ulevi, ukosefu wa elimu bora, ukosefu wa maadili, umaskini, maradhi ya ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa, ukosefu wa malezi bora na ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana.

### 2.3.1 Matumizi ya Mihadarati na Ulevi

Ni jambo la kusikitisha mno tunapoona jinsi vijana wanavyojitumbukiza katika janga la kutumia, kusafirisha, au kuuza mihadarati kwani vijana ndio nguzo na matarajio ya taifa lolote. Pia ni huzuni sana kuona jinsi vijana wanavyoghilibiwa na ulimwengu wa sasa kwa kujitumbukiza katika kina cha utumiaji wa madawa za kulevya. Ni matarajio ya umma wowote kuwakuta vijana wakitumia nguvu zao katika kuimarisha na kulijenga taifa badala ya kuzama katika shughuli za madawa ya kulevya na ulevi kwa jumla. Tujuavyo madawa ya kulevya ni kitu chochote ambacho huharibu fahamu au kuathiri mwili baada ya kukitumia na kumfanya mtumiaji kudhoofika kiakili.

Wimbi hili la kutumia mihadarati limeingia kwa kasi kubwa kama tunavyoona kwenye vyombo vya habari nchini tarehe 5-08-2015. Baada ya wanafunzi kufunga shule kwa likizo ya muhula wa pili waliamua kujikusanya pamoja na kuabiri basi moja kuelekea nyumbani. Cha kushangaza ni kwamba kilichopatikana katika basi walilokuwa wakisafiria ni madawa ya kulevya yaliyotumiwa na wanafunzi hawa bila kubagua jinsia. Kulingana na gazeti la "*The Standard*" tarehe 12-08-2015 kati ya hao wanafunzi

walioshikwa na *bangi* mmoja wao ambaye ni banati amehukumiwa kifungo cha miezi 18 baada ya kukiri kupatikana na makosa hayo. Mara nyingi mambo yanayochangia matumizi ya madawa ya kulevya na ulevi kwa jumla ni uhaba wa kazi, ukosefu wa mwelekeo kwa vijana, athari za shinikizo la rika, kupata matokeo mabaya shuleni na wengine huzitumia kama njia ya starehe. Ajabu ni kwamba hata wengine wamekuwa maajenti na mawakala wa kuwauzia matajiri madawa haya ya kulevya.

Kuna aina mbalimbali za madawa ya kulevya kama vile kokeini, heroini, marijuana au bangi, mandraksi, hashishi, miraa, gundi, sigareti na pombe. Madawa haya hutumiwa kwa njia mbalimbali. Kuna yale ambayo huvutwa, kuna mengine yanatafunwa na mengine hata kudungwa mwilini kwa kutumia sindano. Kuna mengine ambayo ni "unga unga" asili yake ikiwa Bara Hindi, na hujulikana sana kama *Kuber* miongoni mwa vijana na hutumiwa kwa njia ya kumumunya. Vijana wengi huitumia bila kutambuliwa hata wakiwa kwenye darasa. Madawa haya kwa jina moja huitwa mihadarati.

Madawa haya ni hatari kwa maisha ya mtumiaji kwa kuwa huvuruga akili zake na kumfanya mtu kukosa utu na kumgeuza hayawani. Wengine huwa makatili kupita kiasi wakaanza kutenda visanga visivyo na mipaka kama vile ujambazi, ukahaba, uasherati, ubakaji na hata kuua na kuwachinja watu kama kuku! Wengine hata huwabaka ngo'mbe au kuku! Hivyo, humfanya mtu atende na kusema mambo bila kufikiria.Watu wengine hupika pombe haramu; na katika harakati za kupika pombe hiyo wanatumia kemikali hatari zaidi kwa maisha. Kemikali hizi huangamiza maisha na hata kupofusha macho pamoja na kupunguza nguvu za kiume. Hii imedhihirika wazi haswa sehemu za Kati nchini Kenya mahali ambapo kina mama vijana wanalalamika wazi kwamba waume wao

wamekuwa bure kabisa katika kutimiza majukumu yao ya ndoa. Pombe hizi zimebandikwa majina maalum kama vile *kumi kumi*, *jeti*, *kalikali*, *munyeki*, *changaa* na jina moja kwa jumla hujulikana kama "second generation".

Mbali na kuvuruga akili na kupofusha, mihadarati hii ina madhara mengine chungu nzima. Haya ni pamoja na uovu katika jamii, kudhoofika kwa afya, utovu wa nidhamu na heshima, magonjwa ya zinaa hasa ukimwi na uraibu. Madawa ya kulevya hudhoofisha afya ya mtumiaji na kumfanya wakati mwengine kukonda na kukondeana. Afya inapozorota, ni rahisi sana mtu huyo kuambukizwa maradhi mengineyo kwa kuwa mwili hauna kinga ya kutosha. Ni rahisi sana mtumiaji kuaga dunia.

Nidhamu na heshima ni kitu johari sana katika maisha ya mwanadamu. Unapokosa taadhima, ni rahisi sana kutatizika maishani bila ya kumpata mhisani wa kukuamini. Matumizi ya madawa haya huwageuza wengi kuwa watumwa wa vileo hivi. Wengine hata hushiriki wizi hasa katika nyumba za watu ili wapate hela za kununua pombe, na hivyo wakakosa hadhi kwa matendo yao yasiyo ya heshima wala utu. Badala ya kuheshimiwa, wao hubandikwa majina ya lakabu yanayowashushia hadhi. Hubandikwa majina kama vile *mabangi', 'mpaliza hashishi ','mnyonya mrija,' 'mandraksi'* na majina mengine ya kumvunjia heshima.

Mihadarati huwafilisisha watumiaji na kuwaacha fukara, wasio na mbele wala nyuma. Wao hufurahia afyuni hizo kwa sababu huwapumbaza akili na kuwasahaulisha masaibu ya wakati huo; wakatanua vifua vyao na kujishaua jinsi walivyo madume wa madume au hodari katika kila kitu. Lakini wao husahau kwamba hiyo huwa tu ni ndoto ya muda

mfupi kwani wanapolevuka, hujipata shida zao zimeongezaka maradufu. Hela zote zimetumika kununuliaa dawa hizi, hata wengine huacha familia zao bila ya kuwatosheleza mahitaji muhimu kama vile chakula, mavazi, makazi na elimu. Isitoshe, miili hubakia minyonge sana licha ya kuwa na maruerue na akili kuathirika kisaikolojia. Wanaotumia madawa ya kulevya ndio wanaochangia pakubwa katika uenezaji wa magonjwa ya zinaa na ugonjwa hatari wa ukimwi pamoja na kuzoroteka kwa maadili katika jamii.Wengi wao hawajali wanayoyasema wala wanayoyatenda.Wengi wamesheheni cheche za matusi machafu yanayofedhehesha ajabu. Hushiriki katika anasa na mapenzi kiholela maanake huwa wamelewa chakari, hawajijui hawajitambui. Baadhi yao huvaa mavazi ya aibu sana, wakatembea huku wakiwasalimu hata mbuzi barabarani na kucheka ovyoovyo wanapozurura.

Kunao pia wale wanaotumia ugoro, sigara na tambuu. Hawa pia huathirika sana kwani wanapovikosa vitu hivi, akili zao huwa hazifanyi kazi barabara.Watavitafuta vileo hivi mpaka wavionje ndipo wakate kiu na kudai eti sasa watafanya mambo yao barabara kwa kuwa vileo hivyo ni dawa mujarabu! Huu ni upuzi mtupu na utumwa wa vileo. Uraibu hukereketa kooni na vilevile husababisha maradhi ya saratani. Watu wengi wamepoteza maisha yao kutokana na athari ya sigara. Mihadarati kwa jumla hukuza uhalifu, uzembe, maradhi na maafa mengine mengi katika jamii.

Kutokana na fafanuzi tulizotoa kuhusu athari hasi za matumizi ya madawa ya kulevya ni muhimu katika utafiti wetu kuangaza zaidi jinsi ya kusuluhisha matatizo hayo. Aidha tunachunguza jinsi waandishi mbalimbali katika diwani ya *Tunu ya Ushairi* wanavyoshughulikia maswala haya, jinsi wanavyofanana na kutofautiana.

### 2.3.2 Ukosefu wa Elimu Bora

Elimu ni mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni, vyuoni na maishani. Elimu imekuwapo tangu jadi na asili. Kuna elimu ya maarifa na ujuzi ambayo mababu zetu walisoma. Walifunzwa mbinu kuhusu maarifa mbalimbali, wakapata taaluma na ufundi uliowawezesha kuishi maisha ya raha mustarehe. Walikuwa na akili murua za kutambua mambo.

Elimu huondoa ujinga akilini na wanafunzi wote shuleni hufunzwa maarifa na ujuzi anuwai kuhusu mambo tofautitofauti. Wao hutambua na kumakinika kuhusu namna ya kufanya mambo hatua kwa hatua. Hali kadhalika, mtu anayepata elimu huwa mwerevu kinyume na asiyepata elimu ambayo yeye hubaki kama zuzu. Elimu bora humfanya mtu kuhitimu katika taaluma mbalimbali kama vile udaktari, uhasibu, urubani, ualimu, uandishi, uanasheria na taaluma nyinginezo. Kukosa elimu katika karne hii humtia binadamu katika mikururo ya mikasa, (Murono S.E.2005).

Watu wa zamani walibadilishana mawazo na kufunzana hekima huko jandoni na unyagoni. Wavulana walielimishwa na mababu zao ilhali wasichana walielimishwa na nyanya zao. Walifunzwa kuhusu Mungu na wajibu wao kwa Mungu. Walifunzwa pia uadilifu, heshima, bidii kazini, kunga za ndoa, ukarimu, iktisadi, ushirikiano, uvumilivu na mambo mengine mengi, na hii hali ilichangia sana kuishi kwa amani, mapenzi na umoja kinyume na mambo yalivyo sasa.

Siku hizi kuna elimu ya kusoma na kuandika, kinyume na jinsi mambo yalivyokuwa zamani kabla ya mfumo wa kwanza wa elimu kuanzishwa nchini Kenya. Mtu yeyote anayezingatia na kuthamini elimu anaweza kusoma vitabuni yaliyoandikwa na wajuzi na

wataalamu mbalimbali, kisha baadaye akaerevuka na kuishi maisha yatakayomwezesha kukumbana na changamoto za maisha. Elimu pia huleta umoja. Wanafunzi kutoka katika matabaka mbalimbali na nchi mbalimbali hukutana shuleni ama vyuoni na kutangamana vizuri bila ubaguzi wowote. Wote huchukuana kama ndugu wa ukoo mmoja.Maendeleo ya jamii nzima hutegemea wenye elimu kwa hivyo ni bora kila kijana apate elimu nzuri maana watu waliosoma na kuwa weledi wa taaluma fulani huwa na akili na maarifa ya kuinua uchumi wa nchi na kuwafanya wananchi kuishi maisha yaliyo bora. Mara nyingi vijana hukosa ajira kwa kukosa elimu iliyo nzuri.

Elimu rasmi ya Kimagharibi nchini Kenya ilianza zamani sana,Wamishonari walijiunga na watu wa pwani mjini Mombasa na wakaanza shule huko Rabai. Kenya ilianza kampeni ya elimu ya bure baada ya kupata uhuru 1963. Basi tangu wakati huo mfumo wa elimu umekuwa ukibadilikabadilika. Mwaka wa 1985 Rais mstaafu Daniel Arap Moi alitangaza mfumo mpya wa elimu 8-4-4 ambao unachukua miaka minane katika shule ya msingi, miaka minne katika shule ya upili na miaka minne katika chuo kikuu. Mfumo huo huo ndio unatumika hadi sasa. Mwaka wa 2003 mwezi wa kwanza Januari, Rais wa tatu nchini Kenya ambaye pia alistaafu mwaka wa 2013, alitangaza elimu ya bure na ya lazima kwa kila mtoto nchini Kenya kulingana na katiba ya Kenya (kifungo cha 53), ambayo ilikuwepo mwanzoni kabisa. Baadaye serikali ya Kenya ilichukua jukumu la kujua jinsi ambavyo elimu hiyo ya bure inaendelezwa na kama imefanikiwa kupitia kwa "Kenya Education Sector Support Programme" 2005-2010 kwa kuunda shirika linalojulikana kama "National Assessment Centre" (NAC). Mwaka wa 2009 Uwezo Kenya pamoja na NAC walifanya utafiti huo na kupata matokeo ambayo si ya kuridhisha.

Mwanzo kabisa waligundua kwamba sehemu nyingi za Kenya wasichana hufanya vizuri katika lugha yaani Kiswahili na Kingereza ilhali wavulana hufanya vizuri katika hisabati. Sehemu zingine za nchi hata kama elimu ni ya bure watoto wengine hawahudhurii masomo shuleni sababu ikiwa kwamba mila na desturi haziruhusu hasa mtoto wa kike kupata elimu. Katika sehemu hizi za nchi, vijana wa kike yaani wasichana huozwa mapema na hulelewa kama kitega uchumi. Sehemu hizi ni kama Kaskazini Mashariki na sehemu zingine za Bonde la Ufa. Sababu nyingine ya vijana kukosa elimu huchangiwa na vita vya kikabila kwa hivyo wazazi na watoto wanalazimika kuhama nyumbani wasije wakavamiwa. Baadhi ya vijana hujihusisha katika vita hivyo na uhalifu kwa jumla na kwa hivyo kukosa wakati wa kuhudhuria masomo kama wanafunzi wengine katika sehemu zingine za nchi.

Wakati mwingine umaskini ni janga kubwa linalochangia sana wanafunzi kukosa kwenda shule, umaskini ni adui mkubwa sana katika sekta ya elimu maana husababisha njaa ambayo inachangia mno mtoto kukosa shule. Kwa sababu elimu ni ya bure,wanafunzi ni wengi shuleni ikilinganishwa na idadi ya walimu, kwa hivyo nchini Kenya kuna uhaba wa walimu na hii ni changamoto kwa watoto wa taifa la Kenya na vijana kwa jumla. Kwa hivyo ukosefu wa elimu ni tatizo kubwa linalowakabili vijana katika jamii maana bila elimu umaskini utaendelea kuongezeka, uhalifu utazidi na hata matumizi ya madawa ya kulevya. Pia, ndoa za mapema zitakuwa mstari wa mbele kwa sababu elimu huchukua muda mwingi kwa mwanafunzi, kwa hivyo bila elimu vijana watafikiria tu maisha ya ndoa wakiwa katika umri mdogo.

### 2.3.3 Ukosefu wa Maadili

Maadili ni hali ya kuwa na mwenendo mwema, kwa hivyo ukosefu wa maadili ni kinyume cha kuwepo kwa mwenendo mwema. Mara nyingi vijana hupenda mambo makubwa zaidi ya yale waliyo nayo. Hupenda kutofungwa na sheria yoyote ili wapate kufanya mambo jinsi wapendavyo. Lakini hivi sivyo; mtoto hana budi kutii kanuni za nyumbani na ni lazima amkabili baba na mama kwa adabu. Lazima afundishwe utu na kuutambua. Kuna mambo mengi ambayo yanachangia katika vijana kukosa maadili katika jamii.

Watu wa hapo awali walibadilishana mawazo na kufunzana hekima wakiwa kule jandoni na unyagoni, maana sherehe kama hii ilikuwa ni ya jamii. Kinyume na sasa kwa sababu ya ubinafsi ambao umekita mizizi wakati huu. Lakini cha kusikitisha ni kwamba mifumo hiyo ya utamaduni katika mipangilio ya familia imeporomoka kabisa. Zamani kila mtoto alikuwa ni wa jamii yaani mali ya jamii na watoto walikuwa wanamheshimu kila mmoja kama mzazi wake. Siku hizi mambo ni tofauti kila mzazi ana jukumu la kumlea mtoto wake mwenyewe, na la kuhuzunisha wazazi hawana wakati huo maana wengi wamefungwa na kazi mbalimbali zinazowatenganisha na watoto wao. Watoto wengi hujifunza mambo kutoka kwa wafanyakazi wa nyumbani, majirani, televisheni, tarakilishi, na sinema. Yaani kwa ufupi teknolojia imechukua nafasi ya wazazi na walezi katika ufundishaji wa maadili.

Walimwengu wamekuwa wakipiga hatua kiteknolojia kila uchao na ni kweli kwamba ndiyo humwezesha kuishi maisha bora. Enzi hizi, vifaa vingi vimebuniwa ili kuboresha maisha ya watu na kurahisisha mawasiliano. Miongoni mwa vifaa hivi ni runinga na

tarakilishi. Ingawa mtandao kwa jumla hurahisisha mawasiliano na mambo mengine mengi, huja pia athari na madhara mengi kwa vijana katika jamii. Athari za mtandao ni nyingi sana kwa vijana katika jamii kwa jumla. Vijana huona na kuiga mambo mengi ya uzunguni na kama tujuavyo tabia za kigeni ni tofauti sana na za Kiafrika. Mambo haya huchangia kuzorota kwa maadili na tamaduni asili za Mwafrika. Maadili ya Mwafrika yamezikwa katika kaburi la sahau.

Katika utamaduni wa Kiafrika vijana wa kike hawakuruhusiwa kustarehe pamoja na wazee hasa wakati wazee walipokuwa katika sherehe ambapo wangetumia pombe na vinywaji vinginevo vilivyoruhusiwa wakati huo. Hali ni kinyume sasa, kwani vijana ndio walio katika mstari wa mbele kuonja aina mbalimbali za vileo vinavyouzwa kwa njia halali au isiyo halali. Na hali hii ya ulevi kwa vijana imeathiri hata maisha ya ndoa. Zaidi ya hayo, vijana, kutokana na uigaji wa tabia kutokana na athari za teknolojia kama vile kwenye runinga, tarakilishi, filamu, mtandao kwa jumla hutumia maneno ya kufedhehesha bila kujali wanaowazungumzia au umri wao.Vijana wameathirika kimavazi na hata kitabia. Sinema ambazo huonyesha watu wanaopigana na kufanya uhalifu na ujanja mwingi hufanya vijana wetu kudhani kuwa kupigana ndiko kunakodhihirisha nguvu, ustadi na umahiri wa mtu. Vijana hawa huambukizwa tabia za kupigana pamoja na ujanja na uhalifu mwingineo ili kuonyesha umaarufu wao kwa wengine.

Kupigana huku husababisha ukosefu wa amani na hatimaye huwafanya vijana hawa wahalifu sugu. Vijana wa siku hizi wamepevuka katika mambo ambayo hawastahili kuyajua katika umri wao mchanga. Mathalani, utawapata watoto wadogo wakiwa na hisia za mapenzi na hata wengine kubusiana na kufanya mapenzi. Haya hutokana hasa na

picha wanazozitazama kwenye runinga, sinema, tarakilishi na majarida mbalimbali. Vijana wameiga mambo ya mapenzi kati ya jinsia moja na baadaye kugeuka kuwa masago, mashoga, mende au wasenge, Visanga kama hivi ndivyo vinavyochangia kueneza ugonjwa hatari wa ukimwi. Haya ni mambo ambayo Waafrika hawakuyajua kamwe! Vijana wanajidai eti ni watu wazima na hivyo hupuuza mashauri ya wakubwa wao.

Aidha, runinga, tarakilishi na sinema huathiri sana masomo ya vijana. Wanafunzi wengi hujipa starehe kwa kutazama vipindi mbalimbali na hata kucheza michezo kwenye mtandao kuliko masomo, hivyo huponza muda mwingi ambao ungetumiwa kudurusu masomo ya shuleni. Mitihani inapowadia, wanafunzi wawa hawa hufeli na hatimaye kukosa kazi nzuri maishani. Kwa sababu pia ya kutochukua muda mwingi masomoni utagundua kwamba, wanafunzi hawa ndio hupanga migomo shuleni na hata vyuoni kwa sababu hawajajitayarisha ipasavyo katika mitihani yao. Kwa ufupi ni kwamba maadili ya vijana katika jamii yamezorota kwa kiasi kikubwa na hatua ya dharura lazima ichukuliwe ili kusuluhisha janga hili.

### 2.3.4 Umaskini

Hii ni hali ya kukosa mali na kwa hivyo kuwa fukara. Umaskini umekuwa ni kama janga kubwa sana katika jamii kwa maana watu wengi nchini ni maskini kuliko matajiri. Kwanza kabisa hii ni shida ambayo ilianza kitambo sana na wakoloni kisha na viongozi wetu.Wakati ambapo viongozi wanagawa raslimali za kitaifa hakuna usawa kabisa.

Sehemu zingine za nchi kuna mashamba makubwa makubwa ilhali sehemu zingine zina mashamba madogo sana.

Tukio la ukoloni lilileta sera ya ubinafsishaji wa miliki jambo ambalo halikuwepo tangu hapo awali. Walowezi walinyakua ardhi kubwa kubwa na kujinafsisha na waliwaajiri Waafrika katika mashamba yayo hayo kama watumwa wao na malipo yalikuwa duni. Baada ya wakoloni kuondoka na Waafrika kujinyakulia uhuru, waliochukua mamlaka kama viongozi wa Kenya hawakuwa tofauti na wale mabeberu maana walifuata mwenendo ule ule wao na kwa hivyo kujitajirisha wenyewe na kusahau wengine. Hali hii imeendelea kutoka kizazi kimoja hadi kingine na vijana wameathirika mno. Hili ni tatizo ambalo Tume ya Haki na Maridhiano inajaribu kabisa kukabiliana nalo kwa misingi ya dhuluma na uonevu wa kihistoria nchini mwetu.

Jambo lingine ambalo pia limechangia umaskini nchini Kenya kwa kiasi kikubwa ni ongezeko la idadi ya watu. Kulingana na tarakimu za sensa za wakati wa kunyakua uhuru (1963) idadi ya watu nchini Kenya ilikuwa milioni nane tu, tangu huo wakati hadi sasa ni miaka 52, idadi imeongezeka mara tano kuonyesha kwamba kila baada ya miaka kumi idadi ya watu inaongezeka zaidi kwa watu milioni tano. Kulingana na tarakimu za halmashauri ya taifa la Kenya (2013) idadi ya watu ni milioni 38.6, katika hali hii vijana wanaendelea kurithi umaskini ambao kwa kiasi kikubwa utaendelea kudumu milele.

Jambo lingine linalochangia umaskini nchini Kenya ni ukame. Katika kaunti nyingi nchini kuna ukame unaochangiwa  zaidi na ukosefu wa mvua.Utakuta kwamba kaunti hizi zina mashamba makubwa makubwa lakini kwa sababu wanategemea maji ya mvua

hawana chakula kwa sababu ya ukosefu wa mvua. Serikali imesahau kaunti hizi kabisa na ndio sababu vijana katika sehemu hizi hawaendi shule na hili linaendelea kuchangia umaskini katika sehemu hizi. Kwa hivyo vijana wamebakia kuwa maskini hata hawawezi kutimiza majumu yao kama wazazi .

### 2.3.5 Maradhi ya Ukimwi na Magonjwa mengine ya Zinaa

Neno "Ukimwi" ni akronimu ya muungano wa maneno haya Ukosefu wa Kinga Mwilini. Huu ni ugonjwa ambao umekuwa ukimghasi na kumsumbua binadamu kwa miaka kwa vile hauna tiba. Maradhi haya huambukizwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa njia nyingi sana. Wakati mwingine mzazi mhasiriwa humwambukiza mtoto wakati wa kujifungua au mgonjwa aliyepungukiwa na damu mwilini anapoongezewa damu zaidi, huenda hiyo damu ikawa imeambukizwa viini vya ugonjwa huu na hivyo huhasiriwa.Njia nyingine watu hupata ugonjwa huu ni kupitia utumiaji wa kifaa kimoja cha kukatia au kunyolea kama vile wembe ama kisu. Lakini kando na haya yote ile hatari ni kujiingiza katika ngono bila kinga na vijana wetu wameathirika zaidi na janga hili la ukimwi.

Serikali hutumia pesa nyingi inapojitahidi kugharamia matibabu ya waliohasiriwa. Hali hii huifanya serikali kuwa fukara zaidi na kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu muhimu. Mbali na hayo, serikali pia hutumia mipango kabambe ya kuelimisha wananchi kuhusu maradhi haya. Serikali hulazimika kuagiza mipira ijulikanayo kama kondomu ya wananchi kutumia ili kujikinga dhidi ya ugonjwa huu ingawa bado wengi hawaitumii kwa sababu ya kupuuza.  Kuzorota kwa maadili katika jamii huchangia pakubwa katika kuenea kwa ukimwi. Walioambukizwa maradhi haya hushikwa na kichaa cha kutaka

kulipiza kisasi. Wao hujiingiza katika anasa kiholelaholela ili kutosheleza nafsi zao na pia kutaka kuuambukiza ugonjwa huo kwa wengine. Mabwanyenye hutumia ukwasi wao kuwateka bakunja na kuwazaini vijana wadogo kufanya mapenzi nao. Uwele huu umeenea kote na unazidi kusambaa. Umesababisha ndoa nyingi kuvunjika maana vijana wapendanao wanapofunga pingu za maisha hula kiapo kuishi pamoja. Lakini pindi igunduliwapo tu kwamba mmoja wao ana virusi vya ukimwi, mitarafuku na mafarakano huzuka. Tetesi, lawama na shutuma hufuatia na hatimaye ndoa huvunjika; mke na mume hutengana.

Vijana wengi wameathirika sana na janga hili la ugonjwa wa ukimwi kwa njia moja au nyingine. Vijana wetu hujiingiza katika mambo ya anasa kwa sababu mbalimbali. Kwanza kabisa, ukosefu wa ajira husababisha vijana kukaa tu bila kufanya lolote na hili linafanya wajiunge na vijana wengine katika mambo ya anasa au hata watu waliowazidi umri.

Ukimwi na umaskini ni maswala yenye uhusiano wa karibu sana. Familia nyingi nchini Kenya zinaishi maisha ya umaskini sana. Kwa hivyo utamkuta msichana wa umri mdogo akijihusisha na babu mzee ambaye anajulikana kama baba sukari ili kutosheleza mahitaji yao kama vile chakula, mavazi na mengine. Hii sio tu kwa vijana wa kike bali hata vijana wa kiume, wao hujihuzisha na wale wanaojulikana kama mama sukari. La kustaajabisha ni kwamba wahasiriwa wengi ni wale walio na umri wa makamo na wenye taaluma mbalimbali katika nyanja tofauti. Kwa hivyo huwalaghai vijana na kuwaambukiza ugonjwa huu hatari wa ukimwi.

Vijana wengine huachwa kama mayatima na wazazi wao baada ya kufa kutokana na ukimwi, kwa hivyo wanawachwa bila makao, chakula, mavazi pamoja na elimu. Hii inakuwa changamoto kubwa sana na huchangia kwa mambo mengi mabaya ambayo tumekwisha taja hapo juu. Wengine huambukizwa na wazazi wao wakati wa kuzaliwa na kijana yuyu huyu anaambukiza wengine kwa kujiingiza katika anasa. Njia nyingine vijana wanapata ugonjwa huu ni wakati ambapo wanajihusisha katika utumizi wa dawa za kulevya na ni dhahiri kwamba kiwango cha kuambukizwa ugonjwa huu wa ukimwi kinaendelea kuongezeka kila uchao. Hili ni kutokana na matumizi ya sindano moja miongoni mwa vijana wanapojidunga kwenye mishipa madawa hayo ya kulevya. Kwa hivyo ugonjwa huo huenezwa na kusambazwa miongoni mwa vijana pamoja na magonjwa mengine ya zinaa.

Dawa za kulevya pia huchangia mambo ya anasa. Dawa hizi huwapumbaza na kuwatoa katika ulimwengu halisi na kuingia katika ulimwengu dhahania. Hapo wanaweza kutekeleza chochote kikiwemo kujiingiza katika anasa na hapo kuambukizwa ukimwi pamoja na magonjwa mengine ya zinaa.

Jambo lingine pia ambalo huchangia katika kueneza ugonjwa huu hatari ni shinikizo la rika. Vijana wengi hupotezwa na vijana wenzao ambao tayari wamepotoka kabisa. Vijana hudanganyana kwa njia moja au nyingine ili waweze kukubalika katika kundi fulani. Kwa sababu hakuna kijana anayetaka kuwa katika hali ya upweke basi anakubali kujiunga na wengine katika mambo yote wafanyayo wengine wa rika lake. Mtandao pia umechangia sana uenezaji wa ukimwi. Vijana wengi hutazama sinema kwenye mtandao na wanaiga yale yote ambayo wanayaona pale. Kwenye mtandao kuna mambo mengi

machafu yasiyokubalika katika mila na desturi za Kiafrika lakini vijana wanapuuza hayo yote na kuiga kile waonacho kikifanywa na wazungu. Kwa hivyo ugonjwa wa ukimwi ni swala la kutisha miongoni mwa vijana.

### 2.3.6 Ukosefu wa Malezi Bora

Malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kufuata tabia na mwenendo unaostahili. Hata hivyo Naliaka (2012) anasema kuwa, “malezi ni mchakato changamano sana ambao unajumuisha mambo kadhaa yakiwa ni lishe bora, mavazi, makao, elimu pamoja na ushauri ambao ni mwafaka”. Wakati ambapo tunazungumzia asasi ya ndoa na kisha familia tunachukulia kwamba familia kamili ina watu wafuatao; baba, mama na watoto watakaozaliwa kama baraka kwa baba na mama. Ni katika msingi huu ambapo watoto wanatarajiwa kupata malezi bora.

Familia ni asasi muhimu sana katika malezi ya watoto. Pale ambapo wazazi wote wawili wanashirikiana utapata kwamba watoto hawa wana mwelekeo na mwongozo mzuri lakini pale ambapo wazazi hawashirikiani utagundua kwamba kuna matatizo chungu nzima. Kimsingi  familia imefungamana na asasi ya ndoa ambayo inaaminika ilianzishwa rasmi na Mwenyezi Mungu wakati wa uumbaji wa binadamu wa kwanza,yaani Adamu na Hawa kulingana na bibilia takatifu. Baada ya ndoa watoto huja kama baraka kutoka kwa mwenyezi Mungu kwa hivyo ni haki ya mtoto kupata malezi mema kutoka kwa wazazi na ni jukumu la wazazi kuwalea watoto wao vizuri kwa kuwapa malezi yanayofaa.

Ni kweli kwamba vijana ndio nguzo ya taifa na wao ndio viongozi wa sasa na hata baadaye yaani kesho jinsi tulivyotangulia kusema.Wadau, wanataaluma na vinara wote wa kutegemewa watatoka miongoni mwa vijana hawa. Taifa lisilo na vijana ni mfano wa gari bila mtambo au jahazi bila tanga. Ili taifa liwe bora la kutumainiwa, sharti vijana wake walelewe vyema, waelekezwe vizuri, wafunzwe adabu, nidhamu na maadili murua ili waje wawe waaminifu. Katika kuwafunza na kuwaelekeza, vijana wahimizwe kusoma kwa bidii, kwa juhudi na maarifa. Wawe wanyenyekevu na watiifu wa sheria za nchi na mataifa. Wawe na nidhamu miongoni mwao, wazee wao na watu wengine wa kila hirimu. Wasiwe washiriki wa ulevi wowote jinsi ambavyo tunaona katika vituo vya habari na kusoma magazeti kila uchao.

Vijana wanaojulikana kama vijana bora ni wale wenye nidhamu na wingi wa uadilifu na hawarukii mambo ovyoovyo. Humakinika kwa kila walionalo na walisikialo. Hutenda baada ya kutafiti, kuchuja na kuchunguza. Hapo ndipo hufanya na kufuata mambo yaliyo murua tu.

Ujana una vituko na vitimbi. Humfanya mwenye macho akawa haoni ilhali ana macho. Akawa hasikii ambapo anayo masikio yake mawili. Kumbuka, kuharibika ujanani ni hasara na majuto ukubwani, hasa uzeeni. Vijana wote wana jukumu la kuchunga ujana wao sasa maana ujana ni kama moshi ukienda haurudi.

Wazazi wengi siku hizi hushikwa na simanzi wawaonapo watoto wao wanavyotunduka katika kutenda mambo ambayo baba zao hawakudiriki kuyatenda walipokuwa vijana. Wengi wao husingizia kwamba ndivyo walivyo wana wa siku hizi. Kumbe wazazi hao hao wanasahau kwamba wao ndio wamechangia pakubwa kwa kusahau wajibu wao

katika kuwafunza watoto tabia njema, uadilifu na maadili. Ni kweli kwamba vijana wengi wamepotoka sana. Wao hufanya mambo na vituko vya kufedhehesha na kutisha bila kujali wala kutishwa na lolote.Wazazi waliowajibika hawataki lawama za kutowaelekeza watoto wao ziwaangukie ingawa wazazi wa aina hiyo ni wachache mno ikilinganishwa na wasiowajibika. Haifai kamwe kwa wazazi kuacha ama kushindwa kuwafunza watoto wao mwenendo mwema kisha waje kuitupia dunia lawama.

Jambo la kusikitisha ni kwamba ndoa nyingi siku hizi hazidumu kwa hivyo shida huanza nyumbani na hii husababisha wazazi kutengana na watoto wao kwa sababu wazazi wenyewe hawataki kuishi pamoja. Tatizo hili la ndoa kuvunjika limekuwa juu sana nambari ya familia zilizo na mzazi mmoja zimeongezeka mara dufu na huu ni msiba mkubwa sana. Ni kweli kwamba familia hizi ni chanzo cha malezi mabaya. Utagundua kwamba baba amebaki na watoto huku mama amerudi kwao nyumbani au amekodisha nyumba mahali ambapo ni mbali na watoto wake. Au mama amehama na watoto wote wameenda kuishi kwingine bila baba mzazi. Hii inakuwa vibaya kabisa hasa wakati ambapo mambo haya yanatokea na watoto wamefika umri wa kubaleghe. Kwa hivyo wakati ambapo watoto wanaona wazazi wao wakiishi nyumba au miji tofauti, akili zao huchanganyikiwa hata zaidi.

Siku hizi kuna wazazi wengi wanaoishi pekee yao yaani mzazi mmoja na watoto. Ni vigumu sana kulea watoto katika familia iliyogawanyika, na ugumu huo unazidi kuongezeka wakati ambapo inapatikana kwamba kuna mzazi mmoja tu. Pili watu wengi siku hizi pia huamua tu kupata watoto nje ya ndoa na hii imekuwa kama ni mtindo wa kisasa. Watu hawataki kujifunga katika ndoa kwa sababu moja au nyingine kwa hivyo

watoto waliozaliwa nje ya ndoa ni wengi mno ikilinganishwa na wakati wa zamani. Hii pia huchangia kutowapatia watoto wao malezi bora, hasa wanapofika umri wa kubaleghe, mzazi ni mmoja tu wa kike au kiume. Kwa hivyo kama ni mvulana hana baba wa kuiga kama mfano na msichana vilevile hakuna mama katika nyumba wa kuigwa kama kielelezo.

Tatu, vijana hukosa malezi bora kwa sababu wazazi wengi wamechukua muda wao mwingi mbali na nyumbani. Hii ni kwa sababu wengi husingizia masomo ya uzeeni, kazi ambazo wazazi hawa hufanya kama vile biashara za aina tofauti tofauti ambazo hufanya wazazi wahame nyumbani kwa muda, kazi za serikali zinazowatuma viongozi wao nje ya nchi na zingine kukaa ofisini kwa muda mwingi kuliko nyumbani sababu kuu ikiwa ni kutafuta hela. Mambo haya yote yanawatenganisha watoto na wazazi wao. Kwa sababu hii vijana hukosa mwelekeo mwema kutoka kwa wazazi na haya yote huchangia mambo kama kutoendelea na masomo, kujiingiza katika anasa, vijana wa kike kupata mimba zisizo halali, utumiaji wa dawa za kulevya unakuwa katika mstari wa mbele na uhalifu unaongezeka. Ni ukweli kwamba jamii ndio inafaa kulea mtoto lakini ubinafsishaji wa familia umechukua mizizi katika dunia ya sasa na vijana wetu wataendelea kupotoka zaidi.

### 2.3.7 Ukosefu wa Ajira

Kila mtu anapomaliza kozi, matarajio yake makubwa ni kupata kazi. Inakuwa vigumu sana pale ambapo mtu anakamilisha kozi yake vizuri na kupita vizuri, lakini anakosa kazi.Ukosefu wa ajira ni tatizo kubwa sana nchini Kenya na asilimia kubwa

inayooathirika ni vijana kuliko watu wengine. Mwaka wa 2005/06, vijana kati ya miaka 15-19 na 20-24 waliokosa ajira ni takribani kiwango cha asilimia 25 na 24 mtawalia. Kulingana na sensa ya mwaka wa 2009 vijana kati ya umri wa 15-19 na 20-24 kiwango cha ukosefu wa ajira kilikuwa asilimia 15.8 na 13.4 mtawalia. Ukilinganisha kiwango cha vijana wa kiume na kike katika swala la ukosefu wa ajira utagundua kwamba mtindo ni uleule hakuna tofauti iliyoko kati yao.

Ukosefu wa ajira husababishwa na mambo mengi sana nchini Kenya. Hata ingawa serikali ilianzisha mpango wa kazi kwa vijana mwaka wa 2010 lengo lake likiwa kubuni nafasi za kazi katika kila eneo bunge ili kujaribu kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira, lakini bado tatizo hili halijatatuliwa vilivyo maana idadi ya vijana wanaokamilisha shule na kozi nayo inaendelea kuongezeka.

Mwanzo kabisa kinachochangia ukosefu wa ajira nchini Kenya ni mfumo wa elimu unaotumika. Mfumo huo sio mwafaka kulingana na sensa ya 2009 vijana wengi bado wako chini kielimu. Asilimia 62 ambao wana umri wa kati ya 15-34 masomo yao ni chini ya shule ya upili, asilimia 34 wana masomo ya shule ya upili na asilimia moja tu ndio wana masomo ya chuo kikuu.

Tujuavyo masomo ya mtu ndiyo huchangia zaidi katika kuajiriwa kwake kazi na kuifanya ipasavyo. Data nyingine huonyesha kwamba asilimia 40 ya vijana hawajasoma kabisa ama hawakukamilisha masomo ya shule ya msingi. Hata ingawa elimu ni ya bure katika shule za msingi na upili, kuna ukweli kwamba asilimia 14 kati ya watoto milioni 10.6 wa

umri wa miaka 5-14 waliacha shule, asilimia 68 wa shule ya upili kati ya umri wa 14-17 hawakuhudhuria masomo kabisa. Basi hii inaonyesha kwamba vijana kama hawa hawawezi kupata ajira na tatizo hilo litadumu milele.

Elimu nzuri humpatia mtu kazi nzuri, lakini nchini Kenya mfumo wa elimu umebadilika kiasi kwamba la muhimu mno ni kupita mtihani. Kwa hivyo ni jukumu la mwalimu na mwanafunzi kutumia mbinu yoyote ile ili mwanafunzi huyo apite mtihani bila kujua kama mwanafunzi huyo amepata ujuzi au la. Wanafunzi wengine hupita na alama ya ‘A’shuleni bila ujuzi wowote. Hata pale chuoni mambo sio tofauti na yale ya kutaka kupita mitihani. Kazi inapotangazwa kijana huyo hawezi kujitetea maana hajui lolote kuhusu utendaji wa kazi hiyo, anayoyajua ni yale tu ambayo alikuwa akiyasoma vitabuni na kushika kwa ajili ya mtihani; baada ya mtihani kila kitu kinatupwa katika kaburi la sahau.

Tatizo lingine kuhusiana na elimu nchini Kenya ni kwamba mfumo unaotumika hauwapi wanafunzi mwelekeo mzuri kuhusiana na swala la ajira. Utagundua kwamba mwanafunzi anafanya masomo yote yanayofunzwa shuleni hata yale ambayo hatayatumia maishani. Kwa hivyo muda mwingi hupotezwa katika masomo ambayo si muhimu kwa mtoto binafsi. Wakiwa katika shule za upili wanafunzi hawa hawapewi mwelekeo kamili wa kuchagua somo ambalo litamsaidia mbeleni. Labda anachagua tu kwa sababu ya shinikizo la rika lake tu, walimu au hata kuwafurahisha wazazi. Baadaye anakuja kujuta wakati ambapo kosa hilo haliwezi kurekebishwa. Kwa hivyo ni vizuri kuelekeza wanafunzi kwa njia inayofaa. Vijana wengi wameathirika na mfumo huu wa elimu hata

masomo ya chuoni bado ni shida maana baada ya kukamilisha kozi utasikia kwamba bodi ya kozi hiyo hiyo haina habari kwamba chuo hicho kilikuwa na wanafunzi wa aina hiyo.

## 2.4 Hitimisho

Katika sura ya pili, tumejadili dhima ya ushairi katika Jamii, dhana ya vijana na maswala yanayowahusu vijana katika jamii. Katika sura ya tatu tunajadili maswala yenye ulinganifu miongoni mwa waandishi katika *Tunu ya ushairi* na jinsi kila mmoja anavyoyawasilisha.

## SURA YA TATU

## JINSI WAANDISHI WANAVYOWIANA KATIKA DIWANI YA *TUNU YA USHAIRI.*

### 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tumejadili jinsi waandishi hawa wa diwani ya *Tunu ya ushairi* wanavyowiana na kufanana katika kushughulikia maswala ya vijana kwa njia moja au nyingine katika jamii.

### 3.1 Wasia/Onyo

Waandishi wote wanne katika diwani hii ya *Tunu ya ushairi* wametoa wasia kwa vijana katika jamii. Wasia ni maagizo ya mtu kwa watu wengine ambayo anataka yatimizwe. Waandishi wote wanne wameshughulikia hili swala la kutoa ushauri na mwelekeo kwa vijana katika uandishi wao kwa njia mbalimbali.

Mwandishi wa kwanza ambaye ni Andanenga ameshughulikia swala hili la kutoa wasia kwa vijana katika mashairi yake matatu haya ni pamoja na *Fanya Ulizio*, *Kidau na Pendo la pesa.*Katika shairi lake la kwanza *Fanya Ulizio*, mama anatoa ushauri kwa binti yake kuhusu mapenzi. Anamwonya dhidi ya kuleta aibu katika ndoa yake. Mama anamwambia kwamba yeye hataki mapenzi yatakayomletea aibu. Mwandishi anasema haya katika ubeti wa kwanza,

> "Leo nina jambo, nataka kwambia
> Sikiza mrembo, badili tabia
> Mapenzi ya shombo, sitavumilia"

Mama anaendelea kumwambia binti yake kwamba mapenzi ya kweli hayafananishwi na chochote na hayawezi kukopwa kamwe. Jambo la muhimu kuhusu mapenzi ni kuwa na

msimamo wa kuwa na mpenzi mmoja na kudumisha uaminifu. Kwa hivyo mwandishi anazungumzia swala la uaminifu katika ndoa na kusema kwamba ndoa nyingi katika jamii zimevunjika kwa sababu ya ukosefu wa uaminifu.

“ Na wala si haja, wengi kuambata
Mmoja ni tija, ni huyo limbata
Lumbata mmoja, pendo la mashata” (ub.4).

Mwandishi anasema kuwa ni vizuri kijana kufanya uchunguzi mapema kwa jambo ambalo hana uhakika nalo ili apate mwelekeo mzuri utakao mfaa kutoka kwa wenzake na wale waliomzidi umri.

“Kama huyajui, fanya ulizio
Kama hutambui, ulizia wenzio” (ub.5)

Msimamo wa Andanenga katika shairi hili ni kumuonya kijana wa kike na kumshauri kwamba kama ni kuwa na mpenzi basi, awe na mpenzi mmoja maana mapenzi sio mchezo wa paka na panya.

Shairi lingine ni *Kidau,* kidau ni dau dogo na Andanenga ametumia neno kidau kama sitiari kuashiria mtoto mdogo. Mwandishi anasema kwamba kidau kinaenda baharini na tayari nanga imeshakatika. Mwandishi hufananisha kidau na mtoto, na bahari bila shaka huashiria ulimwengu ambao umejaa aina nyingi ya mambo mabaya. Kwa hivyo mwandishi anamwonya kijana ajichunge ili asiteleze maana kuna hatari nyingi duniani na akiteleza kwa sababu nanga imekatika atapoteza mwelekeo maishani. Mwandishi anasema haya katika shairi hili,

“Ndugu upesi kimbia, tenda hima kwa haraka
Polisi maji pitia, kidau kitapasuka
Kidau chapepesuka, kimekatika nangaye” (ub1)

Katika ubeti wa mwisho pia Andanenga anatoa onyo kwa kijana kwa kusema kwamba ni heri abadili tabia yake mapema bila kuchelewa maana dunia imeharibiwa na mambo mengi kama vile anasa, ulevi, wizi na kadhalika. Kijana anaonywa kwamba asipotii ushauri anaopewa basi atakosa msimamo maishani.

"Nakuomba fanya hima, ukichelewa dakika
Kidaucho kitazama, ajizi utapoweka" (ub.7)

Shairi la tatu la Andanenga ambalo linatoa wasia kwa vijana ni *Pendo la Pesa*. Tujuavyo pesa ndio chanzo cha mauti, katika Biblia takatifu kitabu cha Matayo mlango wa 26 kifungu cha 15 Judasi alimsaliti Yesu kwa sababu alipewa hela kidogo tu. Nchini Kenya watu wenye pesa nyingi wamemiliki kila kitu hata wanyonge hawapati haki yao kwa sababu ya umaskini, kwa hivyo hawapewi fursa ya kujieleza na kusema shida zao maana hakuna atakayewasikiliza. Kwa hivyo Andanenga amechukua jukumu la kuonya vijana kuhusu mapenzi ya pesa na kujisahau hasa katika swala la mapenzi. Anasema kwamba pendo linalohusu pesa ni sawa na ufisadi mkubwa na linafananishwa na harufu mbaya sana ambayo inawafukuza watu katika kikao kwa hivyo cha muhimu ni kujiepusha nalo mapema iwezekanavyo kabla ya hatari.

"Pendo la pesa si pendo, mbali nalo jitengee
Pendo lanuka uvundo, mbali nalo lisogee". (ub.1)

Katika ubeti wa nne, mwandishi huyu anaendelea kusisitiza kwamba katika swala la mapenzi, ni mambo mengi ambayo yanahusisha wale ambao wanapendana wanafaa kutimiza ili penzi hilo lisiangamie. Mambo haya ni kama vile kutiana moyo wakati wa shida, kusamehana, kupendana pasipo mahitaji yoyote na n.k. Hii ni sawa na kupaliliwa kwa mapenzi na kuboreshwa kila uchao, kwa hivyo anatoa onyo kwa vijana wajiepushe

na mapenzi ya mali kwa maana mapenzi kama haya si ya kudumu ni sawa na kujibebeza mzigo mzito. Hii inaakisi wazi nadharia tunayoitumia ya uhalisia ambayo inaonyesha wazi mambo yalivyo katika jamii. Watu wengi wamepoteza pendo la kweli na wamekimbilia mali hasa katika ndoa na wengi hujuta maana ndoa hizo hazidumu.

> "Pendo hilo lahaula, ni zigo ujibebee,
> Pendo wawili ni kula, nyama ndimi mnenee" (ub.5).

Mwandishi wa pili ambaye pia ameshughulikia swala la kutoa wasia kwa vijana ni Nyanje. Mwandishi huyu kinyume na wengine ameandika mashairi mengi zaidi kuhusu maswala ya vijana. Hii ndio imetuhimiza zaidi katika kuchagua mashairi yake matano ilhali waandishi wengine tumechukua mashairi manne kutoka kwa kila mmoja. Mashairi ya Nyanje ni pamoja na *Wasia, Wanaume ni wanyama, Malezi mema, Lauzi mwanangu na Wanangu Nawasia.*

Shairi la kwanza ni *Wasia*, katika shairi hili Nyanje anatoa ushauri kwa vijana kwa kuwaambia kuwa wajitahadhari sana na mambo ya dunia maana sio kila kitu wanachoona kinachovutia na kupendeza zaidi duniani ni kizuri kwa maisha yao maana waswahili walisema "si yote yan'gaayo ni dhahabu" huenda ikawa ni hatari kwa maisha yao. Katika jamii vijana wengi husingizia kwamba wametenda jambo fulani kinyume na ilivyostahili kwa sababu ya kutojua. Ndio maana mwandishi huyu anasema kwamba kijana yeyote hafai kusema kwamba hakwambiwa au hakutahadharishwa mapema.

> "Msije juta laiti, mkamba sikuwambia" (ub.1)

Nyanje anaendelea kuhimiza vijana katika jamii wavumilie changamoto zote za ujana hata ingawa ni nyingi.Anaendelea kusema kwamba wakifanya kosa la kuruhusu changamoto hizo ziwatawale basi zitawalemea kiasi cha kushindwa kujinasua. Anasema

kwamba duniani watu wana uzoevu wa kuongea mambo mengi yasiyo mazuri na watu hawa mara nyingi ndio huchangia kupotea kwa maadili kwa vijana hasa shinikizo la rika. Kwa hivyo mwandishi anasisitiza kwamba hata marika wakiongea na kuwashawizi vijana hao vipi na hata wakiwaona kuwa wajinga la muhimu ni kuvumilia na kungoja wakati ufaao. Kwa jumla mwandishi anasema kwamba kujiheshimu ni jambo la maana sana. Mwandishi anasema haya,

> " Kikiki ikaze kamba, ukijana vumilia
> Wakwambe watalokwamba, kwa lolote vumilia"(Ub.7).

Shairi la pili la Nyanje ni *Wanaume ni wanyama*. Kwenye shairi hili anazungumzia wasia wa mama kwa binti yake mpendwa. Mama anaonekana kujuta na kwa hivyo anamwonya binti wake dhidi ya wanaume wote kwa kumwambia kwamba asimwamini na asidanganywe na mwanamume yeyote. Hii ni kwa sababu yeye kama mama wakati mmoja alikuwa kijana na alionywa na wavyele wake lakini hakuweza kustahimili zile changamoto. Alimwambia binti yake kwamba yale aliyoyapitia wakati ule sio tofauti na yale anayoyapitia binti yake wakati huu. Kwa hivyo anazumgumza kutokana na tajriba aliyonayo. Mwandishi anayasema haya katika shairi hilo:

> "Mwanangu u msichana, nakuasa usikile
> Si watu waone vile, wanaume ni wanyama" (ub.1).

Mama anaendelea kumwambia binti yake ajitahadhari na wanafunzi wa shule pia, kwa maana yeye alilemewa na penzi akiwa shuleni baada ya kujihusisha katika uasherati na mwanafunzi mwenzake na kufanya kitendo cha ngono.

> "Na kuna huyo Karisa, mwanafunzi kule shule
> Akiwa hunipapasa, nami pia vilevile
> Mwishowe ikatupasa, tugawe tunda tulile" (Ub. 8)

Mwandishi anasema kuwa matokeo ya mambo haya ni mimba, baada ya kuwa na mimba msichana anafukuzwa shule ilhali mvulana anabaki shuleni na kuendelea na masomo yake kama kawaida. Na ni kweli kabisa mambo sio tofauti na jinsi yalivyo sasa katika jamii hii inaakisi waziwazi nadharia ya uhalisia. Baada ya wanafunzi wa kike na kiume kujamiana, msichana akisha kuwa na mimba yeye ndio anafukuzwa shuleni lakini yule wa kiume anaendelea na masomo. Kwa hivyo ni jukumu la kijana wa kike kujiepusha na mambo kama hayo kabla ya ndoa maana yeye yuko hatarini zaidi. Mwandishi anasema hivi,

> "kuwa ni mjamzito, wamenifukuza shule
> Karisa yu vilevile, angali ywaenda shule".

Shairi lingine la Nyanje linalotoa wasia kwa vijana ni *Lauzi*, *Mwanangu*, katika shairi hili mwandishi ameandika jinsi ambavyo msichana kwa jina Lauzi anapewa ushauri kuhusu mambo ya ulimwengu na mzazi wake. Mwandishi anaanza kwa kumwambia mwanawe awe msikivu mwema yaani asikilize yale yote anayoambiwa kuhusu ulimwengu wa vituko maana ulimwengu una mitego mingi sana kama vile uasherati ambayo vijana wanafaa kujiepusha nayo kabisa. Kwa hivyo ni jukumu la vijana kuvumilia na kusubiri wakati ufaao kwa kila kitu.

> "Ukuapo umaizi, umaizi ulimwengu
> Yasikufike mwanangu, mwanangu nakuusia" ub.1.
> "Ulegezi Usibiri, Usibiri Ulegezi" ub.4.

Shairi la nne la mwandishi huyu ni *Wanangu Nawasia* katika shairi hili mwandishi ameonyesha jinsi ambavyo mzazi anampa mwanawe wasia na mkaza mwana baada ya wao kufunga ndoa. Anamwambia mwanawe katika ubeti wa 3 jinsi ambavyo anafaa kuishi na mke wake na yale mambo ambayo anafaa kuepukana nayo ili ndoa yao ifaulu.

Anamwambia kwamba mtu yeyote ambaye anaingia katika ndoa ni lazima awe tayari kubadilisha mienendo yake hili iwe nzuri. Ni vizuri kuachana na wapenzi wengine na kupenda tu yule ambaye ameamua kumuoa maana ndoa inafaa iheshimiwe. La muhimu kijana anafaa kuelewe kwamba yeye si kapera tena bali ni mume.

> "Kwanza badili fikra
> Wewe hu tena kapera
> Unyumba mekuingia"

Mzazi huyu pia anaendelea kumwelezea mwanawe kwamba, asithubutu kumpiga mkewe kama walivyofanya wazee wa zamani bali ampende kabisa. Kupiga mke ni kinyume na Katiba ya Kenya na kila mwanamke ana haki ya kuishi bila kuchapwa katika ndoa. Anafananisha penzi la vijana hao na tende ambayo ni tamu na hufurahikiwa sana. Mwandishi anasema haya katika ubeti wa 8,

> "Mke hapigwi makonde
> Ni pendo mke mpende
> Kama tunda la mtende
> Unavyolifurahia"

Mwandishi mwingine aliyeshughulikia swala la wasia kwa vijana ni Arege. Mwandishi huyu kama waandishi wenzake ametoa ushauri kwa vijana katika mashairi yake mawili. Shairi lake la kwanza ni *Maisha*. Katika shairi hili anasema kwamba maisha yana sehemu mbili tofauti, yaani sukari na shubiri kwa maana kwamba maisha ni matamu kama sukari na vilevile ni machungu kama shubiri. Hii inategemea jinsi ambavyo mtu anaendesha maisha yake duniani, akiishi vibaya bila tahadhari na kupata ugonjwa bila shaka atajuta. Anasema haya katika ubeti wa 3.

> "Maisha ni karaha , kama bado hukujuwa
> Maisha ni furaha, ikiwa tayapekuwa
> Maisha ni tufaha, kwa wenye kuyaepuwa"

Kwa hivyo mwandishi huyu anatoa ushauri kwa vijana kwamba, maisha sio kitu cha kufanyia mchezo. Ni jukumu la kila kijana kutenda yaliyo mema kwa maana mtu anavuna kile anachokipenda.

Shairi lake la pili linajulikana kama K*izazi.* Shairi hili linahusisha, watu watatu, babu, baba, na kijana. Katika shairi hili baba mzazi analalamika kuhusu tabia mbaya za mwanawe ambazo yeye kama mzazi ameshindwa kukabiliana nazo. Kwa hivyo anaona ni afadhali amujulishe baba yake mzazi hili ampe suluhisho.

Katika ubeti wa 13 mwandishi anasema kuwa, babu anatoa wasia kwa mwanawe pamoja na mjukuu wake, anasema kwamba ni bora baba mzazi kuzungumza na mwanaye kwa kumpa mwelekeo mzuri maana vijana wanahitaji mwelekeo kutoka kwa wazazi wao. Ni kweli kwamba wazazi wengi wamesahau jukumu lao la kuwaelekeza wana wao. Hii ni kwa sababu takribani wazazi wengi wamejihusisha na shughuli nyingi kando na watoto wao na hii imechangia sana vijana kupoteza mwelekeo maishani.Vijana wanapopoteza mwelekeo maishani katika jamii ni dhahiri kwamba jamii hiyo haina viongozi wa kesho na hilo ni jambo ambalo linafaa kuchukuliwa hatua haraka iwezekanavyo.

"Mwanangu nakuusia, mwanao useme naye
Kwa wema kumuelezea, la haki umpatiye
Zako tapojiendea, taifa siangamiye"

Katika ubeti wa kumi na nne mwandishi huyu anasema kwamba, babu anachukua jukumu la kutoa wasia kwa mjukuu wake kwa kumwambia kwamba hakuna mtu duniani ambaye ataishi milele kila mtu ni msafiri. Kwa hivyo si vizuri kufanya mambo yalo mabaya hiyo ni sawa na kujifunga kwa mambo ambayo hayana faida yoyote.

"Nawe mjukuu wangu dunia tu wasafiri
Kufanya yalo machungu, hakuzalishi laheri
Huku ni kujitia pingu, ukawa tumwa wa shari".

Mwandishi wa mwisho anayeshughulikia swala hili la kutoa wasia kwa vijana ni Kiponda. Mwandishi huyu ametumia nafsineni ya mzazi kumwonya mwanawe dhidi ya uasherati, ujeuri, uongo na ufisadi katika shairi *Mwanangu sikubali*. Mwandishi anasema haya,

> "Mwanangu, sherati sikuperembe kukubali"(ub.2)
> "Mwanangu, wajeuri siwe nao, ni shubili" (ub.3)
> "Mwanangu, waongo usiwasifu, kulihali" (ub.4)
> "Mwanangu, wafisadi siwe nao, kemikali (ub.5)

Kibwagizo chake ni *mwanangu sikubali,* kwa hivyo mzazi anachukua jukumu la kumshauri na kumwonya mwanawe dhidi ya kujiepusha na mambo yasiyo mazuri duniani.

Katika shairi la pili la Kiponda linalotoa wasia ni *Dagaa*. Dagaa ni samaki mdogo ambaye anapatikana baharini. Mara nyingi huweza kuliwa kama amekaushwa kwenye jua au hata akiwa mbichi. Dagaa pia ni mtu au kitu ambacho kimedhalilishwa au kudharauliwa. Mwandishi ametumia anwani hii dagaa kimajazi kumfananisha kijana na dagaa. Hii inaonyesha kwamba watu wengi wamemdharau kijana kama mtu mdogo asiye kuwa na busara na hekima na kwa hivyo hana la kusema kwa watu wakubwa. Lakini kulingana na huyu mwandishi anasema kwamba ingawa kijana amefananishwa na dagaa ambaye ni mdogo sana, kwake yeye kijana tayari amepevuka na ni mtu wa maana sana katika jamii ambaye anategemewa kwa kiwango kikubwa na kila mtu. Mwandishi anasema haya,

> "Angawa mdogo, dagaa, amekomaa
> Kanga kidogo, dagaa, atakufaa
> Kalia kinaya, dagaa, h'ondoa njaa" ub.1.

Katika shairi hili anatoa wasia kwa kijana kwa kumwambia kwamba , hata kama yeye ni mtu mdogo katika jamii bado ana mchango mkubwa sana wa kutoa kwa hivyo ajiepushe na mambo mabaya ambayo yatamletea taabu. Ni wazi kwamba kila kijana anafaa awe na msimamo thabiti katika jamii anamoishi ili asinaswe kwenye mitego mingi ya dunia.

"Nasio mzigo, kijana, bado wafaa
Toka kwa mtego, kijana , sinyanyapaa" ub.2.

Mwandishi huyo anaendelea kumhimiza kijana ajitahidi maishani kwa sababu maisha ni magumu hasa kwa mtu yeyote mvivu na mlegevu ambaye anategemea jasho ya watu wengine.

"Chimbua mhogo, kijana, usibung'aa" ub.3.

Mwandishi anaonyesha jinsi nafasi ya kijana katika jamii ilivyo ya muhimu na ni lazima atimize jukumu lake kama kijana maana maishani ni heri kuiga wale wote ambao wamefaulu na kujitenga na wale ambao hawana mbele wala nyuma.

"Maisha ni mwigo, kijana, ushike taa"ub.5.

Shairi la Kiponda la mwisho linaloshughulikia wasia kwa kijana ni *Maisha vidato* .Katika shari hili, wasia wa mwandishi kwa vijana ni kwamba awe mwangalifu na pia awe mtu mwenye busara, asitembee kama mtu mjinga ambaye tayari amepoteza mwelekeo. Anaendelea kusema kwamba maishani hakuna njia ya mkato ni lazima kila mtu apitie vidato vyote vya maisha bila kuchagua kinachomfaa.

Mwandishi anasema haya katika ubeti wa 2,

"Siendi kama kipofu
Asejua aendako
Nenda kwa uangalifu
Makini na hamasiko".

Katika swala hili la wasia, waandishi wametoa ushauri kwa vijana kuhusu mambo yaliyo sawa kama vile kubadilisha tabia na kuwa watu wema, kujiepusha na mitego ya maisha na n.k kwa sababu wao ni watu wa maana sana katika jamii. Kulingana na nadharia ya uhalisia tunayoitumia katika utafiti wetu mambo ambayo waandishi wanazungumzia ni yale ambayo yanaakisi ukweli katika jamii na tunayaona yakitendeka kila siku.

**3.2 Elimu**

Elimu ni mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni, vyuoni na maishani. Katika diwani hii ya *Tunu ya ushairi* waandishi watatu ndio wameshughulikia swala hili la elimu kwa vijana. Ingawa waandishi hawa wanatofautiana jinsi ambavyo wanaliangalia swala hili la elimu, kila mmoja wao angalau amezumgumzia kuhusu kijana na elimu kwa jumla.

Mwandishi wa kwanza ambaye ameshughulikia swala hili ni Andanenga, katika shairi lake *Hili na Lile.* Katika shairi hili mwandishi anasema kwamba ni wazi na kweli vijana katika jamii wamepata elimu, lakini cha kushangaza ni kwamba elimu hiyo haijawasaidia vijana hawa maishani.Hii ina maana kwamba elimu hiyo sio mwafaka kabisa au haina misingi kamili, kwa hivyo Andanenga anazungumza kuhusu ukosefu wa elimu bora kwa vijana. Katika ubeti wa kwanza mwandishi anasema kwamba,

> “Wanambia umesoma, vidatoni umefika
> Hujui baya na jema, kuzama na kuokoka
> Wewe umeelimika, waso elimu wakoje?”

Kama tulivyosema hapo awali ni vizuri kila kijana apate elimu iliyo nzuri na itakayomsaidia maishani, hasaa kwa kupata ajira. Lakini jinsi ambavyo Andanenga anasema ni kwamba vijana katika jamii wamepata elimu lakini mambo wayatendayo ni

sawa na wale ambao hawajasoma kabisa. Kwa hivyo Andanenga anashangaa mambo anayoyaona kwa vijana ambao wanadai wamesoma na anashangaa wale ambao hawajapata elimu kabisa watafanya nini.

Mwandishi wa pili anayezungumzia swala la elimu ni Kiponda katika shairi *Jana si Leo.* Mwandishi huyu ameandika shairi hili kama ngonjera kati ya watu wawili ambao ni bwana Kale ambaye ni mzazi na Kadzo ambaye ni bintiye. Katika shairi hili kuna mvutano kati ya mzazi na bintiye kuhusu swala la elimu. Tulivyoona hapo awali sehemu zingine za nchi hata kama elimu ni ya bure nchini Kenya watoto wengine hawaendi shuleni kwa sababu moja au nyingine. Kwa mfano sehemu zingine kama Kaskazini Mashariki na baadhi ya sehemu za Bonde la Ufa mila na desturi haziruhusu mtoto wa kike kupata elimu, badala yake wanaozwa mapema.

Kwa hivyo Kiponda anatoa picha hiyo wazi katika shairi hili kwa kusema yale yanayopatikana katika jamii tofauti tofauti. Bwana Kale anataka kumwoza bintiye ambaye bado yuko shuleni kama mambo yalivyokuwa wakati wa kale kinyume na yalivyo sasa. Hii ndio sababu Kiponda akaliita shairi hili *Jana si leo* kuonyesha kwamba mambo yamechukua mkondo mpya tofauti na vile mambo yalivyokuwa hapo awali. Cha kushangaza ni kwamba msichana huyu Kadzo ana msimamo thabiti wa kukataa kuolewa maana anataka akamilishe kozi yake kwanza. Baba anamwambia kwamba msichana ambaye ni wa rika lake tayari ameolewa na imebakia yeye tu kuolewa kwa sababu ashapokea mahari kutoka kwa kijana wa mzee Sule. Katika ubeti wa kwanza anasema:-

> "Posa yake iko kwangu, yule shababi Sule"

Hii ina maana kwamba baba amekubali kumwoza binti wake hata kabla ya idhini yake. Lakini kwa sababu Kadzo anajua umuhimu wa elimu na pia anaelewa haki zake kama mtoto. Anamwimbia babake kwa ujasiri na ukakamavu kwamba caha muhimu kwake kwanza ni elimu si ndoa. Na kwa sababu hiyo yeye hayuko tayari kuacha shule ili aolewe. Kwa hivyo hata kama tayari amemea maziwa hiyo si ishara ya kuingia katika ndoa.

> "Baba liwalo na liwe, ndoani sipigi mbizi ub.4"
> Kimila kwetu lazima, mke akimea tezi."
> "Ufunguo maishani, ni elimu si harusi" ub.8.
> "Leo elimu navaa, kesho twavila vinono" ub.9.

Hii inaonyesha kwamba kijana huyu Kadzo kulingana na mwandishi Kiponda anajua na kuelewa haki zake kama mtoto wa kike kwa na kuelewa faida za kupata elimu. Faida hizi ni sawa na kupata kazi nzuri, kuvaa vizuri, kula vizuri n.k hivyo hawezi kushurutishwa na mambo ya utamaduni.

Mwandishi mwingine ambaye ameshughulikia swala hili la elimu ni Nyanje katika shairi lake *Wanaume ni Wanyama.* Katika shairi hili mwandishi amechukua nafsineni mama ambaye anazungumza na binti yake kuhusu uhusiano wa elimu na mambo ya wanaume. Mama huyu anaelekea kujuta maana masomo yake yalikatizwa kwa sababu ya mimba aliyoipata akiwa shuleni kutoka kwa mwanafunzi mwenzake Karisa. Lakini Karisa yeye anaendela na shule ishara kwamba mtoto wa kike yuko hatarini na masomo yake hayatiliwi maanani sana kama yale ya mtoto wa kiume. Anasema kwamba ni vizuri vijana kutii ushauri wanaopewa maana majuto ni mjukuu na huja baadaye. Mwandishi anasema haya katika ubeti wa 8,

"Mwishowe ikatupapasa, tugawe tunda tulile.
Kuwa ni mjamzito, wamenifukuza shule"ub.9.
"Karisa yu vilevile, angali ywaenda shule "ub. 10.

Kwa hivyo katika shairi hili mama anamwonya binti yake Amina dhidi ya wanaume na kumwambia kwamba la muhimu maishani ni elimu mwanzo kisha mengine yaje baadaye. Ni vyema kujua kwamba shule ni mahali muhimu sana kwa watoto maana wakati wao mwingi wanapatikana mikononi mwa walimu. Hii ni kwa sababu walimu hubeba jukumu la kuwaonya wanafunzi wao dhidi ya mimba zisizo halali, magonjwa, ulevi, wizi n.k ndio maana katika ubeti wa sita mwandishi anasema kwamba,

"Mengine kuhusu penzi, mwanangu taonywa shule"ub.6.

Kuhusu swala hili la elimu waandishi wote wanasema kwamba elimu ni kitu cha maana sana katika maisha ya binadamu. Kwa hivyo ni vizuri kila kijana apewe fursa ya kupata elimu ili baadaye aweze kujikimu kimaisha. Katika maisha ya sasa mtu yeyote ambaye hana elimu amekosa kitu muhimu sana maishani. Hii inaafikiana wazi na nadharia ya uhalisia tunayotumia katika utafiti huu maana katika jamii watu wanaendelea kujitahidi kusoma hili waishi maisha ambayo ni mazuri nay a kuridhisha.

### 3.3 Malezi

Malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kufuata tabia na mwenendo unaostahili. Kama tulivyotaja hapo awali familia ni asasi muhimu sana katika malezi ya watoto. Katika diwani ya *Tunu ya ushairi* waandishi wote wanne wameshughulikia swala hili la malezi. Hii ni kwa sababu swala hili ni swala ibuka na wazazi wengi hawajawajibika katika kulea watoto wao. Tulivyoona awali ni kwamba wazazi wengi wanachukua muda wao mwingi

kufanya kazi mbali na nyumbani na kusahau jukumu lao la ulezi. Hii huchangia sana katika maisha ya vijana na husababisha mambo mabaya kama vile uhalifu, usherati, utumizi wa madawa ya kulevya na mimba zisizo halali na n.k. Kwa sababu vijana hukosa mwelekeo mwema kutoka kwa wazazi, ni kweli kwamba vijana hupata mwelekeo kutoka kwa marika wao, wafanyakazi wa nyumbani na katika teknolojia kama vile mtandao, televisheni na hata sinema.

Mwandishi wa kwanza kabisa ambaye ameshughulikia swala la ulezi ni Andanenga katika mashairi yake mawili. Shairi la kwanza ni *Fanya ulizio.* Katika shairi hili mwandishi anasema kwamba mzazi anampa binti yake mwelekeo mzuri kuhusu mapenzi. Katika ubeti wa kwanza mwandishi anazungumza kuhusu mapenzi yaliyo ya adabu na heshima kwa hivyo mzazi anamwambia bintiye kwamba ni lazima abadilishe tabia yake iwe nzuri ili atakapojihisisha na swala la mapenzi.

> "Sikiza mrembo, badili tabia"

Mzazi huyu anabeba jukumu kama mzazi mzuri kumwelekeza msichana wake kwa kumwambia kwamba katika uwanja wa mapenzi lazima uaminifu udumishwe kwa hali ya juu. Hii ni sawa na kusema kwamba ni heshima sana kuwa na mpenzi mmoja tu, sio vizuri kuwa kiruka njia.

> "Na wala si haja, wengi kuambata
> Mmoja ni tija, ni huyo limbata
> Lumbata mmoja, pendo la mashata" ub.4.

Kwa hivyo binti huyu anaelekezwa vizuri na mzazi wake kuhusu swala la mapenzi kwamba kuwa na mpenzi mmoja kuna faida nyingi kama vile kujiepusha na magonjwa ya zinaa.

Shairi lingine la Andanenga linaloshughulikia swala la malezi ni *Hili na Llile.* Katika shairi hili anazungumza kuhusu malezi bora ya wazazi kwa watoto wao. Anasema kwamba ni vyema mzazi kuchukua jukumu la kuwafunza wana wao kwa njia iliyo nzuri. Siku hizi watoto wengi wanalelewa na vijakazi na hii husababisha uvivu au kutojua kufanya kazi za nyumbani kama vile kupika. Naliaka (2012) anasema kwamba, "malezi ni pamoja na lishe, mavazi, makao, elimu pamoja na ushauri". Mwandishi anasema kuwa ni jukumu la kila mzazi kumwonyesha na kumwelekeza mwana namna ya kufanya mambo.

> "Nyama hufunza makinda, jinsi ya nyama kunyaka
> Taalimu ya kuwinda, kupenya mwenye vichaka
> Nasi wazazi hufunda, wana jinsi ya kupika"

Mwandishi wa pili anayezungumzia swala la malezi ni Kiponda katika shairi lake *Mwanangu sikubali*. Katika shairi hili mzazi huyu anachukua jukumu la kumwonya mwanawe kuhusu mambo mbalimbali ambayo vijana hujihusisha nayo. Huyu ni mzazi ambaye angependa mwanawe awe na nidhamu na uadilifu na kufuata mambo yaliyo mazuri tu kwa kumfunza na kumwelekeza ipasavyo. Mwelekeo huu unafaa sana kwa kila kijana kwa sababu dunia imekuwa na mambo mengi ambayo ni ya kupotosha kama vile utumizi wa madawa ya kulevya, uasherati, uhalifu, ubakaji  na mengine mengi. Kwa sababu hiyo ni lazima kila mzazi awajibike kwa kumpa mwongozo mtoto wake.

Katika shairi hili mzazi anachukua jukumu la kumshauri mwanawe dhidi ya uasherati, wajeuri, waongo, wafisadi, waongo na watu wote walio wabaya katika jamii. Haya ni mambo ambayo tunaona kila wakati katika jamii na vijana wengi wameangamia na kupotea kwa sababu ya kuiga marika na yale mabaya ambayo wengine wanafanya. Mwandishi anasema kwamba ni vizuri wazazi wawakanye watoto wao mapema na wajue wale ambao ni marafiki zao maana wengi huhadaa na kupotosha. Katika jamii kuna vikundi haramu ambavyo vijana hujiunga navyo na hii mara nyingi huchangiwa na marika. Kwa hivyo ni lazima kila mzazi ajue mienendo ya watoto wao kabla ya mambo kuharibika.

"Mwanangu, wote walio wabaya, wanadhili"ub.6.

Shairi lingine la Kiponda linalogusia swala hili la malezi ni *Jana si leo,* katika shairi hili mwandishi amezungumzia kuhusu ukosefu wa malezi bora. Hapo awali tulitaja kwamba malezi huhusisha elimu na ni jukumu la wazazi kupeleka wana wao shuleni ili wapate kuelimika. Mzazi yeyote anayemnyima mwanawe elimu ni wazi kwamba anamnyima haki yake na kitu cha maana sana maishani.

Mwandishi anasema kwamba mtoto wa kike ananyimwa masomo, ananyanyaswa na kudhulumiwa vilevile na utamaduni. Hapo awali tuliona kwamba mtoto wa kike anaozwa akiwa na umri mdogo eti kwa sababu ya mila na desturi za jamii fulani. Mwandishi anasema haya, tayari amemwoza bintiye kuonyesha kwamba baba anamkandamiza mwanaye wa kike badala ya kumpa mwongozo mzuri. Mwandishi anasema kwamba ndoa ni kama bahari kubwa ambayo mtu anapoingia anaogelea, kwa hivyo Kadzo anakataa kabisa kuingia katika bahari hilo kinyume na matarajio ya baba yake.

"Posa yake iko kwangu, yule shababi wa Sule"ub.1.

Baba liwalo naliwe, ndoani sipigi mbizi."

Ubeti wa tano baba mzazi anajua umuhimu wa kumpa bintiye elimu lakini anapuuza tu kwa kusema kwamba katika utamaduni wao msichana ni lazima aolewe baada ya kumea matiti. Kwa hivyo anamlazimisha binti yake kuolewa mapema badala ya kuendelea na masomo.

"Kimila kwetu lazima, mke akimea tezi"

Hata hivyo mwisho wa ngonjera hii mwandishi anatoa suluhisho la malumbano hayo. Baba anakubali kushindwa na anakubali ukweli kwamba mambo yamebadilika kinyume na yalivyokuwa wakati wao. Kwa sababu hiyo anamuunga mtoto wake mkono na anakubali aendelee na masomo yake kuliko kuozwa kama alivyokuwa amesema awali. Anajitetea kwa kusema kwamba ajuavyo kusoma ni mila na desturi za kizungu na kwa hivyo kusoma hakuna nafasi yoyote katika utamaduni wa Kiafrika. Lakini kwa sababu mambo yamebadilika hana budi kuungana na wengine na kuunga elimu ya mtoto wa kike mkono.

"Si pendeleo mwanangu, sinione mja muwi
Hizo mila za kizungu, kikwetu hazisitawi
Japo ukweli mchungu, na haki hauchafuwi
Mejua jana si leo, soma yazae matawi" (ub.14.)

Mwandishi mwingine anayezungumzia swala la malezi ni Nyanje. Nyanje amechukua muda wake mwingi kuandika kuhusu malezi katika mashairi yake; haya ni pamoja na '*Wanaume ni wanyama, Malezi mema, Lauzi mwanangu na Wanangu Nawasia.*

Katika shairi lake *Wanaume ni wanyama* mama amechukua fursa kumuelimisha mwanawe Amina kuhusu wanaume. Kama mzazi aliyewajibika hangependa mwanawe

wa kike apitie yale yote ambayo yaliyomkumba katika maisha yake akiwa shuleni. Kwa hivyo anazungumza naye dhidi ya kujiepusha na mitego ya wanaume yaani mambo ya mapenzi kwa jumla, uasherati na anasa. Kwa hivyo katika shairi hili mama anachukua jukumu la kumwongoza mtoto wake wa kike aliye katika umri wa kubalehe. Mwandishi anasema kwamba mama anachukua jukumu la kumwambia binti yake kwamba wanaume watamhadaa kwa kumpa pesa, kuvalia vizuri, kuendesha gari za kifahari kumbembeleza na kumrai. Lakini cha muhimu ni kwamba ameonywa kuhusu hayo yote na kwa hivyo asiwasikize wanaume hao hata kidogo. Pia, asithubutu kufanya mapenzi na wanaume hao walaghai ni vizuri asubiri mpaka aolewe.

> "Ngawa waje na manoti, "Nakupenda"wakwambile
> Wakuvalie makoti, usiwaachie milele
> Hata wapige magoti, wambile mna kelele"ub.3.

Katika shairi la pili *malezi mema*, mwandishi Nyanje anachukua fursa ya kuwaelimisha wazazi kuhusu malezi yaliyo bora. Anasema kwamba malezi mema si ya kumbembeleza na kumdekeza mtoto maana hii ni sawa na kumharibu na kumpotosha kabisa na mwishowe kama mzazi kujuta baadaye kwa kumpoteza njia. Mwandishi anasema haya,

> "Malezi mema si yale,mtoto kumdekeza"ub.1.

Mwandishi huyu anaendelea kuonya wazazi dhidi ya kutaka kuwafurahisha wana wao kwa kuwanunulia vitu vya bei ghali na kuwapa uhuru kupita kiasi. Mzazi ni lazima awe mkali na aweze kumkataza mtoto mambo ambayo ni mabaya kama vile utumizi wa madawa ya kulevya , marika wabaya ambao ni wa kupotosha, anasa na mimba zisizo halali, uhalifu wa aina yote, ubakaji na kuiga mambo yaliyo mabaya katika mtandao na teknolojia kwa jumla.

“Daima usikubali,kuridhi kumpendeza
Lazima uwe mkali,mengine kumkataza
Na wala usikubali, maneno kukuigiza” ub.2.

Katika ubeti wa nne, mwandishi huyu anawaonya wazazi wasiwe wanasikiliza mambo ya watu bila kufanya uchunguzi na kuanza kutetesha mtoto kwa sababu ya makosa fulani. Hii ni kwa sababu watu wengine ni wachochezi tu na wanapenda kuharibu familia zinazoishi kwa furaha. Kwa hivyo ni jukumu la mzazi kuchunguza yale yote ambayo anaambiwa na watu kabla ya kumchukulia mwanawe hatua yoyote ile.

“Mzazi usithubutu, mwanao kumteteza
Uambiwapo na watu, mwanzo alofanyiza
Kuwa na hali ya utu, kadhia kuichunguza”( ub.4.)

Mwandishi anasema haya katika ubeti wa mwisho kwa wazazi, kwamba iwapo mtoto amekubali kuwa amefanya makosa ni bora aonywe na kukosolewa ili asirudie kutenda kosa hilo na apewe mwongozo mwema sio kushutumiwa.

“Iwapo amakusudi, makosa kuyatimiza
Kumrudi huna budi, jukumu kutekeleza
Lau usipomrudi, kosa taliendeleza”.

Shairi lingine la Nyanje linalozungumza swala la ulezi ni Lauzi Mwanangu. Katika shairi hili Nyanje anazungumza mambo mengi kuhusu malezi ya vijana.Haya ni pamoja na maisha duniani, uzembe, magojwa, wizi, ujambazi na ulaghai. Mwandishi anasema haya katika ubeti wa kwanza kwamba dunia ni ngumu sana na hakuna aliye na ujuzi wa kuishi duniani. Na yeyote asiyesikia mambo ya wazazi basi atafunzwa na ulimwengu usiokuwa na huruma ila matatizo makubwa.

“Kisha hulewi ulezi,ulezi wa ulimwengu
Usokuwa na mbawazi, mbawazi ili machungu”ub.1.

Katika ubeti wa pili, mwandishi anazungumza juu ya maisha. Anasema zaidi ni kuishi duniani. Hii ni kwa sababu hakuna anayeweza kupata asilimia mia kwa mia kwa kuishi duniani bila matatizo maana maisha ni changamano. Kuhusu swala la ulezi, mwandishi anamwonya kijana dhidi ya ulaghai na ushenzi, maana akijitia katika mambo haya atajuta baadaye. Kulingana na mwandishi, mzazi wa Lauzi anachukua jukumu la mzazi mwema aliyewajibika na kumwonya mwanawe juu ya maisha magumu na mitego duniani. Anasema kwamba maisha ya dunia ni magumu ukiteleza tu kidogo unapoteza mwelekeo na kwa hivyo ni vizuri kijana ajiepushe na mambo mengi ambayo yatamletea balaa. Ni vizuri watoto kusaidia wazazi wao wakati ambao wanahitaji msaada, kwa hivyo ni lazima wawe tayari kutoa msaada kwa wazazi wao wakati wote.

> "Ewe mwanangu ridhia, ridhia haya malezi" ub.2.
> "Kusaidia wazazi, wazazi hasa mamako"ub.3.

Katika ubeti huu mama anamwambia binti yake Lauzi kwamba yeye kama mzazi amempa ulezi na mwongozo mwema. Kwa hivyo asiwe mtu mvivu kwa kazi maana mtu mvivu hana chake. Anaendelea kumshauri kwamba awe mtoto wa kusikia na kusaidia wazazi wake. Hata hivyo hangependa kumnyima haki yake ya kucheza na kukaa na rika lake, lakini isiwe kwamba muda wake mwingi unatumika hapo. Kwa hivyo mwandishi anazungumza kuhusu umuhimu wa vijana kujitegemea katika kufanya kazi zao maishani. Hii ni kinyume na mambo yalivyo sasa katika familia nyingi, watoto wengi hawajui kazi za nyumbani kwa sababu wazazi wengi hawa na wakati wa kuwafundisha watoto wao. Kazi nyingi aghalabu zinafanywa na vijakazi wa nyumbani na kwa sababu hii watoto wengi hukua tu bila ya kujua kufanya kazi za nyumbani ambazo ni muhimu kama vile

kufua, kupika na zingine. Hapo awali tulisema kwamba watu wa kale walibadilishana mawazo na kufunzana mambo ya hekima.

Wakati huo wavulana walielimishwa na mababu zao ilhali wasichana walielimishwa na manyanya zao. Vijana hawa walifunzwa mambo mengi kama vile kumcha Mungu, uadilifu, heshima, bidii kazini, kunga za ndoa na mengine mengi. Kulingana na mwandishi huyu mambo yamechukua mkondo mwingine katika jamii na ni jukumu la mzazi kumuelimisha mtoto wake. Nyanje anaendelea kushauri vijana dhidi ya ulaghai, udanganyifu, wizi na ujambazi. Anasema kwamba udanganyifu ni kitu ambacho kinachukiza sana katika jamii. Ni jambo la aibu sana ikiwa mzazi hajatimiza wajibu wake wa kumuongoza na kumuelekeza mwanawe.Hii ni kwa sababu mtoto asipoelekezwa vizuri atajiingiza katika mambo mengi ambayo ni mabaya.Haya ni pamoja na wizi,ujambazi na ulaghai. Mwandishi anaendelea kusema kwamba ni vizuri vijana waelewe kwamba mambo yote ambayo wanayafanya yana malipo, kwa hivyo yeyote ambaye anapatikana akifanya uhalifu anauawa bila huruma na kusahulika kabisa. Ni jukumu la kila kijana kujiepusha na mambo kama kama hayo ambayo yanahatarisha maisha ya mtu. Na zaidi ya yote ni lazima kila mtu katika jamii akumbuke kwamba siku ya hesabu ipo,na kila mtu atasimama peke yake mbele ya mwenyezi Mungu na hii inadhihirisha wokovu miongoni mwa vijana.

"Usambe mwana wakora, wakora wanauawa" ub.5.

Shairi la mwisho la Nyanje linalozungumzia ulezi ni *Wanangu nawasia*. Katika shairi hili mwandishi amezungumzia ulezi ambao wazazi wanatoa baada ya vijana kufunga ndoa.Ni jukumu la mzazi kuzungumza na mwanawe baada ya ndoa kwa sababu wengi huingia

katika ndoa bila ya kuelewa wanachostahili kufanya kama mke na mume.Ndoa nyingi siku hizi hazidumu kwa sababu moja au nyingine kama vile,wazazi wamesahau kutimiza wajibu wao wa kuwaongoza wana wao baada ya kuingia katika ndoa. Hii ni kwa sababu wengi huchukulia kuwa hawa ni watu wazima na kusahau kwamba bado ni watoto ambao wanahitaji mwelekeo kutoka kwa wazazi wao.

Pia, wazazi wengi wamefungwa na kazi mbalimbali ambazo haziwaruhusu kupata fursa ya kukaa na wanao.Katika shairi hili mwandishi anazungumzia mambo mengi yanayowahusu vijana waliofunga ndoa. Hii ni pamoja na uaminifu katika ndoa, mapenzi yanayo dumu,kuwajibika kama mume,kujiepusha na watu wabaya na wachochezi, kuwa msiri kwa mambo ya nyumbani na kuwa kielelezo chema katika jamii pamoja na kusamehana.

> "Kwenu isiwepo siri
> Ambianeni dhahiri ule"ub.13

Mwandishi amezungumzia swala la uaminifu katika ndoa anasema kwamba hili ndoa yoyote ifaulu lazima watu wawe waaminifu kwa kuwa na mpenzi mmoja ambaye unamthamini kabisa. Hii ni kwa sababu uaminifu huzuia mambo mengi kama vile magonjwa ya zinaa.

> "Pendo la nje ya ndoa
> Siafiki lina ndoa"ub.9.

Kuhusu upendo, kuwajibika na kusamehana, mwandishi anasema kwamba mwanamke baada ya kuolewa anafaa aonyeshwe mapenzi badala ya kupigwa maana hili ni tendo ambalo limepitwa na wakati.

Mwandishi pia anaonya vijana kuhusu kujiepusha na watu wabaya hasa wale ambao wanapenda kuzungumza mambo ya uongo katika jamii. Anaendelea kusema kwamba watu wengine ni wabaya na wenye wivu na hawapendi kuona familia ya bibi na bwana wanaoishi maisha mazuri kwa hivyo wanatafuta njia ya kuvuruga ndoa hiyo. Pia anasema kwamba ni vizuri waishi maisha ambayo vijana wenzao wanaweza kuiga na iwafae kabisa ndiposa hata wao watamani ndoa.

> “Musiyape usikizi
> Maneno ya wachochezi ub.18
> Iweni kielelezo
> Kwa umma na familia” ub.27

Mwandishi wa nne tena wa mwisho anayezungumzia swala hili la malezi kwa vijana ni Arege.Mwandishi huyu anazungumzia swala hili katika mashairi yake mawili, *Maisha na Kizazi*.Katika shairi la *Maisha* mwandishi anazungumzia jinsi maisha yalivyo magumu duniani.Anachukua jukumu la ulezi na kuwaelimisha vijana katika jamii kwa njia mambalimbali.Anazungumza kuhusu ugumu wa maisha na ndoa. Anasema haya katika ubeti wa kwanza, maisha ni magumu yeyote asijaribu kucheza nayo, kwa hivyo ni jukumu la mzazi kuelimisha mwanawe kuhusu maisha hili kumpa mwelekeo.

Kuhusu ndoa anasema kwamba, maisha sio kitu cha kubahatisha ni lazima kijana afanye uamuzi ulio bora asijute baadaye. Anasema kwamba maisha yanategemea jinsi ambavyo mtu ameamua kuishi maana yanaweza kuwa mazuri vile vile yawe mabaya. Kwa hivyo anasema kwamba maisha yana sehemu mbili tofauti yaani furaha na karaha.

> “Maisha ni karaha, kama bado hukujuwa
> Maisha ni furaha, ikiwa tayapekuwa
> Maisha ni tufaha, kwa wenye kuyaepuwa”ub.3.

Mwandishi anasema kuwa maisha yanaweza kuwa magumu zaidi kwa watu ambao ni wanyonge, wavivu na wajinga, lakini kwa watu werevu yanaweza kuwa mazuri. Kwa hivyo ni jukumu la kijana yeyote katika jamii kuchagua lile ambalo litamfaa na kujitenga na lile ambalo litamdhuru. Ni vizuri pia waelewe kwamba hutegemea sana mambo mengi kama vile elimu bora na maadili.

Amefananisha maisha na jipu kwa kusema kuwa jipu lina muwasho ambao huwezi kufananishwa na kitu chochote na jipu hilo likiiva halina budi kupasuliwa. Hii ina maana kwamba maisha yakienda mrama ni lazima yahitaji kufanyiwa marekebisho ili yabadilike kwa njia iliyo bora. Kwa hivyo ni jukumu la kijana yeyote katika jamii kuamua lile ambalo litamfaa na kulifuata.

> “Maisha ni jijipu, likiwiva lipasue”ub.6.

Shairi la pili la mwandishi huyu ni *Kizazi*. Katika shairi hili baba mzazi ameshindwa na ulezi wa kijana wake na imebidi amuhusishe babu wa mwanawe yaani baba yake. Mwandishi anasema kwamba kijana huyu amejihusisha na mambo yasiyo mazuri kama vile ulevi, utumizi wa dawa za kulevya, uhalifu, ubakaji na n.k. Kwanza kabisa anasema kwamba madawa ya kulevya anayoyatumia yamemletea madhara mengi. Kwanza kabisa yamevuruga akili zao yamefanya baadhi yao vipofu na afya zao zimedhoofika kabisa. Wamekosa heshima na nidhamu na pia wameambukizwa magonjwa ya zinaa hata ukimwi ambayo haina tiba.

> “Mosi ni haya madawa, wasiyoisha kuyala
> Mezifanya lawalawa, utadhani ndo chakula
> Mazuzu wameshakuwa, dawa zishawatawala”ub.1

Mwandishi anaendelea kusema kwamba kwa sababu ya ulevi vijana wamekuwa wezi na wabakaji yaani maadili katika jamii yamezoroteka kabisa. Lakini kijana alalamika na kumsingizia mzazi wake akisema kwamba lawama yote inamwendea mzazi kwa sababu alikosa kumwelekeza mapema na kwa njia ipasayo. Kwa hivyo wazazi wamekosa kuwaongoza wana wao vyema na kwa sababu hiyo wanajiongoza wenyewe bila kujua kilicho kizuri na kibaya ambacho wanafaa kujitenga nacho na matokeo ya hayo yote ni maangamizi.

"Usalama mezorota, watu wote kuwakera
Lo! Ubikira mekwisha, vya wenyewe ametwaa"ub.7
"Wazazi metwachilia, mwongozo tukakosa
Shughuli meng'ang'ania pasiwe wa kutuasa"ub.9.

Mwandishi anasema kwamba, kijana huyu analalamika kwamba hakuna mzazi au mtu ambaye ni kielelezo kwake katika familia au hata katika jamii ambaye anaweza kuiga.

"Hapana hata mmoja, wa mfano kupigiwa
Wamezidisha viroja, binti zao wameowa
Wasiyaone kiwa hoja, mazito haya ingawa"ub.10.

Katika ubeti 12 babu anamlaumu mwanawe kwa kukosa kumwongoza na kumpa mwelekeo mtoto wake na kwa hivyo hapaswi kumkaripia na maneno makali na kumwachilia tu. Mwandishi anasema kwamba mzazi anafaa kumwekea misingi mizuri mwanaye ambayo itamwongoza maishani mwake.

"Mwanangu umesikiya, kilio cha mwanao
Msingi hukumwekeya, wala miliki hanayo
Mebaki kumkemeya, na kumwachia kiliyo".

Kwa hivyo katika ubeti wa 13 babu anamwambia mwanaye kwamba amekosea kutomwelekeza mtoto wake vizuri, kwa hivyo inafaa azungumze naye na kumpa

mwelekeo mwema ili taifa lisiangamie. Pia anazungumzia kuhusu haki ya mtoto ambayo ni lazima kila mtoto apate. Kulingana na katiba ya Kenya watoto wana haki zao na lazima haki hizo zitimizwe. Haki hizi ni malezi mema , makazi, elimu n.k. Kwa kuwapa vijana mwelekeo mwema basi taifa lina matumaini haliwezi kuangamia.

> "Mwanangu nakuusia, mwanao useme naye
> Kwa wema kumuelezea, la haki umpatiye
> Zako tapojiendea, taifa siangamiye".

Swala hili la malezi limezua mjadala mkubwa sana kwa waandishi wa diwani ya *Tunu ya ushairi* na kwa pamoja wanasema kwamba ni kweli wazazi katika jamii wamesahau jukumu lao la kuwaongoza watoto wao hasa wafikapo katika umri wa kubaleghe. Jambo hili kwa kiasi kikubwa limechangia sana katika kuzorota kwa maadili na kusababisha mambo mengi mabaya kama ulevi, magonjwa ya zinaa na n.k. Nadharia ya uhalisia moja kwa moja inaakisi mambo halisi yanayoendelea katika jamii jinsi ambavyo yameshughulikiwa na waandishi katika diwani ya *Tunu ya ushairi.*

**3.4 Ukosefu wa Maadili**

Maadili ni kuwa na mwenendo mwema, kwa hivyo ukosefu wa maadili ni kinyume cha mwenendo mwema.Waaandishi watatu katika diwani ya *Tunu ya ushairi* wameshughulika swala hili la ukosefu wa maadili miongoni mwa vijana katika jamii.Hawa ni pamoja na Nyanje, Kiponda na Arege.Waandishi hawa wameangalia swala hili kwa njia mbalimbali. Mwandishi wa kwanza ni Nyanje ambaye ameshugulikia swala hili kwenye mashairi yake manne. Haya ni pamoja na *Wasia*, *Wanaume ni wanyama, Lauzi mwanangu na Wanangu Nawasia.*

Kwenye shairi la *Wasia*, mwandishi anasema kwamba anasa ni jambo ambalo halifai kabisa na kwa sababu hiyo vijana wanafaa kabisa kujitenga nalo. Katika ubeti wa tano, anasema wale wote ambao waliingia katika anasa hawapo kwa sababu wote wameaga dunia kwa kupata magonjwa yanayoua. Anasema kwamba kuwa na maadili mema huenda sambamba na kumcha Mungu.

> "Wawapi leo madume, anasa walopapia?
> Wamepita ja umeme, leo yao sitoria
> Shime enyi wana shime, bora kumcha Jalia"

Katika ubeti wa 6, mwandishi anaendelea kuzungumzia swala hilo la ukosefu wa maadili kwa kusema kwamba, hakuna faida yoyote mtu apatayo kwa kujiingiza katika mambo yasiyo mazuri ila maangamizi kama vile magonjwa hasa ukimwi na mwisho kifo. Kwa hivyo anawahimiza vijana wote katika jamii kubadilisha mienendo iliyo mibaya hili iwe nzuri na ya kuvutia kwa kila mtu anayekutana naye.

Shairi lingine la Nyanje linaloshughulikia ukosefu wa maadili kwa vijana katika jamii ni *Wanaume ni wanyama*. Kwenye shairi hili mwandishi anaonya vijana dhidi ya kuzurura mitaani na kusema kwamba tendo kama hilo husababishwa na ukosefu wa maadili. Pia katika ubeti huo huo mwandishi anaonya vijana hasa wa kike kwa kufanya mambo kisirisiri kwa sababu matokeo ya hayo yote hayatakuwa mazuri kamwe.

> "Kuzurura mitaani, si tabia njema ile
> Si kwenda vichochoroni, kuwaona kina wale"

Katika ubeti wa nane mwandishi anaendelea kuzungumzia swala la ukosefu wa maadili miongoni mwa vijana. Anasema kwamba kule shuleni marika ni hatari sana kwa hivyo wasichana wajiepushe na mambo ya mapenzi shuleni na wanafunzi wenzao wa kiume na

walimu wa kiume pia ili kukwepa mitego ya anasa. Swala la ngono ni swala ambalo linafaa lingoje hadi pale mtu atakapoolewa.

> "Akawa hunipapasa, nami pia vilevile
> Mwishowe ikatupasa, tugawe tundatulile".

Kushiriki katika anasa ni ukosefu wa maadili katika jamii miongoni mwa vijana. Hili jambo huchangia mambo mengi sana kama vile mimba zisizo halali kwa vijana wa kike. Baada ya mtoto wa kike kushika mimba anafukuzwa shule na masomo yake hukatizwa ghafla na kuharibika akiwa umri mdogo. Kinyume na yule wa kiume ambaye hana mzigo wa kubeba, kwa hivyo anabaki shuleni na kwendelea na masomo yake vizuri. Mwandishi anasema haya katika ubeti wa 9,

> "Kuwa ni mjamzito,wamenifukuza shule".

Shairi lingine la Nyanje ni *Lauzi mwanangu*, katika shairi hili mwandishi huyu anazungumza kuhusu ukosefu wa maadili miongoni mwa vijana. Katika ubeti wa mwisho anasema kwamba tabia ya ulaghai na udanganyifu ni tabia ambayo inachukiza sana. Tabia ya kuiba vitu vya wenyewe na hata mifugo kama vile mbuzi na ngombe ni ukosefu wa maadili. Katika jamii nyingi nchini Kenya hasa upande wa Kaskazini Mashariki kuna wizi wa mifugo na vita kati ya jamii mbalimbali na wanaohusika ni vijana. Hata hivyo kuna vikundi vidogo vidogo ambavyo hufanya kazi ya ulinzi na kuleta usalama vijijini, vikundi hivi ni sawa na *sungusungu* na *chinkororo* kutoka jamii ya Gusii. Mwandishi anasema kwamba mambo ya ulaghai na udanganyifu pamoja na wizi ni mambo ambayo ni ya kuchukiza kabisa na suluhisho la dharura linafaa kupatikana.

> "Ubazazi ni chukizi, chukizi kwetu wakera
> Akawapora wakazi, wakazi wenye mapora
> Usambe mwana wakora, wakora wanauawa".

Shairi la mwisho la Nyanje linalohusu ukosefu wa maadili ni *Wanangu nawasia*. Katika shairi hili Nyanje anazungumza kuhusu ukosefu wa maadili katika mapenzi na ndoa. Vijana wengi wanapofunga ndoa huwa na mapenzi lakini baada ya siku chache penzi hilo linaanza kudidimia. Wakati huu nchini Kenya familia nyingi zinavunjika kwa sababu ya ukosefu wa maadili miongoni mwa vijana waliooana. Hili kuchangia mambo kama magonjwa kuenea hasa ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa, ndoa kuvunjika na kuwa na wapenzi wengine nje ya ndoa yaani "mpango wa kando. Kwa hivyo ni jukumu la hawa wawili kupendana bila kuwa na wapenzi wengine.

Katika ubeti wa 11 mwandishi anakashifu mazoea ya kupiga mke. Anasema kwamba hili ni jambo ambalo limepitwa na wakati kama tulivyosema hapo awali na ni kinyume na sheria.. Anaendelea kusema kwamba jambo kama hili linadhihirisha wazi ukosefu wa maadili maana mke anafaa kupendwa na pendo hilo linafananishwa na tunda la mtende linalofurahiwa wakati wote. Kwa hivyo anaonya vijana kutofuata utamaduni wa babu zao kwa kuwapiga wake wao.

Mwandishi wa pili anayezungumzia swala hili la ukosefu wa maadili ni Kiponda katika mashairi yake mawili *Mwanangu sikubali na Maisha vidato.*

Katika shairi *Mwanangu sikubali,* mwandishi anawaonya vijana katika jamii dhidi ya ukiukaji wa maadili, hii ni pamoja na uasherati, ujeuri, uongo na ufisadi. Mwandishi huyu amepanga beti zake kulingana na jinsi ambavyo anatoa ushauri wake kwa vijana katika jamii. Mwandishi anasema kwamba vijana wanaonywa wasikubali mambo ya watu ambao ni washerati. Katika ubeti wa tatu, mwandishi anasema kwamba ujeuri ni

ukosefu wa maadili vilevile na kwa hivyo ni vyema vijana katika jamii wajiepushe na watu wote wajeuri hili wasije wakaige mienendo hiyo.

> “Mwanangu, wajeuri siwe nao, ni shubili
> Mwanangu, usifwate njia zao, pita mbali
> Mwanangu, ujeuri sera yao, mazohali
> Mwanangu sikubali!” .

Katika jamii yoyote ile watu ambao wanadanganya na kukosanisha watu walioishi kwa amani ni wabaya sana. Mwandishi anasema kwamba ndimi za watu waongo zimepoteza wengi kwa hivyo ni heri kujitenga nao na vilevile wafisadi maana wameangamiza jamii.

> “Mwanangu, wafisadi siwe nao, kemikali
> Mwanangu, tamaa ndo utu wao, si Injili
> Mwanangu, wahepe kila uchao, kiakili”ub.5

Haya yote ambayo mwandishi anazungumzia hapa ni ukosefu wa maadili kwa vijana katika jamii kwa hivyo vijana wanaonywa dhidi ya mambo mengi mabaya ya dunia ambayo ni ya kupotosha.

Shairi lingine la Kiponda ni *Maisha vidato.* Katika shairi hili mwandishi anaandikia vijana kuhusu maisha. Anasema kwamba ili kufaulu maishani haifai mtu kuzurura ovyoovyo kama mtu ambaye hajui aendako huku ni kupoteza mwelekeo maishani. Mwandishi anasema hivi kwa sababu vijana wengi wamepoteza mwelekeo maishani kwa sababu ya shinikizo la rika. Vijana wengi wanawaiga vijana wenzao ambao tayari wamepotoka maishani bila kujua kwamba huu ndio mwanzo wa mauti katika maisha yao. Kwa hivyo mwandishi anasema kwamba ni vizuri kila kijana katika jamii awe mwangalifu na mwenye makini ndiposa aweze kufaulu.

> “Siendi kama kipofu
> Asejua aendako
> Nenda kwa uangalifu”

Mwandishi wa mwisho anayezungumzia swala la ukosefu wa maadili ni Arege. Anashughulikia swala hili katika mashairi yake mawili, *Ule mwamba mkubwa na Kizazi*. Mwandishi huyu anasema kwamba vijana wamekosa tumaini kama viongozi wa kesho kwa sababu ya ukosefu wa maadili. Hii ni kwa sababu wengi wao wamejiingiza katika ulevi na utumizi wa mihadarati na kupoteza mwelekeo. Katika shairi hili, *Ule mwamba mkubwa* Arege anasema kwamba vijana wamekosa maadili maana wamejiingiza kwa mambo yasiyo mema kama vile matumizi ya dawa za kulevya na vileo kupita kiasi kwa sababu ya kupoteza matumaini.

> "Vijana wetu tumaini wamepungua
> Wamebaki kujinywea vidawa
> Na vileo vya mauti
> Na vinywa vyao haikosi
> Mioshi kufuka" ub.1.

Maisha ya vijana katika jamii yamekuwa magumu zaidi na wanaonekana kudhoofika na kuonekana kama wazee zaidi kuliko umri wao. Haya yote huchangiwa na ulevi kupita kiasi miongoni mwa vijana kwa sababu ya kupotoka kimaadili. Kando na ulevi vijana katika jamii wamejiingiza katika wizi na kuombaomba mitaani. Hata wengine wao wamekufa kwa sababu ya mambo haya ambayo ni ulevi na wizi. Wengi wao wameuawa kwa kupigwa risasi na polisi kwa sababu ya wizi na uhalifu.

> "Wamebaki kuiba na nyingi kuwamiminia risasi
> Wamebaki kuomba na nyinyi kuwacheka
> Wamebaki waliokuwa jana na nyinyi mbele mwaenda" ub.2.

Hapo awali tulisema kwamba vijana ni viongozi wa kesho katika jamii. Lakini mwandishi huyu anasema kwamba ni jambo la kuhuzunisha sana maana wakati ambapo

vijana watahitajika kuongoza jamii hawatakuwepo maana watakuwa wamepotelea kwenye ulevi na ujambazi na hata wengine watakuwa tayari wamepoteza maisha yao. Hii yote ni kwa sababu ya ukosefu wa maadili miongoni mwa vijana. Kwa hivyo jamii nzima itakosa matumaini kwa kugonga mwamba na hakuna kijana atakayeweza kuliokoa. Mwandishi anawalaumu viongozi wa jamii kwa kukosa kuwapa vijana mwelekeo na uongozi mwema.

Shairi lingine la Arege linalozungumzia swala la ukosefu wa maadili ni *kizazi*. Katika shairi hili mwandishi anasema kwamba, baada ya kijana kupoteza mwelekeo unaofaa anamlaumu babake mzazi kwa kutompa mwelekeo mzuri. Mbali na hilo kijana anatoa sababu nyingi za kujitetea ambazo zinachangia utovu wa nidhamu, na kusingizia wazazi. Hizi ni pamoja na ukosefu wa ajira na ukosefu wa malezi mema.

> Maishani lijikaza, ‘lema sikuambuliya
> Hata kazi sikuweza, kupata wa kunipeya” ub.4.
> “Uongozi mekwamia, vijana tusishiriki
> Na kazi wamechukua, vyeo kamwe hatushiki” ub. 11

Vijana wanalalamika kwamba maadili ya jamii yamezorota kwa sababu watu wakubwa ambao wanatarajiwa kuwa mfano mwema wa kuigwa wamejiingiza katika mambo

> “Hapana hata mmoja, wa mfano kupigiwa
> Wamezidisha viroja, binti zao wameowa
> Wasiyaone kiwa hoja, mazito haya ingawa” ub.10.

Katika ubeti wa 6 na 7, mwandishi anasema kwamba baba mzazi anaendelea kulalamika kuhusu mwanawe kwa ukosefu wa maadili kwa kusema kwamba, kando na ulevi mwanawe amekuwa mhalifu ambaye anapiga watu ngeta na kuwapora mali  na pia ameanza tabia ya ubakaji.

Katika ubeti wa tano babu anamshauri mjukuu wake kwa kumwambia kwamba ukosefu wa ajira na malezi mema sio tikiti ya kujiingiza katika ulevi, uhalifu, wizi na hata ubakaji. Hii ni kwa sababu ukiukaji wa maadili huleta majuto na vilio ambavyo havina suluhisho. Mwandishi anasema kwamba kujitia katika ulevi ni sawa na kujitia pingu.

Kuhusu swala hili la maadili waandishi wanasema kwamba, ukosefu wa maadili husababisha mambo mengi mabaya ambayo yanaangamiza jamii kama vile wizi, vifo, ulaghai na n.k. Kulingana na nadharia ya uhalisia mambo ambayo husababishwa na ukosefu wa maadili yanadhihirika wazi na huchangia sana katika kuangamiza jamii.

**3.5 Ndoa na Mapenzi**

Ndoa ni makubaliano rasmi ya mwanamke na mwanaume kuishi pamoja kama mume na mke, na mapenzi ni hali ya kuingiwa moyoni na kuthamini mtu zaidi ya mwingine. Katika jamii nyingi nchini Kenya ndoa imeheshimiwa sana na tujuavyo ndoa ni matokeo ya mapenzi.

Katika utafiti huu wetu tumeamua kuunganisha ndoa na mapenzi kama swala moja ambalo linawahusu vijana ambao wamefika umri wa kuoa na kuolewa katika jamii. Kama tulivyosema awali ndoa ziliheshimika katika kila jamii. Katika diwani ya *Tunu ya ushairi* waandishi wote wanne wamezungumzia swala hili la ndoa na mapenzi kama swala ibuka katika jamii miongoni mwa vijana.

Mwandishi wa kwanza anayezungumzia swala hili ni Andanenga katika mashairi yake mawili ambayo ni *Fanya ulizio na Pendo la pesa.*Katika shairi la kwanza *Fanya ulizio*,

mwandishi huyu anawaonya vijana wa kike wabadili tabia maana mapenzi hayahitaji mambo ya kuleta aibu.

Katika ubeti wa pili mwandishi anasema kwamba mapenzi hayafananishwi na chochote maana hayakopwi na yanachohitaji ni uaminifu.Anaendelea kusema kwamba mapenzi hayataki maneno yenye kuudhi au kuchukiza au hata usumbufu. Haya yote yakiingia kwenye penzi la watu wawili basi penzi hilo halina budi kufumuka.

> "Mapenzi ni ladha, iso mithilika" ub.2

Jambo lingine ambalo Andanenga anasema kuhusu mapenzi ni kwamba, katika mapenzi mtu hafai kuwa na zaidi ya mpenzi mmoja kama tulivyosema hapo awali. Watu wengi katika jamii tunamoishi wana mazoea ya kuwa na wapenzi wengi kinyume na Bibilia takatifu na hii imechangia sana katika kuvunjika kwa ndoa nyingi sana. Kwa sababu hii mwandishi anatoa ushauri kwa vijana kwamba ni jambo la busara kuwa na mpenzi mmoja ambaye. Hii ni kwa sababu kujihusisha na wapenzi zaidi ya mmoja huchangia sana kueneza magonjwa kama vile ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa.

> "Lumbata mmoja, pendo la mashata" ub.4.

Kwa hivyo msimamo wa mwandishi huyu Andanenga kwa vijana katika jamii kuhusu swala hili la ndoa na mapenzi ni kupendana kati ya watu wawili tu na kuwa waaminifu katika ndoa ndio penzi litakuwa tamu na la kufurahisha.

Shairi la pili la Andanenga linaloshughulikia swala hili ni *Pendo la pesa.* Katika shairi hili mwandishi anaonya vijana dhidi ya pendo linalohusisha pesa yaani kupenda mtu kwa sababu ya pesa alizonazo.

Katika jamii tunamoishi tunaona haya yakitendeka kila uchao.Pendo la kweli limeangamia na wengi husema tu wanapendana kwa sababu ya pesa bila kujua kwamba hakuna mapenzi ya kweli hapo. Kama tulivyosema hapo awali,vijana wa kike wanawapenda baba sukari na vijana wa kiume wanawapenda mama sukari. Sio kwa sababu marika wao hawapo ni kwa sababu ya kupenda pesa maana baba sukari na mama sukari ni watu ambao wamekomaa na wako sawa kifedha na wengi wao wana kazi nzuri na biashara zilizoendelea vizuri kiuchumi. Kwa hivyo mwandishi huyu anachukua jukumu la kuwatahadharisha vijana kuhusu swala hilo. Anakashifu pendo hilo la pesa katika beti zote nne za shairi hilo akitumia maneno tofauti tofauti kulirejelea .

Katika ubeti wa 1 anasema kwamba pendo la pesa lina harufu mbaya sana na halina faida yoyote kwa mwenye kushiriki. Pendo la kweli lina mvuto ambao ni wa kufurahiwa na kila mtu sio upande mmoja.

Ubeti wa pili mwandishi anasema kwamba pendo hilo lina uvundo na si la kudumu hasa wakati ambapo pesa zimekwisha na anawaonya vijana kwamba wasikubali penzi liwalemee maana ni hatari. Anawaonya vijana kuwa pendo la pesa halina heshima yoyote na huisha wakati wowote hasa pesa zinapoisha.

"Pendo halina kudumu, hadi pesa umwekee" ub.2.

Mwandishi anafananisha pendo la kweli na tunda la mtende ambalo ni tamu kama tulivyoona hapo awali.

Katika ubeti wa sita mwandishi anasema kwamba, kila mtu ana haki ya kuchagua yule anayempenda bila kulazimishwa na yeyote. Anafananisha penzi na ufunguo ambao una kufuli yake maalumu, ufunguo huo hauwezi kufungua kufuli yoyote ila tu ile yake. Kwa hivyo ni sawa na kusema kwamba kila mtu ana mpenzi wake na ni chaguo la kila mtu. Maneno haya ya Andanenga ni kinyume na mambo yalivyokuwa zamani. Katika

tamaduni za jamii nyingi nchini Kenya msichana angeolewa na mtu yeyote bila idhini yake na wengi waliolewa baada ya kupashwa tohara kulingana na utamaduni. Basi Andanenga anasema wazi kwamba mambo hayo yamepitwa na wakati na hayafai kabisa wakati wa sasa.

> "Pendo kwa watu chaguo, lazima nielezee
> Pendo ni sawa funguo, kufuli imngojee"

Mwandishi mwingine anayeshughulikia swala hili la ndoa na mapenzi ni Kiponda. Mwandishi huyu amezungumzia swala hili katika shairi lake moja ambalo ni *Jana si leo* kwa mapana. Kulingana na kichwa cha shairi *Jana si leo* linasema wazi kwamba mambo ya jana ni tofauti na ya leo.

Kama tulivyoona hapo awali kuna baadhi za jamii nchini Kenya ambazo hazithamini elimu ya wasichana. Kwa hivyo msichana badala ya kuenda shule anaozwa akiwa na umri mdogo. Cha kuhuzunisha mno ni kwamba msichana huyu anaozwa kwa mzee ambaye ni rika la babake au hata mzee zaidi. Msichana anaolewa kama bibi wa pili au wa tatu. Hata hivyo mwandishi huyo amepinga mambo haya na kusema kuwa yamepitwa na wakati. Mwandishi amekashifu kabisa ndoa za lazima na mapema za mtoto wa kike. Tukimrejelea mwandishi Andanenga pendo halilazimishwi ni haki ya mtu kuamua mwenyewe kupenda.

Kiponda anasema kwamba baba mzazi anamwoza binti yake kwa lazima kwa kijana wa Sule. Anamwambia kwamba tayari ameshapokea maombi ya kijana huyo ya kutaka kumwoa. Katika ubeti wa tano mwandishi anasema kwamba baba mzazi anafuata mambo ya utamaduni ndio maana anamwambia binti yake kwamba, lile analomwambia si la

maana kwake na haliwezi kubadili mawazo yake. Kwake yeye inaonyesha kwamba utamaduni ndio wa maana sio masomo.

Mwandishi mwingine katika diwani ya Tunu ya ushairi anayeshughulikia swala hili ni Nyanje. Hii inadhihirika wazi katika mashairi yake mawili *Wanaume ni wanyama* na *Wanangu Nawasii*. Katika shairi la kwanza la *Wanaume ni wanyama*, mwandishi ameandika kumwonya mtoto wa kike dhidi ya wanaume walaghai sawa na mwandishi Andanenga ambaye anaonya kuhusu pendo linalohusu pesa. Anasema kwamba wanaume hutumia pesa kuwatongoza wasichana, kwa hivyo ni vizuri vijana wa kike wawe waangalifu na kwamba wajitenge nao. Katika ubeti wa tano mwandishi anasema kwamba mapenzi yaliyo halali ni yale ya hadharani lakini yale ya wanafunzi hayakubaliki kabisa. Kwa hivyo wanafunzi wajiepushe sana na mapenzi ya mapema ambayo huchangia katika kuharibu masomo.

Katika mapenzi kuna mitego nyingi sana kama asemavyo Kiponda lakini ni jukumu la kila kijana kujitahidi ili asilemewe na mapenzi na kuingia katika mitego ya aina hiyo. Mitego hii ni kama anasa na mimba zisizo halali.

> "Ila nikajitahidi, kukwepa mitego ile"

Shairi lingine la mwandishi huyu ni *Wanangu Nawasia*, katika shairi hili mwandishi anaonyesha jinsi mzazi anazungumza na mwanawe baada ya kumuoza kwa mke aliyempendeza.

> " Hivi leo nakuoza,
> Mke alokupendeza
> Hivyo basi nisikiza" ub.2.

Mwandishi anasema kwamba ili kujitayarisha kuingia katika ndoa ni vyema kila mtu agundue kwamba ni lazima mambo mengi yabadilike maana kuingia katika ndoa ni sawa na kuanza maisha mapya kabisa.

"Unyumba mekuingia".ub.3.

Katika ubeti wa tano, mwandishi anasema kuwa katika maisha ya ndoa, ni jukumu la mume kumpenda mkewe na kumpa heshima. Kulingana na Bibilia takatifu kitabu cha mwanzo mlango wa 2 kifungu cha 24 inasema, "mme atawaacha wazazi wake aunganishwe na bibi yake na wawe kitu kimoja".Vilevile kitabu cha Matayo 19 kifungu cha 5 na 6 Bibilia inasema, " Na kwa sababu hii mwanamume atawaacha wazazi wake na kuunganishwa na bibiye na watakuwa kitu kimoja sio wawili tena".

"Nyinyi si tena wawili
Mumeungika kamili
Mfano ngozi na mwili
Ghairi ya jinsia" ub.6.

Anaendelea kusema kwamba mapenzi katika ndoa ni kama mmea unaohitaji kutunzwa kwa kupaliliwa na kuwekewa mbolea. Mmea wowote ule ukiachiliwa bila kutunzwa bila shaka magugu yatamea na utakauka kabisa bila kunyunyuziwa maji. Mwandishi anasema haya,

"Mapenzi kama mmeya
Yatilieni mboleya
Kwa kusafiana niya
Yasije yakawafia" ub.8.

Katika ubeti wa tisa, mwandishi anamwonya kijana aliyefunga ndoa dhidi ya kuwa na pendo lingine la nje ya ndoa yaani 'mpango wa kando' kama ijulikanavyo katika jamii.

Kwa jumla mwandishi anazungumza kuhusu uaminifu katika ndoa kama tulivyoona hapo awali.

Mwandishi Nyanje katika ubeti wa 12 anamwoya kijana wa kiume dhidi ya kuwa mwanaume tu jina na kimavazi. Anasema kwamba ni lazima mwanamume awajibike nyumbani kwake kwa kuwatafutia na kulisha familia yake. Mwandishi anaendelea kusema hivi kwa sababu wanaume katika jamii nyingi wamesahau majukumu yao kama wanaume na wamejitia katika vileo na mambo mengine mabaya ambayo yanavunja familia.

"Mwanangu mume ni kazi
Usiwe mume ni kazi
Kanzu, suti na kofia".

Mwandishi anachukua muda wake pia kuzungumza kuhusu mambo ya nyumbani. Anamwambia kijana wa kike kwamba mambo ya nyumbani mwao yawe yao tu; asiwe yule wa kutangaza mambo ya siri hadharani hata kwa wale ambao hawafai. Ni vizuri azungumze na mumewe amwambie yale yote yalomchukiza na watatue wenyewe.

Baada ya mke kuzungumza na mumewe na mambo bado hayabadiliki, mwandishi anasema kwamba ni bora amwambie mavyaa wake matatizo anayoyapitia ili aweze kumsaidia. Katika maisha ya ndoa ni lazima mume na mke wahitilafiane kimawazo kwa hivyo ni vizuri waambiane mambo yao vizuri kwenye kikao. Mwandishi anasema kwamba ni vizuri pia wawajulishe wazazi matatizo yao ili suluhu ipatikane mapema.

La mwisho kabisa anawaambia kuwa ni vyema wawili hawa yaani mume na mke wawe mfano mzuri kwa vijana, umma na familia hili waweze kuigwa.

"Iweni kielelezo Kwa umma na familia" ub.27.

Mwandishi mwingine anayeshughulikia swala la ndoa na mapenzi ni Arege. Ingawa hajalizungumzia sana anasema kwamba katika maisha ya mwanadamu hasa katika ndoa ni lazima mtu achague yule atakayemuoa mwenyewe maana katika ndoa maisha ni magumu na yana changamoto aina zote. Katika shairi lake *Maisha* mwandishi huyu anasema haya,

> "Maisha ni sumeno, mbele nyuma wakata
> Maisha ni mshono, chagua wa kuukata
> Maisha ni tukano, kilipokea si mata" ub.2.

Katika ubeti wa nane, anamithilisha maisha na sukari kwa kusema kwamba maisha ni matamu kama ilivyo sukari, vilevile ni makali kama shubiri. Kwa hivyo inategemea jinsi ambavyo kila mtu ameamua kuishi.

> "Maisha ni sukari, vivyo hivyo ni shubiri" ub.8.

Shairi lake lingine linalohusu swala hili ni *Vidato vya maisha.* Tujuavyo maishani kuna vidato vitatu ambavyo ni lazima kila mtu apitie, kuna cha kwanza ambacho ni kuzaliwa, kuoa na kufa. Ingawa Arege amezungumzia vidato hivi hajavipanga kwa njia hiyo lakini cha muhimu ni kwamba amezungumzia mapenzi na ndoa kama kidato mojawapo muhimu katika maisha ya mwanadamu,

Anasema kwamba katika maisha kuna "kupenda na kuchukia, kufaulu na kushindwa" hili linadhihirisha wazi kwamba kabla watu waoane kuna kupendana kwanza, kisha ndoa kufuata baadaye. Pia katika haya maisha ya ndoa kuna kufaulu yaani kuishi kwa raha na kuweza kusuluhisha matatizo ya nyumbani vizuri kama familia. Kando na hayo mwandishi huyu anasema kwamba kuna kule kushindwa kustahimili, kwa hivyo Arege anaandika kuwaelimisha vijana kuhusu maisha ya ndoa na mapenzi. Anaendelea kusema

kwamba hili ni jambo ambalo mtu anafaa kujitayarisha kimawazo na fikra kabla ya kuingia.

> "kupenda
> na
> kuchukia,
> kufaulu
> na
> kushindwa".

Kwa hivyo waandishi hawa wana mwelekeo sawa kuhusu swala hili la ndoa na mapenzi ambalo linahusu uaminifu katika ndoa, kuwa wasiri katika mambo ya nyumbani vilevile kuoana kwa hiaari sio kwa kulazimishwa.

### 3.6 Changamoto za Maisha kwa Vijana

Katika jamii vijana wamechanganyikiwa na kulemewa na mambo mengi ya maisha. Maisha yamekuwa magumu kwa sababu kadha wa kadha ambazo tumeziona katika mashairi ya diwani ya *Tunu ya ushairi* na jinsi waandishi tofauti walivyoonyesha changamoto hizo. Maisha ni namna ya kuishi. Waandishi wote wanne katika diwani ya *Tunu ya ushairi* wameshughulikia swala hili la changamoto za maisha kwa vijana. Andanenga katika shairi lake, *Pendo la pesa* anawaonya vijana dhidi ya kulemewa na penzi. (ub 2) Mapenzi kama tulivyoona hapo awali ni hali ya kuthamini mtu zaidi ya mwingine .Lakini mapenzi haya hayafai kulemea mtu kiasi kwamba anakosa kujielewa na kutenda mambo yasiyofaa.Vijana wanapofika umri wa kubaleghe wengi huchanganyikiwa sana na hali hii, na wasipopata mwelekeo mwema basi watalemewa na kuangamia kabisa. Mwandishi anasema haya katika ubeti wa pili,

> "Pendo ninalilaumu, mimi lisinilemee
> Pendo halina kudumu, hadi pesa umwekee".

Mwandishi mwingine anayezungumzia swala hili ni Kiponda. Katika shairi lake *Maisha ni vidato* anasema kwamba ni vyema vijana waelewe kuwa maisha sio kitu rahisi. Anaendelea kusema kuwa maisha yana madaraja mengi na lazima kila mtu afuate madaraja hayo maana hayana njia ya mkato jinsi watu wengi wanavyotaka.

> "Maisha yana vidato
> Si viwili si vitatu
> Hayana njia mkato
> Kama watakavyo watu". ub.1.

Katika ubeti wa pili anawaonya vijana jinsi ya kuishi duniani na kukabiliana na changamoto za ujana. Anasema kwamba sio vizuri mtu kutembea ovyo ovyo bila ya kujua aendako, anafananisha haya na maisha ya kipofu ambaye bila kuelekezwa hawezi kujua mahala pa kwenda.

> "Siendi kama kipofu
> Asejua aendako
> Nenda kwa uangalifu" ub.2.

Kiponda anasema haya katika ubeti wa tatu, kwamba kuna changamoto nyingi maishani yaani dunia ina mambo mengi ambayo ni ya ajabu. Kuna milima ya kupanda na mabonde ya kushuka. Anampa kijana moyo wa kuishi lakini anamwonya kuwa kuishi duniani kunahitaji uvumilivu, bidii, uangalifu na mengine mengi hii ni kwa sababu maisha si mteremko kuna kupanda na kushuka.

Mwandishi mwingine anayezungumzia hili swala ni Nyanje kwenye shairi lake *Lauzi mwanangu.* Mwandishi anawashauri vijana katika jamii kwa kuwaambia kwamba hakuna mtu duniani aliye na ujuzi wa kuishi. Kwa hivyo ni lazima kila mtu apewe mwelekeo na mwelekeo huo ufwate kwa makini kabisa.

"Ukuapo umaizi, umaizi ulimwengu
Kwamba hauna mjuzi, mjuzi wa ulimwengu" ub.2.

Katika ubeti wa pili anasema kuwa chuo kigumu zaidi ni kuishi duniani na hakuna atakayeweza kusema kwamba yeye amefanikiwa kabisa na kwamba hana shida. Mwandishi ansema kwamba ili mtu aishi duniani vizuri ni lazima ajiepushe na mambo ya udanganyifu, ulaghai na uhalifu wa aina yote maana malipo ya haya mambo yote ni kilio na majuto.

"Utaishia kulia, kulia pasipo chozi
Muradi ukijitia, ukijitia bazazi
Dunia kikukalia, lia kutoka huwezi".

Mwandishi anasema kwamba ni vyema kila kijana ajue kufanya kazi ilomhitaji hii ni kwa sababu hata Biblia takatifu inasema kwamba."Yeyote asiye fanya kazi asile".

Mwandishi wa mwisho ni Arege, Arege ameshughulikia swala hili la maisha katika mashairi yake mawili *Vidato vya maisha na Maisha.* Katika shairi la kwanza ambalo ni vidato vya maisha sawa na Kiponda anasema kwamba maisha yana vidato vingi. Vidato hivi vinafananishwa na sarafu ambayo ina pande mbili, na anaendelea kusema kwamba maisha yana sehemu mbalimbali kama vile kichwa na upande wa pili.

Mwandishi huyu anaonya vijana kwamba kuna changamoto nyingi maishani kwa hivyo ni jukumu la kila mmoja kujua ni jinsi gani atakabiliana na kila changamoto. Kwa hivyo ni lazima wajichunge na wajue jinsi ya kuishi bila majuto ya baadaye.

"Vidato
vya
maisha
mithili
ya
sarafu.

Shairi lingine la pili ni M*aisha*, katika shairi hili Arege anasema kwamba maisha yana pande mbili yaani nzuri na mbaya. Anafafanua kwa kusema kuwa maisha ni mazuri kwa yeyote ambaye ameamua kuishi maisha mazuri yasiyo na udanganyifu wowote. Hili linafananishwa na vijana ambao wamejitolea katika masomo na pia wanamwamini Mwenyezi Mungu katika maisha yao. Mwandishi anasema kwamba maisha ni furaha pia ni karaha kama tulivyoona hapo awali. Upande mwingine wa maisha ni kwamba, maisha ni magumu sana na ni safari ambayo kila mwanadamu hana budi kuifuata hata kama ni ngumu.

> "Maisha ni taabu, muhali kuenda mbali" ub.1

Katika ubeti wa sita, mwandishi huyu anafananisha maisha na jipu ambalo ni lazima lipasuliwe pindi tu linapoiva.

> "Maisha ni jijipu, likiwiva lipasue"

Anaambia vijana katika jamii kwamba maisha ni safari ambayo kila mtu hana budi kuifuata bila kuchagua. Na wale ambao wanaweza kujikaza na kuendelea wanafaidika.

Katika ubeti wa mwisho wa shairi hilo, mwandishi anamaliza akisema kwamba maisha yana sehemu mbili tofauti. Kuna sehemu ya kwanza ambayo ni tamu na anaifananisha na utamu wa sukari na vilevile ni kali kama shubiri. Kwa jumla maisha ni changamano hasa kwa vijana wanaokua. Kwa hivyo vijana wanashauriwa kuchagua njia zao vizuri.

> "Maisha ni sukari, vivyo hivyo ni shubiri" ub.8.

## 3.7 Hitimisho

Katika sura ya tatu, tumejadili jinsi waandishi wanne tofauti wa diwani ya *Tunu ya ushairi* wanavyowiana katika kushughulikia maswala ya vijana katika jamii. Maswala haya ni wasia, elimu, malezi, ndoa na mapenzi na changamoto za maisha kwa vijana. Maswala haya yanaonyesha ukweli wa jinsi vijana katika jamii wamekumbana na mambo tofautitofauti ambayo yanahitaji kuchukuliwa hatua na hii inaambatana moja kwa moja na nadharia ya uhalisia ambayo tumetumia katika utafiti wetu.

## SURA YA NNE

## JINSI WAANDISHI WA DIWANI YA *TUNU YA USHAIRI* WANAVYOTOFAUTIANA

### 4.0 Utangulizi

Katika sura ya hii ya nne tumejadili jinsi ambavyo waandishi wanne wa diwani ya *Tunu ya ushairi* wanavyotofautiana katika kuangalia maswala ya vijana katika jamii. Licha ya waandishi hawa kufanana kimawazo katika kushughulikia maswala ya vijana pia wametofautiana kwa kiwango kikubwa. Mwandishi kama Arege ameshughulikia mambo kama ukosefu wa ajira na utumizi wa madawa ya kulevya ambayo ni maswala ibuka katika jamii kinyume na wengine.

Nyanje ni mwandishi mwingine ambaye ameshughulikia swala la magonjwa katika mashairi yake swala ambalo halijatajwa na waandishi wenzake. Mwandishi Andanenga ametofautiana na waandishi wengine maana ni yeye tu ameshughulikia swala la umaskini katika diwani hii.

Kiponda ambaye ni mwandishi wanne na wa mwisho ameandika kuhusu utamaduni ambao umekita mizizi katika baadhi ya jamii nchini Kenya.

### 4.1 Ukosefu wa Ajira

Tulivyoona hapo awali ni kwamba ukosefu wa ajira ni tatizo kubwa sana nchini Kenya na asilimia kubwa inayoathirika ni vijana kuliko watu wengine. Pia tuliona kwamba hali hii husababishwa na mambo mengi sana kama vileo mfumo wa elimu ambao ni duni, kukosa elimu kabisa, ufisadi, ukosefu wa subira na kukosa tumaini miongoni mwa vijana, ukosefu wa mwongozo au mwelekeo mwema na kukosa vielelezo vya kuigwa na

mengine mengi. Arege kama mmoja wa waandishi wa diwani ya *Tunu ya ushairi* anasema kwamba kijana analalamika kutopata ajira hata baada ya kumaliza kozi yake vizuri. Ni kweli kwamba vijana wengi katika jamii wamekamilisha kozi tofauti tofauti na kufaulu vyema lakini wamekosa ajira. Mwandishi anasema kwamba maisha ya vijana yamekuwa magumu hata baada ya kujitahidi kwa uwezo wao. Haya yanadhihirika wazi katika ubeti wa nne.

> "Maishani lijikaza, 'lema sikuambuliya
> Hata kazi sikuweza, kupata wa kunipeya"ub.4.

Mwandishi anasema kwamba vijana katika jamii wanalalamika kutopata kazi kwa sababu nyingi ambazo zinatajwa na Arege katika kazi yake. Mwanzo kabisa katika ubeti wa tisa kijana anawalaumu wazazi wao kwa kuwaachilia na kukosa kuwaelekeza vyema hii husababisha vijana kupotea kabisa. Mwandishi anaendelea kusema kwamba babu anaunga mjukuu wake mkono katika ubeti wa 12, kwa kusema kwamba ni kweli wazazi wamekosa kuwaelekeza watoto wao katika misingi ipasayo. Kwa hivyo sio vizuri wazazi kuwakemea watoto wao na kuwalaumu katika jamii bila kuwapa mwongozo unaofaa.

> "Babu nimekusikia, lakini si langu kosa
> Wazazi metwachilia, mwongozo tukakosa
> Msingi hukumwekaye, wala miliki hanayo
> Mebaki kumkemeya, na kumwachia kiliyo".ub.12.

Pili, mwandishi anasema kwamba vijana wanalalamika kwa sababu hakuna mtu ambaye ni kielelezo kwao ambaye wanafaa kuiga. Walio wakubwa wao wamepotoka kabisa na hawawezi kuwaongoza vizuri.

> "Hapana hata mmoja, wa mfano kupigiwa
> Wamezidisha viroja, binti zao wameowa
> Wasiyaone kiwa hoja, mazito haya ingawa" ub. 10.

Katika ubeti wa 13, mwandishi anasema kwamba ni heri mzazi amwelekeze mwanawe kwa njia iliyo nzuri na ajitahidi katika kutimiza mahitaji yake kwake kama mzazi. Anaendelea kusema kwamba kila mzazi akitimiza wajibu wake basi hakuna jamii ambayo italalamika na kila kijana atakuwa wa maana katika jamii.

> "Mwanangu nakuusia, mwanao useme naye
> Kwa wema kumuelezea, la haki umpatiye
> Zako tapojiendea, taifa siangamiye" ub 13.

Tatu,viongozi wamekatalia uongozini, ufisadi umeenea na wamejinyakulia vyeo vyote. Kwa mfano nchini Kenya, hapo awali wafanyakazi wa serikali walikuwa wanastaafu wakiwa na umri wa miaka 55, lakini sasa wazee hao wameongezewa miaka hadi 60. Hili linadhihirisha kwamba vijana wengi hata baada ya kukamilisha kozi zao hawana mahali pa kwenda kufanya kazi maana zote zimenyakuliwa. Jambo lingine kuhusu ukosefu wa ajira kwa vijana ni kwamba, nchini Kenya ni lazima utoe hongo yaani '*kitu kidogo'* kama inavyojulikana ndiposa uweze kupewa kazi. Vijana wengi hawana njia ya mapato kwa hivyo inakuwa vigumu kupata pesa za kuhonga ili waweze kuajiriwa. Vilevile ni lazima ujue mtu mkubwa serikalini ili upewe kazi. Kwa hivyo wale ambao wanapata kazi ni wale ambao familia zao zinajulikana kwamba zinajiweza kifedha na tujuavyo vijana kama hao ni wachache ikilinganishwa na wale maskini ambao hawana watu wa jamii yao serikalini.

> "Uongozi mekwamia, vijana tusishiriki
> Na kazi wamechukua, vyeo kamwe hatushiki
> Ufisadi ndo metwachia, tukabaki kuhiliki" ub.11.

Katika shairi la pili *Ule mwamba mkubwa* Arege anasema kwamba kwa sababu vijana wamekosa kazi jambo hili limechangia sana katika vijana kupoteza matumaini maishani. Kwa sababu hii wengi wamejiingiza katika mambo yaliyo mabaya ili kuweza kusahau

hali yao. Kwa mfano katika shairi hili mwandishi anasema kwamba vijana wamejiingiza katika utumizi wa madawa ya kulevya pamoja na pombe kwa sababu ya ukosefu wa kazi. Katika jamii vijana wamekuwa walevi chakari kwa sababu wanapoamka asubuhi hawana mahala pakwenda kisingizio kikiwa hakuna kazi.

> **"**Vijana wetu tumaini wamepungua
> Wamebaki kujinywea vidawa
> Na vileo vya mauti
> Na vinywa vyao haikosi
> Mioshi kufuka" ub.1.

Katika ubeti wa pili, mwandishi huyu anasema kwamba kwa ajili ya ukosefu wa kazi vijana wengi hupoteza matumaini na hujiingiza katika ulevi na wizi. Katika ulevi vijana hawa huwa wajinga kupindukia. Tujuavyo katika jamii pombe haramu ni ya bei ya chini ikilinganishwa na ile halali. Vijana wengi hupenda ile inayojulikana kama '*second generation'* kwa maana ni ya bei ya chini hii ni kwa sababu mapato yao ni duni au hata wakati mwingi ni kuomba tu.

> "Wamebaki kuiba na nyingi kuwamiminia risasi
> Wamebaki kuomba na nyinyi kuwacheka"

Kila wakati vijana wanapoiba wengi wao hupoteza maisha kwa kuuliwa na polisi kwa kupigwa risasi au hata kulemazwa na kwa sababu hiyo matumaini ya jamii yanaendelea kupunguka maana wakati ambapo watahitajika hawatakuwepo kamwe.

> "Mtakapofika ukingoni na pembeni kuitwa
> Nahodha watakuwa hawakusalia"

**4.2 Utumizi wa Madawa ya Kulevya na Ulevi**

Arege pia tofauti na waandishi wengine katika *Tunu ya ushairi* anazungumzia swala la madawa ya kulevya na ulevi kwa jumla. Kama tulivyoona awali utumizi wa madawa ya

kulevya na vileo unaeendelea kuongezeka kila kuchao miongoni mwa vijana katika jamii zetu. Kwa mfano nchi ya Kenya imeweka mikakati kabambe ya kukomesha tabia hii lakini bado swala hili ni changamoto kubwa nchini Kenya hasa sehemu za pwani. Kwa hivyo swala hili ni kati ya maswala ibuka katika jamii zetu.

Mwandishi huyo tofauti na waandishi wengine anashughulikia swala hili katika mashairi yake mawili *Ule mwamba mkubwa na Kizazi.* Anasema katika shairi la *Ule mwamba mkubwa* kwamba vijana wengi wamepoteza tumaini maishani mwao na kwa hivyo wamejiingiza katika ulevi na matumizi ya mihadarati. Mwandishi anasema kwamba vileo hivyo vyote ni vya kupeleka mtu kwenye kaburi.

> "Vijana wetu tumaini wamepungua
> Wamebaki kujinywea vidawa
> Na vileo vya mauti" ub.1.

Mwandishi anaendelea kusema kwamba taifa litaangamia maana vijana waliotarajiwa kuongoza wakati wao ufikapo hawatakuwepo maana wote watakuwa wameangamia kabisa sababu ya ulevi na utumizi wa mihadarati.

Vijana wamekosa mwelekeo kutoka kwa wazazi pamoja na viongozi wao. Badala ya kutafutia vijana hawa suluhisho, viongozi wengine wanawatumia vijana hawa kwa kuwanunulia vileo ili baada ya kulewa wawasifu na pia katika kuwauzia madawa ya kulevya wao wakingoja tu pesa. Kwa sababu hii mwandishi huyu Arege anasema kwamba vijana wamebaki kule kule walipokuwa na viongozi wanaendelea kutajirika.

Kwa hivyo katika shairi hili mwandishi analaumu viongozi ambao wanawatumia vijana vibaya katika kujitajirisha na kusahau kwamba vijana hawa ndio matumaini ya jamii.

Katika shairi lake la pili *Kizazi*, mwandishi anasema kwamba baba mzazi alalamika kwa sababu kijana wake ameangamia kwenye pombe na amekosa tumaini naye. Ameshindwa

kulikabili tatizo hili mwenyewe ndio maana anaomba usaidizi kutoka kwa baba yake ambaye ni wa umri wa makamo.

Katika ubeti wa pili mwandishi anasema kwamba madawa ya kulevya ndio yamegeuka chakula kwa vijana hawa katika jamii.Anasema hili kwa sababu muda mwingi vijana hutumia katika kulewa na wanasahau mambo mengine yanayowahitaji. Na kwa sababu hii vijana wengi wamekuwa wajinga maana dawa ndizo zinazowatawala kabisa.

> "Mazuzu wameshakuwa, dawa zishawatawala" ub.2.

Mwandishi anasema kwamba ni vizuri vijana waelimishwe ili wajue kwamba hata ingawa hakuna kazi nchini suluhisho sio kujiingiza kwenye vileo na utumizi wa mihadarati. Hii ni kwa sababu ulevi huu hauna faida yoyote kwa maisha ya mwanadamu ila tu yanafanya mtu mfungwa na mtumwa kwayo.

> "Hiyo mjukuu wangu, tikiti ya vileo
> Wewe wajitia pingu, za utumwa wa vileo" ub.5.

### 4.3 Magonjwa

Vijana wengi wameathiriwa na magonjwa mbalimbali na swala hili la magonjwa ni swala ibuka katika jamii. Mambo mengi sana yamechangia magonjwa kuenea miongoni mwa vijana haya ni pamoja na utumizi wa dawa za kulevya, shinikizo la rika na teknolojia pia kwa kiwango kikubwa. Tulipoona awali ni kwamba kwenye mtandao, runinga na sinema vijana huiga mambo mengi ambayo ni ya kigeni na hili huchangia sana katika kuenea kwa magonjwa.

Magonjwa ambayo tunazungumzia katika utafiti huu wetu ni pamoja na ukimwi na magonjwa mengine mengi ya zinaa. Mwandishi huyu Nyanje anatofautiana na wenzake watatu kwa kushughulikia swala hili. Yeye ameandika mashairi mawili

yanayoshughulikia swala hili katika diwani hii ya *Tunu ya ushairi* kinyume na wenzake watatu. Mashairi yenyewe ni *Wasia na Lauzi mwanangu.*

Katika shairi *Wasia*, mwandishi anasema hivi katika kibwagizo "uonapo vyangaria, tahadhari vitakula". Mwandishi ametumia msemokwa kusema kwamba usione chochote ambacho ni kizuri kutoka nje ukadhani ni kizuri yaani usichague nyumba kwa kuona uzuri wa mlango ni vizuri uingie ndani kwanza.

Anawatahadharisha vijana katika jamii kwa kusema kwamba mtu anaweza kuonekana mzuri na wa kuvutia lakini kilicho ndani yake hakuna anayejua. Anasema dunia imeugua kumaanisha kwamba watu wengi wameathirika na magonjwa na ni vigumu kutofautisha aliyeathirika na asiyeathirika. Ushauri wa mwandishi kwa vijana ni kujiepusha na mambo ya anasa kabisa.

> "Japo aula kushufu, na machoni vyavutia
> Dunia wana dhaifu, yaugua nisikia
> Vijana nawasarifu, falau mkisikia" ub.2.
>
> "Jepusheni na zinaa, mlale penye sheria
> Msije andama baa, makaa kujipalia
> Jepusheni na zinaa, madhara kukadiria" ub.3.
>
> "Ngawa waone wazuri, nadhifu kukuvalia
> Wajimwaie uturi, na mapoda kumichia
> Si mlango nyumba nzuri, ngia ndani shuhudia" ub.4.

Katika ubeti wa tano, mwandishi anasema kwamba wale wote ambao waliingia katika anasa na kujifurahisha hawapo tena maana furaha yao ilikatizwa na vifo. Vifo hivi huja baada ya watu kushiriki kwenye ngono bila kinga na kwa sababu ya kutojali.

“Wawapi leo madume, anasa walopapia?
Wamepita ja umeme, leo yao sitoria
Shime enyi wana shime, bora kumcha Jalia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula”.

Katika ubeti wa sita anaonya vijana kwamba anasa haina faida yoyote kwa mtu kwa sababu baada ya mtu kupata ugonjwa hasa wa ukimwi, na akaendelea na mienendo hiyo mibaya matokeo yake hayatakuwa mazuri kamwe. Katika jamii nyingi nchini Kenya mtu akijulikana kwamba amekufa kwa sababu ya kupenda mwenyewe yaani mienendo mibaya, mtu hudharauliwa hata kama ni maiti.

Shairi la pili la Nyanje ni *Lauzi mwanangu*. Katika shairi hili mwandishi anasema kwamba dunia ni kozi na hakuna anayeweza kudai kwamba yeye amefuzu mia kwa mia yaani anaishi vizuri bila matatizo yoyote. Kozi ni aina ya ndege anayechukua wanyama wadogo, na ndege huashiria dunia kulingana na mwandishi kwa hivyo vijana wasipotahadhari ni rahisi sana kuchukuliwa na dunia kisha kuangamia. Anaonya vijana kwa kusema kwamba wakati utafika ambapo mtu anajuta yale yote aliyoyafanya mabaya lakini atakuwa tayari amechelewa. Na kwa hivyo hata akilia vipi “maji yakimwagika hayazoleki”.

“Chuo kigumu dunia, dunia hii ni kozi
Huwezi mia kwa mia, mia kufuzu huwezi
Utaishia kulia, kulia pasipo chozi
Muradi ukijitia, ukijitia bazazi
Dunia kikukalia, lia kutoka huwezi” ub.2.

### 4.4 Umaskini

Katika jamii tunamoishi watu maskini ni wengi sana kuliko matajiri.Umaskini huu umesababishwa na mambo mengi kama tulivyotaja hapo awali hii ni pamoja na ukame, ongezeko la idadi ya watu, viongozi wafisadi na elimu duni. Mwandishi ambaye

anashughulikia swala hili katika mashairi yake ni Andanenga tofauti na waandishi wengine watatu.

Andanenga anazungumza kuhusu swala hili la umasikini kwa njia tofauti tofauti katika shairi lake *Hili na Lile.* Anatumia maneno haya katika kibwagizo cha shairi hili,*'wewe umeelimika, waso elimu wakoje?'* Mwandishi huyo anashangaa sana jinsi vijana waliopata elimu wanaishi maana maisha yao ni ya kustaajabisha mno.Wengi wa vijana hawa wanaishi maisha ambayo ni ya umaskini mno hata majirani waliokosa elimu huwacheka kwa sababu wanaona kwamba elimu waliyoipata haina faida yoyote kwao. Kwa hivyo wanajiona kwamba wako afadhali sana hata ingawa hawakusoma kuliko wale ambao wamesoma.

"Waso elimu wakoje, nambie siyo dhihaka
Maisha wanaishije, na majirani hucheka
Wewe umeelimika, waso elimu wakoje?" ub.2.

Katika ubeti wa sita, mwandishi anasema kwamba kwa sababu ya ukosefu wa kazi vijana wengi hawawezi kutimiza mahitaji kwa watoto wao ipasavyo.Tujuavyo kila mtoto ana haki ya elimu, chakula, mavazi na matibabu.Kwa hivyo ni jukumu la mzazi kutimiza haya mahitaji yote. Hii ni changamoto kwa vijana ambao ni wazazi kwa sababu hawawezi kutimiza yale yote yanayohitajika kwa sababu ya umaskini.

"Mwanao awe na dhiki, njaa yamsukasuka
Akakuomba samaki, waweza kumpa nyoka?" ub.5.
"Mwana njaa imsete, msaada kwako ataka
Akakuomba mkate, jiwe utampashika?" ub.6

Mwandishi anasema kwamba, kwa sababu ya umaskini hata mavazi yamekuwa ni changamoto kubwa sana kwa watu katika jamii, watoto wanatembea wakiwa wamevaa matambara.

### 4.5 Utamaduni

Utamaduni ni mila au desturi za kundi la jamii fulani. Katika diwani hii ya *Tunu ya ushairi* mwandishi anayeshughulika na swala hili ni Kiponda. Nchini Kenya kuna jamii nyingi na jamii hizi zina mila na desturi tofauti tofauti, ambazo watu wa hiyo jamii hufuata.

Tulivyoona awali ni kwamba jamii zingine kama zile za sehemu za Kaskazini Mashariki na Bonde la Ufa mtoto wa kike hapelekwi shule bali anaozwa akiwa na umri mdogo. Baadhi ya jamii nchini hupasha watoto wao wa kike tohara kinyume na Katiba ya Kenya. Hii yote huchangia swala la dhuluma ya mtoto wa kike na kumnyima haki zake huku utamaduni ukisingiziwa.

Mwandishi huyu Kiponda anatofautiana sana na waandishi wengine jinsi ambavyo anashughulikia hili swala la utamaduni. Katika shairi lake *Jana si leo* kulingana na anwani yenyewe, mambo yaliyopitwa na wakati hayafai kuzingatiwa hivi sasa. Mwandishi anasema kwamba ndoa za lazima na za mapema za watoto wa kike ni swala ambalo limepitwa na wakati na jamii ambazo bado zinashikilia utamaduni huo ni heri ziachane nao. Mwandishi anasema kwamba huku ni kupoteza vijana wa kike katika jamii na kuwaangamiza.

Zamani baba mzazi ndiye alikuwa anapokea posa ya bintiye, kisha anachukua jukumu la kumwelezea tu bintiye jinsi mambo yalivyo. Wakati huo msichana hakuwa na uwezo wa kukataa mambo ya wazazi wake ila ni kukubali tu kinyume na mambo yalivyo sasa, kila mtoto ana haki. Katika shairi hili mwandishi anasema kwamba baada ya baba mzazi

kumlazimisha bintiye kuacha masomo ili aolewe, kwa sababu msichana huyu anaelewa haki zake anakuwa mkakamavu na kumkataza baba yake mambo hayo ambayo yamepitwa na wakati. Anasema kwamba cha muhimu kwake kwanza ni elimu wala sio ndoa. Katika ubeti wa tatu mwandishi anasema kwamba wazazi wengine wamefuata mila na desturi za jamii zao na kwa sababu hiyo wamewapoteza binti wao wengi maana wameacha shule na kuolewa mapema kwa sababu ya utamaduni wa jamii hiyo. Mwandishi katika shairi hili anasema kwamba mzazi anataka binti wake aolewe mapema ili asiharibiwe na wanaume wengine ambao anawaita mwewe.

> “ Uepuke uchafuzi, wa bure uharibiwe
> Shukuru Mungu mwenyezi, kwamba waepushwa mwewe” ub.3.
> Vije mie niolewe, huku nikiacha kozi?
> Sikulini nitolewe, na kuhiniwa na ujuzi:
> Baba liwalo na liwe, ndoani sipigi mbizi” ub.4.

Katika ubeti wa tano, mwandishi anasema kwamba mzazi anayefuata mila na desturi za jamii yake ambazo zimepitwa na wakati anashangaa ni kwa nini binti yake anakataa kukubali kuolewa. Kwa hivyo anaona kwamba mambo ya kusoma ni kupoteza wakati na mali kwa kijana wa kike kwani ndoa ni muhimu kwa maoni yake. Mwandishi pia anasema kwamba katika utamaduni msichana akimea matiti yafaa aolewe katika kipindi hicho kwani hafai kamwe kuendelea na shule.

> “ Ama mwachekesha umma, watoto wa siku hizi
> Kulivumbuka kusoma, basi imekuwa kazi
> Mwasahau kule nyuma, tulokuwa kubarizi
> Kimila kwetu lazima, mke akimea tezi” ub.5.

Ubeti wa mwisho wa shairi hili mwandishi anasema kwamba kile ambacho kinawekewa lawama kulingana na baba mzazi ni utamaduni bali sio wazazi. Wazazi wengi ambao hawajaelimika wanaamini kwamba kusoma kwa vijana wa kike ni mila za kizungu

ambazo hazifai kamwe kufuatwa na Waafrika. Msichana wa kike anafaa kuolewa na mahala pake ni jikoni kulingana na mila na desturi za Kiafrika ambazo tayari zimepitwa na wakati.

> "Si pendeleo mwanangu, sinione mja muwi
> Hizo mila za kizungu, kikwetu hazisitawi
> Japo ukweli mchungu, na haki hauchafuwi
> Mejua jana si leo, soma yazae matawi" ub.14.

## 4.6 Hitimisho

Katika sura ya nne, tumejadili jinsi waandishi hawa wanne tofauti wa diwani ya *Tunu ya ushairi* wanavyotofautiana katika kushughulikia maswala ya vijana katika jamii. Maswala haya ni ukosefu wa ajira, utumizi wa madawa ya kulevya, magonjwa, umaskini na utamaduni. Maswala haya yanaafikiana kabisa na nadharia ya uhalisia ambayo tumetumia katika utafiti wetu. Ni kweli kwamba maswala haya yanadhihirika wazi katika jamii.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii tumetoa hitimisho la utafiti wetu na kuthibitisha haipothesia zetu na mwishowe kutoa mapendekezo kwa watafiti wengine.

## 5.1.0 Hitimisho

Katika tasnifu hii tumechunguza maswala ya vijana na jinsi yameshughulikiwa na waandishi wanne tofauti katika diwani ya *Tunu ya ushairi*.Tumetumia nadharia ya uhalisia ambayo imetuongoza vizuri na imependekeza kazi ya fasihi iwasilishe maisha ya jamii kwa njia ya kweli na katika mazingira ya kawaida.Tumeshughulikia jinsi waandishi hawa wanne wa *Tunu ya ushairi* wanavyofanana na kutofautiana katika kushughulikia maswala ya vijana. Katika sura ya kwanza tumejadili usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na msingi wa nadharia ambao ni uhalisia na mwishowe mbinu tulizozitumia katika utafiti wetu.

Katika sura ya pili tumejadili dhima ya ushairi katika jamii, dhana ya vijana na maswala yanayowahusu vijana katika jamii. Kisha tumeonyesha jinsi waandishi hawa wa diwani ya *Tunu ya ushairi* wanavyowiana katika kushughulikia maswala ya vijana katika sura ya tatu. Baadaye tumeshughulikia tofauti zilizoko kati ya waandishi hawa katika kazi zao katika sura ya nne.

Tumezingatia mashairi yanayowalenga vijana katika jamii kwenye diwani ya *Tunu ya ushairi* kwa kutumia sampuli lengwa na kuchagua mashairi kumi na saba manne manne kutoka kwa kila mwandishi isipokuwa mmoja ambaye tumechagua mashairi yake matano.Utafiti wetu umeonyesha uhusiano wa karibu wa waandishi hawa kimawazo na jinsi ambavyo maswala ya vijana katika jamii ni mengi na yanahitaji suluhisho haraka iwezekanavyo.

### 5.1.1 Madhumuni ya Utafiti

Katika kazi hii tulinuia kufanya mambo matatu. Kwanza tumeonyesha jinsi maswala ya vijana yameshughulikiwa na waandishi wanne tofauti katika diwani ya *Tunu ya ushairi*.

Pili, tumetathimini mwelekeo wa waandishi katika diwani ya *Tunu ya ushairi* na kugundua kwamba wana mielekeo iliyo sawa katika kushughulikia maswala ya vijana katika sura ya tatu.

Tatu, tumechunguza jinsi waandishi hawa wanne wa mashairi katika diwani ya *Tunu ya ushairi* wanavyotofautiana katika kushughulikia maswala ya vijana.Haya tumeyashughulikia katika sura ya nne.

### 5.1.2 Matokeo kuhusu Nadharia Tete

Baada ya kufanya utafiti wetu tuligundua kwamba ni kweli vijana katika jamii tofauti huwa na changamoto sawa. Pia makisio yetu kuwa waandishi wote katika diwani ya *Tunu ya ushairi* wana mwelekeo sawa na uhusiano wa karibu sana kimawazo kuhusu vijana. Tunasema hivi kwa sababu ni kweli maswala wanayoyashughulikia ni maswala ibuka katika jamii na yanawahusu vijana. Pia tumethibitisha kwamba waandishi hawa katika

diwani ya *Tunu ya ushairi* wanatofautiana kwa njia moja au nyingine katika kushughulikia maswala ya vijana.

## 5.2 Mapendekezo

Kila mhakiki ana uelewa tofauti na mwingine, hivyo ningewaomba wahakiki wengine walinganishe na kulinganua kipengele mojawapo kwa mfano elimu na wajikite katika fasihi ambayo ni riwaya, tamthilia au hadithi fupi. Pia, wahakiki wengine wanaweza kushughulikia fani katika diwani hiyo ya *Tunu ya ushairi* kwa kujikita katika mwandishi mmoja badala ya wote jinsi ambavyo tumefanya katika utafiti wetu.

## MAREJELEO


Arege,T. (2013) *Tunu ya Ushairi*. Nairobi: Oxford. University Press

Becker, Eva (2011) 'Youth Rights in The Kenyan Constitution'.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Uppsala Sweden. (Haijachapishwa)

Brown, B.B, Larson, R.W (Eds) (2002) *The World's youth adolescence in Eight Regions of the Globe*: United Kingdom. Cambridge University Press.

Erikson, H. E. (1961) *Youth Change and Challenge.*New York: America Academy of Art and Science.

Chacha, N. C. (1980*)* 'Uhakiki wa Ushairi wa Abdilatif Abdalla'. Tasnifu, Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

--------------- (1986) *Mazingira ya Mwanamke katika Fasihi ya Kiswahili*: Rosa Mistika wa Kezilahabi,' Katika Mwamko.

Gazeti la " *The standard*" tarehe 12-08-2015.

Government Printers, (2010) *Katiba ya Kenya*, Nairobi.

Iribemwangi,P.L.(2007) *Alidhani Kapata na hadithi Nyingine.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Kaaru, M.G. (2008) *Daftari la Ushairi*. Kwa Mwanafunzi wa Shule ya Upili: Oxford University Press

Kezilahabi, E (1971) *Rosa Mistika*. Nairobi: KLB

…………….(1974) *Kichwamaji.* Nairobi: East Africa Publishing House.

Kenya Bureau of *Statistics Census* (2009)

Kiongera K.J. (2010) 'Mchango wa Vijana katika Mabadiliko Chanya katika Tamthilia Nne za Kiswahili'.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

Kingei, G. K. na Kemoli, A. (2001) *Taaluma za Ushairi.* Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

King'ei, G. K. na Kisovi, C. M. (2005) *Msingi wa Fasihi Simulizi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kimani, N. na Chimerah, R. (1999*) Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Lugano, R.S. (1989) 'Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi'.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

Mamuya, S.J. (1974*) Ujana*. Nairobi: Kenya Ritho Ltd.

Mazrui, A. na Syambo, B. K. (1992) *Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi. East African Educational Publishers.

Mbatia, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishers.

………… ( 2006) *Migogoro*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mberia, K wa (1997) *Natala*. Nairobi: Marimba Publications.

……………… (2001*) Kifo kisimani*. Nairobi: Marimba Publications.

…………......( 1999) *Maua kwenye jua la asubuhi.* Nairobi: Marimba Publications.

Mohamed, S.A. (2000) *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Nairobi: Oxford University Press.

Momanyi, C. (2006) *Tumaini.* Nairobi: Vide~ Muwa Publishers.

Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugenda, O. & Mugenda, G. (1999). *Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press

Mungania, B. (1985) 'Maudhui mbalimbali katika Ushairi wa Mathias E. Mnyampala'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

Murono, S.E. (2005) *Tadubiri za Insha.* Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Mutua J. (2007) 'Mtazamo wa Vijana na Wazee kuhusu ukombozi wa Mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili'.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Naliaka, R. (2012) 'Hali ya Vijana katika Riwaya ya Vipanya vya Maabara'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkonge, G. (2006) 'Athari za Udhanaishi katika Kichwa Maji na Nguvu ya Sala'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

Obore, E.M.(2012)`Dhuluma Dhidi ya Vijana wa Kike Katika Riwaya ya Rosa Mistika'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

Robert, S. (1952*) Adili na nduguze*. London: Macmillan.

…………( 1952) *Utenzi wa Hati*. London: Macmillan.

Shitemi, N. L. (2010) *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini.* Nairobi: Oxford University Press

Stanford University (14 March 2011*)."The Definition of Morality".Stanford Encyclopedia of Philosophy*. Stanford University. Retrieved 22 March 2014.

TUKI (2006) *English – Swahili Dictionar*y. Dar es Salaam:

____(2010) *A Standard Swahili – English Dictionary*. Nairobi: University Press.

___ (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

UNICEF. *Education Program:Rice University/ Human Development in Global and Local Communities,* Section 2 (Spring 2014) "Kenya: Statistics"]. Retrieved 20 March 2014.

Wafula, R. (1999) 'Uhakiki wa Tamthilia tatu kuhusu wahusika Vijana'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

Wafula, R. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation

Wamitila, K.W. (2001) *Nguvu ya Sala.* Nairobi: Longhorn Publishers.

______(2002) *Uhakiki wa Fasihi Msingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers

_____( 2003) *Pango.* Nairobi: Focus Publishers.

______ (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

_____ (2008) *Kanzi ya Fasihi Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide~muwa Publishers Ltd

Watuha, A. (2011) 'Maudhui ya Waadhi katika Utenzi wa Adili'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Werner, A. & Hichens, W. (1934*) Utendi wa Mwanakupona. The Advice of Mwanakupona upon wifely Duty.* Medstead: Azania Press.